**7 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 7 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

Naibu Spika *(Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI– KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. LEAH J. KOMANYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na Mheshimiwa Leah umependeza leo. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda.

Na. 544

**Kujenga kwa kiwango cha lami barabara zinazopita vilima vikali**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara za vijijini zinazopita katika vilima vikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali ilitenga fedha shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa barabara kilometa mbili kwa kiwango cha lami katika Kilima Kikali wa Miyuyu - Ndanda na kazi imekamilika. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, shilingi milioni 825 zimetengwa kwa ajili ya kujenga kilomita mbili za lami, kilometa mbili kwa kiwango cha changarawe na kujenga daraja dogo *(box culvert)* moja katika kilima hicho ambapo kazi hizo zinaendelea kutekelezwa na zimefikia asilimia 52.2 ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 jumla ya shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kilometa moja kwa kiwango cha lami katika kilima kikali cha Miyuyu-Ndanda na kiasi cha shilingi milioni 300 kimetengwa kujenga kilometa 0.5 kwa kiwango cha zege kwenye eneo la kilima katika Barabara ya Malatu Juu – Mnauke – Mitahu - Mkululu yenye urefu wa kilometa 16.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TARURA* imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kufanya usanifu na kujenga barabara zenye changamoto ya vilima vikali kwa kiwango cha lami kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha kwa kila mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwanza tunaishukuru lakini nataka kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ili barabara hii ilete ile tija ambayo imekusudiwa ni vyema ikakamilika kwa haraka ili kunusuru maisha ya wananchi pamoja na mali zao. Ni upi sasa mkakati wa Serikali wa kuhakikisha barabara hii inatengewa fedha za dharura ili iweze kukamilisha ujenzi kwa haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, jiografia ya Wilaya ya Newala kila upande ambao utaingilia unakutana na vilima vikali. Kwa mfano Nadimba Chiwata, Mikumbi, Mpanyani, Mkoma II Chimemena, Lihanga Chikalole. Ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba barabara hizi ambazo nimezitaja zinajengwa angalau kwa kiwango cha changarawe? nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mtanda la kwanza la mpango wa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekwishakusema katika majibu yangu ya msingi kwamba Serikali katika mwaka wa fedha huu ambao tupo sasa tumeutekeleza ilitenga shilingi milioni 825 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Mwaka wa fedha tunaoenda kuuanza mwezi Julai 2023/2024 *TARURA* imetenga shilingi bilioni moja na tayari bado matengenezo haya yanaendelea na yapo asilimia 52.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuhakikisha kwamba hii bilioni moja inaenda haraka katika Jimbo la Newala Vijijini kwa ajili ya kutekeleza kipande cha barabara ambacho kimetengwa kwa utekelezaji wake ili wananchi waweze kupita kwa sababu barabara hii inaunganisha Jimbo la Ndanda na Jimbo la Newala Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Mtanda wamekuwa wakifatilia sana barabara hii. Nikienda kwenye swali lake la pili la barabara hii ambayo inapita Nandimba, Chiwata ambayo inatoka Newala Vijijini kuelekea Masasi tutaendelea kutafuta fedha na kutenga fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hii na kipaumbele kikiwa katika maeneo ya vilima vikali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Francis Koka Mbunge wa Kibaha.

Na. 545

**Kuupa hadhi ya Manispaa Mji wa Kibaha**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaupa hadhi ya Manispaa Mji wa Kibaha ambao ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri huanzishwa au kupandishwa hadhi kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2014 ambapo umeainisha vigezo na taratibu zinazopaswa kufuatwa ili kuanzisha na kupandisha hadhi halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aprili, 2023 Halmashauri ya Mji Kibaha iliwasilisha ombi la kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Manispaa. Maombi haya yamepokelewa na yatafanyiwa kazi kwa kuzingatia vigezo vilivyopo.

**NAIBU SPIKA:** Daktari Alice Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeridhika na majibu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tunaendelea Mheshimiwa Reuben Kwagilwa Mbunge wa Handeni.

Na. 546

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kwamagome – Handeni Mjini**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Kwamagome?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kwagilwa

Reuben Nhamanilo, Mbunge wa Jimbo la Handeni Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, Halmashauri ya Mji Handeni, ilitengewa shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati ya Kwamagome na mwaka wa fedha wa 2021/2022 shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati ya Kwaluwala katika Kata ya Kwamagome.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshatoa jumla ya Bilioni 117 kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya ya Msingi kwa ujenzi wa vituo vya afya kwenye Kata za kimkakati kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga pamoja na wataalam wa Ofisi ya Rais (TAMISEMI), watafanya tathmini ya kina kuhusu kata hii na mara fedha zitakapopatika Kituo cha Afya katika Kata ya Kwamagome kitajengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwenye swali langu la msingi. swali la kwanza ni lini sasa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga kwa kushirikiana na hao wataalam wa TAMISEMI uliowasema watafanya tathmini hiyo ya kujenga kituo cha afya pale Kwamagome?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ahadi hii ya ujenzi wa kituo cha afya ilifanywa kwenye mkutano wa hadhara na Waziri wa TAMISEMI.

Je, uko tayari baada ya Bunge hili la bajeti tuambatane mpaka Kata ya Kwamagome ili ukawaeleze wananchi kwa nini ahadi hii haijatekelezwa kwa miaka miwili tangu imetolewa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kwagilwa hili la kwanza la Ofisi ya Mganga Mkuu lini itaenda na hii timu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Naomba nitumie Bunge lako hili Tukufu kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga pamoja na timu yetu ya tathmini iliyopo Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhakikisha wanafika katika Halmashauri ya Mji Handeni na Kata ya Kwamagome kwa ajili ya kufanya tathmini na kuona kama idadi ya watu inayohitajika na ukubwa wa kata ile vinakidhi vigezo vya kupata kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba nisisitize wafanye hivyo mara moja huku wakiwasiliana vilevile na Mheshimiwa Kwagilwa ili aweze kuwepo kwa niaba ya wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pii nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Kwagilwa kuweza kufika Kata ya Kwamagome.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mrimi jiandae Mheshimiwa Noah.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Kemgesi pamoja na Ligicha Wilayani Serengeti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni majuzi tu ambapo tulikaa na Mheshimiwa Mrimi aliwasilisha maombi haya katika Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya kituo cha afya Kemgesi na kadiri ya upatikanaji wa fedha tutahakikisha Mheshimiwa Mrimi kule wanaserengeti wanapata kituo hichi cha afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Noah.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu jiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, lini Serikali itajenga vituo vya afya kwenye Kata za Bwawani, Bangata, Kidina, Otoroto na Kimnya kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu kuweza kuona kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya hivi ndani ya jimbo lake na pale ambapo fedha imetengwa tutahakikisha inaenda mara moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo hivi vya kata.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Sangamwalugesha Wilaya ya Maswa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaanza ujenzi wa vituo hivi vya afya ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge Wilayani Maswa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea na wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Kanyasu.

Na. 547

**Kulinda viwanja vya michezo mashuleni**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kupata viwanja vya michezo na kuvilinda kwani baadhi ya shule zimetumia kujenga madarasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Costantine John Kanyasu, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya vigezo vya kuanzishwa shule ni pamoja na uwepo wa viwanja vya michezo. Michezo ni muhimu kwa kuwa husaidia kuimarisha afya za wanafunzi na kujenga akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) itafuatilia jambo hili na kujiridhisha, endapo kuna shule ambayo imetumia viwanja vya michezo kujenga madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule pamoja na Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia kanuni na taratibu zote zinazohusu usajili na uendeshaji wa shule ikiwa ni pamoja na kulinda miundombinu iliyopo shuleni kama viwanja vya michezo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa club nyingi ambazo zinaanzishwa hapa nchini zimekuwa zikitumia maeneo ya taasisi ambayo sasa

hivi ni machache na sehemu zingine hakuna kabisa. Ni upi mkakati wa Serikali wa Kitaifa wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na maeneo ya *public* ambayo ni *theme* ya michezo mbalimbali nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili hivi karibuni Serikali ilitangaza ajira za walimu takribani 15,000. Nataka kufahamu katika idadi hiyo ya walimu ni walimu wangapi wenye taaluma ya michezo ambao wamechukuliwa kwa taaluma yao na kupelekwa kwenye halmashauri kama ajira ya Serikali? Nakushuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kanyasu la kwanza nini mkakati wa Serikali kuwa na maeneo yake ya michezo na kuacha kutegemea taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumeona mbele ya Bunge lako hili Wizara ya Michezo ikipitisha bajeti yake na tayari kwa mfano hapa Dodoma wana mkakati wa kujenga uwanja pale katika eneo la nane nane ambalo litakuwa linamilikiwa na Serikali. Katika mikoa mingine vivyo hivyo wameendelea kuweka mpango kwa ajili ya kuwa na maeneo ya wazi na tutashirkiana na wenzetu wa Wizara ya Michezo kuona ni namna gani tunaweka kipaumbele hicho katika kujenga maeneo haya ili wanafunzi waweze kufanyia mazoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili kwenye idadi ya walimu walioajiriwa hawa hivi karibuni ni wangapi ni walimu wa michezo. Nitakaa na Mheshimiwa Kanyasu ili kuona katika orodha hii ya majina ambayo hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ametangaza ni walimu wangapi ambao wameingia wa kada ya michezo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Moshi Kakoso.

Na. 548

**Ujenzi wa Daraja la Mto Mnyamasi**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Mto Mnyamasi ili Barabara ya Kambanga-Ifinsi hadi Bungwe iweze kutumika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto wanayopata Wananchi wa Kijiji cha Kambanga-Ifinsi wakati wa kuvuka Mto Mnyamasi na inaendelea kufanya jitihada mbalimbali kukabiliana na changamoto hiyo. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali kupitia *TARURA* imetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo. Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 11 Mei, 2023 na Mkandarasi yupo kwenye hatua ya maandalizi ya kuanza kazi ambayo inatarajiwa kukamilika Februari, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa kufanya jitihada za kupeleka mradi hasa wa ujenzi wa Daraja la Mto Mnyamansi. Kwa kuwa eneo la Ifinsi kwenda Kijiji cha Bugwe hakuna mawasiliano ya aina yoyote. Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hiyo ili iweze kuwasaidia wananchi kwenye eneo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili tunatambua jitihada za Serikali zilizofanywa, mmefungua barabara ya Kamibanga hadi Ifinsi, Majalila hadi Ifinsi lakini barabara zote hizo zilizofunguliwa hazijawekewa molamu na madaraja. Ni lini Serikali itaanza kujenga na kuboresha barabara hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kakoso. La kwanza juu ya mpango wa ujenzi wa barabara hii ya Ifinsi – Bugwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba barabara hii haikuwepo na ilikuwa wananchi hawa wanakaa kwenye kisiwa kipindi ambapo mvua zinanyesha. Tayari baada ya utengaji huu wa bajeti ya 1.5 billioni, Serikali pia katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imetenga kiasi cha shilingi milioni 475 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha changarawe kwenye vipande korofi na kuweka mifereji katika maeneo mbalimbali ya barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili lla Barabara za Kambanga – Ifinsi na maeneo mengine aliyoyataja Mheshimiwa Kakoso tutakaa naye Mheshimiwa Mbunge na kuona ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya ukarabati na kuweka kifusi katika barabara hizi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Mwamkulu – Kakese hadi Misunkumilo yenye kilometa 30 kwa kiwango cha lami kupitia *TACTIC* Awamu ya Pili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Mwakulu – Kakese ipo katika mpango wa ujenzi wa mradi ule wa *TACTIC* na hivi karibuni watatangaza kazi ya kuweza kuwapata wale watakaofanya usanifu wa barabara hii na itaanza ujenzi wake kwa vipande. Kwa hiyo, wakipata wale watu wa kwenda kufanya usanifu tutamjulisha Mheshimiwa Kapufi ili naye aweze kushiriki katika zoezi la utiaji saini kama ambavyo tulifanya kwenye miradi mingine ambayo ipo chini ya TAMISEMI.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa. Je, ni lini Serikali itajenga daraja la kutoka Mlambalasi ambayo ni Kata ya Kiwere kwenda Kalenga ambako ndiko kwenye Makumbusho ya Chifu na wananchi wamekuwa wakipata shida sana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge kuweza kupitia bajeti ya *TARURA* ya mwaka 2023/2024 na kuona ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili la Mlambalasi kuelekea Kalenga; na kama bajeti imetengwa tutahakikisha mara moja fedha hiyo inakwenda ili ujenzi huu uweze kuanza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mhata kwa niaba Mheshimiwa Mwambe.

Na. 549

**CRDB kufungua tawi Mji wa Mangaka**

**MHE. CECIL D. MWAMBE K.n.y. MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, lini Benki ya CRDB itafungua tawi katika Mji wa Mangaka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya *CRDB* imeanza ujenzi wa tawi katika Mji wa Mangaka. Tawi hilo linatarajiwa kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa mji huo kabla ya mwezi Septemba 2023, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba ni mwezi ambao tunategemea kuanza kilimo katika maeneo yetu;

Je, Serikali haioni haja ya kuwataka Benki ya *CRDB* waanze kutoa mikopo kwa wakulima ili waweze kutayarisha mashamba yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kata za Msikisi, Kijiji cha Namalembo na Matutwe, Chiwalwe, Namajani pamoja na Mpanyani zipo mbali sana na makao makuu ya wilaya ambako ndiko zinatolewa huduma za kibenki kwenye Jimbo la Ndanda;

Je, Serikali haioni haja ya kuwasogezea wananchi huduma kwenye maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu Maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwambe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba benki itatoa huduma zote mara tu baada ya kukamilika kule Liwale ikiwemo mikopo *CSR* na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, tutashauriana na benki ili wapeleke huduma hizo za kibenki katika zile kata ambazo hazijafikiwa na benki ili kuepusha utapeli ambao unafanyika katika shughuli za wanadamu kiuchumi za kila siku.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendela, Mheshimiwa Ezra Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Ezra upo? Au bado unafikiria medali? *(Makofi)*

Na. 550

**Kauli ya Serikali juu ya fedha zinazotumwa nje ya nchi**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu ucheleweshaji fedha zinazotumwa Nje ya Nchi kutokana na Mabenki kuwa na uhaba wa fedha za Kigeni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imechukua hatua kadhaa katika kupunguza athari kwenye soko la ndani la fedha za kigeni ili kusaidia shughuli za

biashara na miamala kuendelea kufanyika. Hatua hizo ni pamoja na:-

a) Kuanzia Machi 2023 Benki Kuu imeongeza kiasi cha fedha za kigeni kinachouzwa katika soko la jumla la fedha za kigeni kutoka Dola za Marekani milioni moja hadi Dola za Marekani milioni mbili kila siku.

b) Kuongeza kiwango kinachoruhusiwa kuuzwa kwa muamala mmoja kwa njia ya rejareja kwenye soko la fedha za kigeni baina ya Mabenki kutoka Dola za Marekani 250,000 hadi Dola za Marekani 500,000.

c) Kuhakikisha ukwasi wa Shilingi ya Tanzania unabakia katika viwango vinavyoendana na mahitaji halisi ya kiuchumi kwa kutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki za biashara nchini zimeendelea kutunza amana ya kutosha katika akaunti kwenye benki nje ya nchi ili kufanikisha miamala ya ulipaji wa bidhaa na huduma mbalimbali zinazoagizwa na kuuzwa nje ya nchi. Aidha, nazielekeza benki zote nchini, kuhakikisha kuwa zina akiba ya kutosha ya fedha za kigeni kabla ya kupokea fedha kutoka kwa mteja anayetarajia kuzituma nje ya nchi ili kuepuka ucheleweshaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa mabenki mengi hapa nchini bado yana uhaba wa fedha tofauti na Mheshimiwa Waziri ulivyosema. Hali ambayo imepelekea sasa hivi wafanyabiashara wengi wa Soko la Kariakoo, hawa wadogo wadogo na wengine wakubwa wanapata shida ya kupata pesa za kigeni, kiasi kwamba *CRDB in a day* sasa hivi huwezi kupata zaidi ya dola 1,000 na mabenki mengine kama *NMB* na *NBC*

huwezi kutoa zaidi ya dola 500 kwa siku. Kitu ambacho kama mtu anahitaji kutuma pesa nyingi nje ina mchukua muda mrefu sana kuzunguka kwenye benki mbalimbali kukusanya hela na haruhusiwi ku-*change* hizo hela;

Je, sasa ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha tunawapeleka wafanyabiashara katika *dreams* zao za kupata fedha za kigeni ili waweze kufanya shughuli zao za biashara vizuri bila kukwama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kihalisia Nchi zetu zimekuwa zinafanya *trading* kubwa sana na Nchi za Asia ikiwemo China, India na Uturuki pia, lakini wafanyabiashara wa Tanzania wanalazimika kubadilisha pesa zao kuwa kwenye shilingi kupeleka katika dola na wanapofika kwenye yale Mataifa wana-*change* tena kutoka kwenye dola kupeleka kwenye pesa za wale mataifa;

Je, sasa wanakuwa wanapata hasara ya *exchange rate* hapo, hamuoni kwamba iko hajia ya Serikali ya Tanzania kuongea na mataifa haya makubwa ambayo tunafanya nayo biashara na tunatembelea kwa kiasi kikubwa na uanguko wa dola hasa zinaposhindwa kupatikana, wakaturuhusu tukaanza kufanya *exchange rate* ya pesa za nchi zao; kwa mfano anaenda China akaondoka na *Yuan* akiwa hapa hapa akifika kule asipate usumbufu wa kubadilisha kwenye dola halafu watoke kwenye dola warudi kwenye pesa ya Mataifa yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, tayari Serikali imechukua hatua kadhaa ili kupunguza au kuondoa changamoto hiyo. Kwa hiyo naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, hivi karibuni changamoto hiyo imeondoka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, shauri lako Mheshimiwa *Engineer* tumelichukua na tunalifanyia kazi. Ninachotaka kukuambia, hivi karibuni tumeanza mazungumzo na India katika shauri ambalo umelitoa na Nchi nyingine tutaenda.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendela, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Njau.

Na. 551

**Utaratibu wa kutambua *fire hydrats* nchini**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka utaratibu mzuri wa kutambua *fire hydrants* nchini na kuziwekea alama ili kusaidia wakati wa majanga ya moto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshirikiana na Mamlaka za Miji na Maji kukagua na kutambua *fire hydrants* 2,348 ambazo zipo Nchi nzima. Jeshi limeanza kutekeleza utaratibu maalum wa kimataifa wa utambuzi wa *fire hydrants* ambao ni kuziwekea alama ya *FH*. Jeshi pia linaziweka *fire hydrants* hizo katika mfumo wa utambuzi Kijiografia *(Geographical Information System – GIS)* na kuzijengea mifuniko migumu itakayozuia uharibifu wake. Aidha, Jeshi linawasiliana na mamlaka zinazohusika na ujenzi wa barabara na uendelezaji wa miji kudhibiti ujenzi holela wa makazi na upanuzi wa barabara za mitaa unaohusisha kuzifukia *fire hydrants*. Lengo ni kuzitunza *fire hydrants* zilizopo ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji wakati wa kutelekeza majukumu ya kuzima moto yanapotokea majanga, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini na maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *fire hydrants* zinazotakiwa nchini ni 285,000 na zilizopo ni 2,348 sawa na asilimia 8.2 tu;

Je, Serikali haioni haja ya kujenga miundombinu hiyo ili kuzuia majanga makubwa ya moto yanatokea ili kuzuia pia Serikali kupata hasara na wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa changamoto hii inatokea katika miji na majiji makubwa;

Je, Serikali haiona sasa kuna haja ya kuweka miundombinu hiyo katika miji na majiji makubwa, kwenye masoko na shule ili pia kuzuia majanga hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba *fire hydrants* zilizopo ni chache hazilingani na zile zinazohitajika, na ndiyo maana Jeshi letu la Zimamoto na Uokozi linawasiliana na mamlaka zote za ujenzi za miji pamoja na mamlaka za maji kila wanapotekeleza miradi hiyo wazingatie uwekeji wa hizi *fire hydrants.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili ninakubaliana naye, kwamba miji mikubwa ndiyo iko kwenye changamoto kubwa zaidi ya kukumbana na majanga ya moto na kwa msingi huo mkazo zaidi utawekezwa kwenye miji mikubwa kadiri tunavyoendelea kuimarisha huduma za *fire* na uokozi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha, washa *microphone* yako.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, aah**!** *Sorry,* ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Je, Serikali imewaandaje Askari wa Jeshi la Zimamoto katika uokoaji kwenye uvamizi wa nyuki katika makazi ya watu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kama ambavyo jukumu lake limebainishwa linashirikiana na mamlaka za misitu kila inapotokea janga kama hilo la nyuki kama ilivyotea siku tatu zilizopita hapa Dodoma, wameshirikiana vizuri sana wenzetu wa idara ya misitu kukabiliana na janga lile na kuwahamisha kabisa nyuki kutoka eneo lile. Nadhani ni jambo ambalo tunaomba wananchi inapotokea makundi ya nyuki kwenye maeneo yao wapige namba ya dharura inayoonyesha *always* 114 ili vyombo vyetu viweze kukabiliana nayo kabla haijaleta madhara kwa jamii zetu, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 552

**Kulipa fidia wananchi wanaoathirika na ujenzi Bwawa la Umeme Lumakalya – Makete**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, lini wananchi waliopitiwa na ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mto Lumakali Makete watalipwa fidia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Mto Lumakali unalenga kuzalisha umeme wa *MW 222* kwa kutumia maji ya Mto Lumakali mkoani Njombe na unahusisha pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa *kV* 220 yenye urefu wa kilometa 65 kutoka kwenye mitambo hadi Kituo cha Kupoza Umeme cha Iganjo mkoani Mbeya. Gharama za ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme ni takribani shilingi trilioni 1.42 na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ni takribani shilingi bilioni 50.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya awali ya mali za wananchi wanaopisha Mradi wa Ujenzi Bwawa la Umeme la Mto Lumakali imekamilika na Serikali imetenga fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya kuanza malipo ya fidia kwa wananchi hao. Kwa sasa kazi ya uhakiki inaendelea kwa mwezi Juni, 2023 na baada ya kazi hiyo kukamilika malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi yanatarajiwa kuanza kulipwa kuanzia mwezi Julai, 2023, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Jambo la kwanza kwa niaba ya wananchi wa Makete tuishukuru Serikali kwa mradi huu ambao ni mradi mkubwa ambao tayari *dermacation* imeshafinyaka na sisi wananchi wa Makete tupo tayari kupokea. Utayari wa Serikali kwamba Mwezi wa saba itaanza kulipa fidia kwa wananchi wetu kwa mwaka huu. Maswali yangu mawili ya nyongeza ni yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaozunguka eneo hili la bwawa wa Vijiji vya Busokelo, Madihani, Bulongwa, Mwakavuta, Itete pamoja na Ruangwa; vijiji hivi vyote sasa hivi shughuli za kiuchumi zimesimama kwa sababu ya *dermacation*. Sasa tulikua tunaomba kujua;

Je, mko tayari kuturuhusu wananchi waweze kulima yale mazao ambayo yanaweza kuondoka wa mfupi kwa maana ya mahindi, njegere na shughuli zingine ambazo hazichukui muda mrefu, kwa sababu muda huu shughuli zote zimesimama?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, bwawa hili linahusisha miradi ya ujenzi wa barabara, kwa maana ya kutoka Makete kuelekea Busokelo kwa Mheshimiwa Mwakibete;

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha miundombinu hii inajengwa kwa sababu huu ni mradi mkubwa ambao utapitisha vifaa vingi; Serikali itajenga barabara hizi lini wakati wa utekelezaji wa mradi huo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya Serikali na mimi nipokee shukurani na pongezi za Wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa ujumla na Mkoa wa Mbeya ambako bwawa linafika hadi Busokelo. Lakini nimuombe Mheshimiwa Sanga aendelee kuwashawishi wananchi watuvumilie kwa sababu tunatarijia kuanza kulipa fidia mwezi unaokuja au labda mwezi unaofuata baada ya hapo. Katika muda mfupi wananchi watapata kile ambacho wanakistahili ili eneo hili waliweze kuliacha kwa ajili ya sasa Serikali kuwa tayari kufanya shughuli zake ambazo ni za uendelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuahidi Mheshimiwa Sanga kwamba wananchi hawatachukua muda mrefu watakuwa wamepata fidia yao na wanaweza wakaendelea kujiendeleza kwenye maeneo yao na maeneo yao. Lakini pembeni ya hilo tutaendelea kujadiliana na tuzungumze. Tunayo *experience* mbaya, kwamba tunapotoa nafasi kama hiyo wananchi sasa wanarudi moja kwa moja hata baada ya kulipwa fidia wanataka waendelee kubaki kwenye maeneo yao. Kwa hiyo, tutajadiliana na viongozi wa Serikali wa maeneo husika na wewe Mheshimiwa Mbunge ili tuone namna bora ya kuwahudumia wananchi katika kipindi hiki ambacho ni cha mpito

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye eneo la pili, ni kweli tutagenga miundombinu mbalimbali katika maeneo hayo barabara, madaraja kwa ajili ya kubeba mzigo kuhudumia mradi. Na kwa sababu mradi bado haujaanza, *plan* yetu ni kuanza kulipa fidia tukamilishe mambo madogo madogo halafu tujenge miundombinu kwa ajili ya kuweze kufikia lile eneo. Kwa hiyo kabla

ya mradi kuanza mwaka wa fedha ule mwingine unaokuja barabara na maeneo mengine yanayotakiwa kuwekea miundombinu itawekwa ili ihudumie eneo la mradi lakini pia ihudumie wananchi kwa maendeleo yao ya kila siku.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane jiandae Mheshimiwa Catherine.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Je, ni lini Wananchi wa Kitongoji cha Cheketu, Kijiji cha Somanga Kusini, Wilayani Kilwa watalipwa fidia ya kupisha ujenzi wa miundombinu ya umeme katika eneo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la Mheshimiwa Ndulane linahusiana na ujenzi wa mradi wa kujenga kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia gesi *Megawatt* 350 pale Somanga Fungu, na tayari tumepata mfadhili, mwenzetu wa *JICA,* tunaendelea na kukamilisha mazungumzo. Tutakapokuwa tayari kumaliza mazungumzo na kujenga mradi wananchi wa eneo hilo watapewa fidia yao. Tuombe Mheshimiwa Mbunge aendelee kutusaidia eneo hilo liendelee kulindwa ili muda wa kulipa fidia utakapofika basi isiwe ni shida kulipa fidia ili kuweza kukamilisha mradi wetu wa *Megawatt* 350 kwa kutumia…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Katika Mkoa wa Arusha maeneo mengi hususan Wilaya ya Monduli umeme wa *REA* nguzo zimesimikwa nyanyazimeshawekwa lakini mpaka leo wananchi hawajapata umeme;

Je, ni lini sasa wananchi hawa watapata umeme ili waondokane na adha hii kubwa ya kukosa umeme? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna maeneo mengi ambapo nguzo zimesimikwa na miradi haijakamilika. Katika maeneo aliyoyataja ya Monduli na maeneo mengine Arusha tunaye mkandarasi anayeitwa ambaye tayari yuko kazini anaendelea na kazi. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge Catherine Magige pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kwamba kabla ya Desemba mwaka huu miradi yote ya *REA III Round II* itakuwa imekamilika na ndugu zetu wananchi wa Monduli na wengine watapata umeme kwa kadri tulivyokubaliana.

**NAIBU SPIKA:** ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Ameir kwa niaba Mheshimiwa Londo.

Na. 553

**Nafasi ya ubunifu katika mageuzi kiuchumi**

**MHE. DENNIS L. LONDO K.n.y. MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR** aliuliza:-

Je, ubunifu una nafasi gani katika kuleta mageuzi ya kiuchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, Mbunge Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ubunifu ni nyenzo na kichocheo cha kuongeza ufanisi katika sekta mbalimbali za uzalishaji na kutoa huduma nchini. Matumizi ya ubunifu yameongeza ufanisi katika uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma. Aidha, maeneo yaliyonufaika zaidi ni pamoja na: mawasiliano, huduma za fedha, utawala, masoko, afya, tafiti na usimamizi wa fedha za umma, mitambo inayojiendesha, kompyuta na roboti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubunifu wa teknolojia mpya ikiwemo mifumo ya TEHAMA katika undeshaji wa shughuli za Serikali *(e-Government)* na kukusanya mapato ya serikali kwa njia ya kielektroniki *(GePG)* kwa kiasi kikubwa zimechangia katika mageuzi ya kiuchumi tunayoshuhudia nchini. Mathalan ubunifu uliowezesha kutuma na kupokea fedha kupitia simu za mkononi, umeleta mageuzi makubwa ya kiuchumi nchini hasa kwa wafanyabiashara na wananchi mijini na vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kuna ongezeko kubwa la thamani ya bidhaa zinazotokana na ubunifu, kwa mfano, kutoka mwaka 2002 kulikuwa na shilingi bilioni 208, kufikia mwaka 2020 zaidi ya shilingi bilioni 700 kwa takwimu za Umoja wa Mataifa. Je, Serikali imejipangaje kulinda hakimiliki za wabunifu wa Kitanzania ili washiriki kikamilifu katika uchumi bunifu wa dunia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa uchumi bunifu na bidhaa bunifu ni utajiri wa kibiashara na kiutamaduni. Je, Serikali haioni wakati umefika sasa Wizara ya Elimu kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Wizara ya Fedha na taasisi nyingine za kibiashara kuona kwamba Tanzania inashiriki kikamilifu katika uchumi bunifu katika dunia yetu? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Londo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi kwanza kuchochea bunifu mbalimbali hapa nchini na kuanzia mwaka 2019, Serikali imekuwa ikiendesha Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu maarufu kama KISATU kwa ajili ya kualika watu mbalimbali walete bunifu zao, washindanishwe, zitambuliwe na ziendelezwe. Baada ya kuendelezwa ziweze kulindwa kwa kupata hakimiliki. Tangu tuanze mashindano hayo tayari bunifu

283 zimeshahakikiwa, 38 tayari ziko sokoni nazo hizo zinalindwa kwa ajili ya kuingia sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake Serikali inaona umuhimu sana wa kuchochea bunifu kwa ajili ya maendeleo ya uchumi, ndiyo maana vile vile tunasaidia vijana wetu ambao wanaenda na bunifu mbalimbali katika mashindano ya Kimataifa na baadhi yao wameshinda tuzo mbalimbali na sisi tunachochea waingie sokoni kwa ajili ya kubiasharisha bunifu zao.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, Serikali ina mpango gani wa kutambua na kuendeleza ubunifu unaofanywa na wanafunzi kwenye vyuo vyetu hapa Tanzania kikiwepo Chuo cha *DIT* ambapo kuna mwanafunzi mmoja anaitwa Angella Cliff Nkya ametengeneza mfumo wa ku-*control* makosa ya barabarani ili waweze kuendelezwa na Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua bunifu zote za wanafunzi na watu mbalimbali hata watu walioko vijijini na wanafunzi wamechangia vile vile katika baadhi ya bunifu ambazo sasa hivi zimeanza kuingia sokoni. Zipo bunifu ambazo tayari zimeshaanza kutambulika, zinafahamika na hatua iliyobaki kwa kweli sasa hivi ni kuhakikisha kwamba bunifu hizo zinaingia sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe mfano mmoja tu, bunifu ya kuweza kulipia bili ya maji kwa kutumia simu janja ambayo imegunduliwa na Mtanzania, sasa hivi inafanyiwa majaribio kwa ajili ya kununuliwa na Mamlaka ya Maji Tanzania na kutumika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Kasabago. Mheshimiwa Kasabago jina hilo hutaki kulitumia, haya Mheshimiwa Mushashu.

Na. 554

**Kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza nchini**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti Magonjwa yasiyoambukiza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali imetenga shilingi milioni 725 kwa ajili ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Tatu wa Kitaifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza (2021 – 2026) ambapo umeainisha mikakati mahususi ya udhibiti wa visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza ambayo ni kuimarisha uratibu na ushirikishwaji wa sekta mtambuka; Kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma; Kuwajengea uwezo watumishi katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza; Kuimarisha na kusimamia shughuli za utafiti; pamoja na kuhamasisha wananchi kuhusu njia za kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza. Njia hizi ni kufanya mazoezi, pamoja na kuzingatia kanuni bora za lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mushashu.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo

maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa duniani kwa sasa, watu zaidi ya 28 wanakufa kila sekunde kwa sababu ya magonjwa yasiyoambukiza na kwa sababu Tanzania kwa sasa kisababishi kikubwa cha vifo Tanzania ni magonjwa yasiyoambukiza. Kwa nini Serikali isitoe fedha za kutosha ili wananchi waweze kupata elimu, wajue visababishi, wajue na namna ya kujikinga kwa sababu haya magonjwa yanaweza kuzuilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumbaku ni zao la biashara ndani ya Tanzania, lakini tumbaku hiyo hiyo ni kisababishi kikubwa kinacholeta magonjwa yasiyoambukiza kama kansa, *stroke,* presha na kisukari. Je, ni lini Serikali itawawezesha wakulima wa tumbaku nchini ikawapa mazao mbadala, wakawatafutia na masoko ili kusudi waondokane na hiki kilimo ambacho kinaathiri afya zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuja na swali hili zuri ambalo ni eneo kwa kweli ambalo Mheshimiwa Waziri wa Afya ameliwekea msisitizo wa nguvu sana kwa sababu ndiyo tatizo kubwa kwa sasa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza; kwanza Serikali imeweka fedha nyingi kwa sababu ukiona kwenye miundombinu, lakini ukiona manunuzi ya *CT scan* na mambo mengine, lakini Wabunge wamemwona Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hapa karibuni alisaini mikataba na Wakuu wa Mikoa kwenye eneo hili la lishe. Pia wameona viongozi mbalimbali wakishiriki katika matamasha makubwa. Kwa hiyo fedha tulizotaja hapa ni fedha tu kwa ajili ya hamasa, lakini hatujazungumzia kwa ujumla dawa na sehemu zingine mtambuka ambazo fedha zimewekezwa kwa ajili ya eneo hilo. Kwa hiyo kuna fedha za kutosha na tutaendelea kuona ni namna gani tutasisitiza eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu tumbaku; kupanga ni kuchagua, ni ukweli kabisa kama ambavyo Mbunge anasema tumbaku ina madhara mengi, siyo tumbaku tu

pekeyake pamoja na kelele zinazopigwa mitaani pamoja na mambo mengine mengi ambayo tunayatumia. Sasa Mheshimiwa Mbunge pamoja na ukweli huu wa kwamba tunahitaji kutafuta zao mbadala wa tumbaku, naomba nisiseme lolote hapa kwa sababu linahusu Wizara zote na taratibu zetu na maslahi ya wananchi, tutashirikiana na Wizara husika na tuone ni namna gani tunaweza kufanya, lakini kweli kuna tatizo hili na siyo tumbaku peke yake kuna mambo mengi yanayosababisha tatizo hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali; je, mpango ukoje kwa Bima ya Afya kwa Wote kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa hawa wa magonjwa yasiyoambukiza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa bima ya afya ulikuja hapa kwa ajili ya sisi kuja na Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote ili kuweza kabisa kuboresha mambo mengi ambayo yangeweza kusaidia pamoja na eneo hili tunaloliona. Kwa hiyo kikubwa mimi na wewe tuendelee kushirikiana kuona ni namna gani tunapambana kupeleka Muswada wetu wa Bima ya Afya kwa Wote uweze kurudi na iwe ajenda ya Mbunge ya kudumu na ajenda ya kudumu ya Wabunge ili wananchi waweze kupata huduma tukija na mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na tabia wagonjwa wa magonjwa ya kuambukiza wakienda kwenye *dispensary* na vituo vya afya hawapewi dawa za magonjwa ya kuambukiza kama presha. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha inatoa dawa kwa wagonjwa wetu hata huku kwenye ngazi ya *dispensary* na vituo vya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge tulikuwa na tatizo hili, lakini kama Wabunge wanakumbuka juzi nilijibu swali kwamba kwenye eneo la *dispensary* zimeongezeka dawa zinazotolewa kutoka 243 mpaka 459, maana yake madawa hayo ya presha, sukari yameongezwa kwenye *level* ya *dispensary,* kwa hiyo tatizo hilo halitakuwepo tena. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga.

Na. 555

**Mgogoro wa mpaka kati ya wananchi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatatua mgogoro wa mpaka kati ya wananchi wa Kata ya Tambukareli na Jeshi la Wananchi wa Tanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo linalozungumziwa lipo katika Kambi ya Jeshi Usule katika Manispaa ya Tabora. Eneo hilo la Jeshi lilipimwa na ramani yake kusajiliwa Mwezi Septemba, 2004 na kupewa nambari 41,574. Mwezi Februari, 2023 Wizara imepeleka fedha kiasi cha shilingi 194,029,643 kwa Manispaa ya Tabora kwa ajili ya kugharamia fidia kwa wananchi wa maeneo ya Usule na Itaga waliopo katika eneo la Jeshi na tayari wahusika wameshalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua zipo changamoto za mipaka katika eneo la *buffer zone* katika Kata ya Tambukareli. Naelekeza Idara ya Miliki na Ushauri Majenzi katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kufika eneo hili na kuainisha changamoto hizi na kuzipatia ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kusisitiza wananchi kutovamia maeneo ya Jeshi, kwani ni hatari kwao na mali zao, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nishukuru Serikali kupitia Jeshi la Wananchi Tanzania kwa malipo ambayo wameshayafanya katika Kata ya Mbugani huko Usule ambako wananchi wote waliokuwa wanahusika wameshapewa malipo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu lilikuwa, huko kwenye *buffer zone* ambako ni Tambukareli; je, jeshi wana mpango gani wa kuhakikisha wanaonesha kabisa kwamba haya ni maeneo yao na haya ni maeneo ya wananchi ili kuondoa huu mgogoro uliopo? Wao hawana tatizo na eneo la jeshi, tatizo lao ni kujua mipaka ya jeshi iko wapi na wao wanaishia wapi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Swali jipya hilo eeh? Haya Tambukareli.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kwa Jeshi la Wananchi Tanzania na ninaomba kujibu swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge hili nimuahidi Mheshimiwa Mbunge nitaambatana naye ili tufike eneo hili pamoja na Idara ya Miliki na Majenzi kutoka Wizarani ili tuweze kuangalia changamoto hii, lakini niwahakikishie wananchi wa maeneo haya tutaweka mipaka bayana ili wananchi wajue wanaishia wapi na jeshi linaishia wapi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mwakiposa Kihenzile.

Na. 556

**Mradi wa kuhifadhi mazingira Mufindi**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta mradi wa kuhifadhi Mazingira katika chanzo cha maji cha Mto Ruaha na shamba la miti la *Sao Hill*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira na kulinda vyanzo vya maji kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwemo chanzo cha Mto *Little Ruaha* kilichopo kwenye Shamba la Miti la *Sao Hill.* Mto huo ni chanzo cha maji kwa wananchi wa Mji wa Iringa na viunga vyake na unatumika kwa shughuli za uzalishaji umeme, ufugaji na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada mbalimbali za kutunza vyanzo hivyo zinaendelea ikiwemo kuanzisha Jumuiya nne za Watumia Maji Wilaya za Mufindi, Kilolo na Iringa; kutoa elimu ya uhifadhi wa vyanzo; na kutekeleza *program* ya kupanda miti rafiki na maji ambapo miti 3,000 imepandwa katika halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara inaandaa Mpango wa Uhifadhi wa Vidakio wa mwaka 2021 hadi 2035. Kwa kupitia mpango huo, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imepanga kuweka alama ya mipaka ya kudumu katika chanzo cha Mto *Little Ruaha* ndani ya Shamba la Miti la *Sao Hill*; kuweka mabango yenye jumbe za katazo za shughuli za binadamu katika chanzo cha uhifadhi wa chanzo; kupanda miti rafiki na maji;

kutoa elimu kuhusu umuhimu wa uhifadhi endelevu wa vyanzo vya maji na mazingira; na kuajiri walinzi wa kulinda vyanzo vya maji kwenye shamba hilo hususani kwenye maeneo yenye uharibifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Moja; kwa kuwa wananchi wa Mufindi Kusini wameamua kuwa na shughuli mbalimbali mbadala ili wasikate miti na kuharibu vyanzo vya maji. Je, Serikali iko tayari sasa kuwaunga mkono na itaanza lini kuchimba mabwawa ili waweze kufanya shughuli zingine mbadala kama za uvuvi katika eneo la Mufindi Kusini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuzingatia unyeti na uzito na umuhimu mkubwa wa Mto Ruaha kwenye Taifa letu. Je, Serikali iko tayari kufanya elimu kwenye Mamlaka za Serikali Mitaa ili itoe fursa kwa wananchi kujua pengine umuhimu wa kuhifadhi mto huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Kihenzile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uchimbaji wa mabwawa katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Kwanza nimpongeze kwa sababu alishiriki katika hili kuona kwamba tafiti inakamilika na kupita Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Rufiji, tafiti ile Mheshimiwa Mbunge imeshakamilika na tunatarajia mwaka ujao wa fedha tuweze kuchimba mabwawa maeneo yale ambayo tunaona yatakuwa ni msaada kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa suala la fedha kwa ajili ya kuendeleza semina mbalimbali kutoa elimu kwa jamii; kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, tayari sisi kama Wizara tumeanza kutoa elimu kwa hasa viongozi wa vyombo vya

watumia maji, lakini sasa hivi tutakwenda zaidi kwa viongozi na makundi mbalimbali na jukumu hili litatekelezwa na Bonde la Rufiji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Dkt. Kimei.

Na. 557

**Mito ya Ghona, Rau na Deu**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mabwawa katika Mito Ghona, Rau na Deu ili kupunguza athari za mafuriko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mito ya Ghona, Rau na Deu inapitisha maji kiasi cha lita 103,310 kwa sekunde (sawa na mita za ujazo 267,940.21 kwa siku) ambapo Mto Rau ni lita 98,000 kwa sekunde, Mto Dehu Lita 3,100 sekunde na Mto Ghona ni lita 2,210 kwa sekunde. Mito hiyo hupeleka maji yake katika Mto Ruvu na hatimaye kufika katika Bwawa la Nyumba ya Mungu. Serikali kupitia Bodi ya Maji Bonde la Pangani imeshafanya upembuzi wa awali na kubaini kuwa sehemu ya maji ya mito hiyo haifiki kwa wakati kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu na badala yake husambaa na kuacha mkondo wake na kuathiri wananchi kandokando ya mito hiyo ikiwemo Vijiji vya Chekereni na Kileo kupitia Mto Ghona; maeneo ya Majengo, Msaranga, Mabogini, Oria, Ngasini, Mandakamnono yanayoathiriwa na Mto Rau; na Vijiji vya Mongalia, Soko, Ngaseni na Kiterini huathiriwa pia kupitia Mto Deu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ya maji ya mito hiyo kusambaa ni kutokana na kuharibika kwa kingo za mito husika katika maeneo ya tambarare kunakosabisha maji kutoka katika mikondo yake na kusambaa katika maeneo wanayoishi wananchi. Serikali imeanza kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na ufukuaji wa mikondo ya mito katika baadhi ya maeneo korofi ya mito hiyo na kazi ya ufukuaji itaendelea katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 mpaka itakapokamilika. Aidha Bonde la Pangani litafanya tathimini kwenye maeneo yanapitiwa na mito hiyo ili kubaini kama kuna uwezekano wa kujenga mabwawa bila kuathiri upatikanaji wa maji katika Bwawa la Nyumba ya Mungu ambalo linatumika katika shughuli nyingi za kijamii na kiuchumi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri na yenye tija, naomba niulize maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo la Vunjo kuna mabwawa mawili moja linaitwa Urenga katika Kata Kirua Vunjo Mashariki na nyingine ni Koresa Kata ya Kirua Vunjo Kusini yameharibika sana sasa hivi ni kama vile hayapo. Nataka nijue kama Waziri atakubali kutembelea eneo hili na kuyaona haya mabwawa ili aone kama watafanya nini kuyakarabati? *(Makofi)*

Swali la pili. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu ukamilishaji wa miradi iliyoanza mwaka juzi kule Mamba Kaskazini na Kusini, Mwika Kaskazini na Kusini na Marangu Mashariki na Magharibi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Charles Kimei kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kutembelea mabwawa ambayo kwa sasa hayafanyi vizuri. Mheshimiwa Mbunge, naomba nikuhaidi baada ya Bunge hili tutakwenda kuyatembelea na kuona nini kinaweza kufanyika kupitia watalaam wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kukamilisha miradi Mheshimiwa Mbunge pia hili tutakapokuwa tunatembelea tutaona kwa nini miradi hii haijamilika kwa wakati? Nakuhakikishia tutahakikisha inakamilika ili wananchi waweze kupata huduma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, maswali yamekwisha na muda umekwisha, tunaendelea na matangazo ya wageni waliopo Bungeni leo hii.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Jukwaa la Spika, Spika Mstaafu wa Bunge la Tanzania na Kamishna wa Sensa ya Watu na Makazi Tanzania, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, ahsanteni, karibu sana Mheshimiwa Makinda, karibu sana kwenye Bunge, Bunge hili litakukumbuka kwa mambo mengi ambayo umeyafanya, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango; Dkt. Natu Eli-Maamry - Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango; Ndugu Jenifa Omolo - Naibu Katibu Mkuu, Huduma za Hazina; Ndugu Lawrence Mafuru - Naibu Katibu Mkuu, Usimamizi wa Uchumi; Ndugu Amina Shaban - Naibu Katibu Mkuu, Usimamizi wa Fedha za Umma; na Ndugu Emmanuel Tutuba - Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Alphayo Kidata - Kamishna Mkuu Mamlaka ya Mapato Tanzania; Ndugu Albina Chuwa - Mtakwimu Mkuu wa Serikali; Ndugu Mwanyika Semroki - Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali; Ndugu Ernest Mchanga - Katibu wa Tume ya Pamoja ya Fedha; *CPA*. Seif Omary Haji - Kamishna Msaidizi wa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; Ndugu Eliakim Maswi - Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma *(PPRA);* na Dkt. Baghayo Sagware - Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)*. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Frank Nyabundege, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADBA);* Ndugu Lilian Mbassy - Mtendaji Mkuu wa Benki ya Maendeleo *(TIB); CPA*. Nicodemus Mkama - Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na

Dhamana; Ndugu James Mbalwe - Mkurugenzi Mtendaji, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania; Profesa William Pallangyo, Mkuu wa Chuo – Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA);* Profesa Geraldine Rasheli, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini *(GPSA);* na Ndugu Godfrey Malekano, Mtendaji Mkuu wa Soko la Bidhaa Tanzania *(TMX)*. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Sabasaba Moshingi, Afisa Mtendaji Mkuu – Benki ya Biashara Tanzania *(TCB);* Ndugu James Sando, Katibu Mtendaji – Mamlaka ya Rufaa za Zabuni *(PPAA); CPA*. Pius Maneno, Mkurugenzi Mtendaji – Bodi ya Taifa Uhasibu na Ukaguzi *(NBAA);* Ndugu Bahati Moshi Ndeserua, Katibu – Bodi ya Rufaa ya Kodi *(TRAB);* na Ndugu Mohamed Magate, Msajili – Baraza la Rufani za Kodi *(TRAT)*. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mudith Buzenza Cheyo, Afisa Mtendaji Mkuu Mfuko wa *Self (SELF MF);* Ndugu Godfred Mbanyi, Mkurugenzi Mtendaji – Bodi ya Wakurugenzi Wataalamu wa Ununuzi wa Ugavi *(PSPTB);* Ndugu Simon Milenge Miganga, Afisa Mtendaji Mkuu – Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja *(UTT – AMIS);* Ndugu Leonard Mwangike, Mwenyekiti wa *(TPRA);* Profesa Hozen Mayaya, Mkuu wa Chuo cha Mipango; Dkt. Tumaini Katunzi, Mkuu wa Chuo cha Takwimu; Profesa Josephat Mlotto, Mkuu wa Chuo cha *IFM*; na Ndugu Josephine Kurwa, Meneja Mahusiano Mwandamizi Benki ya *NMB*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 70 wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati, Chawa' wa Mama kutoka Mkoa wa Kagera, karibuni. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Benaya Kapinga kutoka Mpapa Mbinga Mkoa wa Ruvuma, karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mgunduzi wa *Traffic Lights Violation Monitoring System for Motorcycle* Ndugu Angela Cliff Nkya na Ndugu Georgeas Cliff Joshua, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mtaalam wa Maabara kutoka Kondoa Mkoa wa Dodoma, karibu. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Abubakari Asenga, Jukwaa la Walimu Wazalendo kutoka Kilombero Mkoa wa Morogoro, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Madiwani na Watumishi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kankoo Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Fatma Toufiq kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kamonga kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Aida Khenani kutoka Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo kutoka Musoma, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunae mgeni wa Mheshimiwa Mashimba Ndaki kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe kutoka Wilaya ya Kyela, Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 136 na walimu 21 kutoka *Mount Kibo School* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 38 na walimu 14 wa *Homage Primary School* kutoka Sumbawanga Mkoani Rukwa, karibuni. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi watatu wa Chuo cha Maji cha Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa niwaombe wageni tunaowatambulisha hapa ni kwa mujibu wa utaratibu, watambulishwe kwa majina yao. Siyo mnaleta mizigo ya watu huko mjini, mnawaleta humu ndani halafu hamuwataji majina, mnanielewa ninavyosema hivyo eeh? Maana wenye mizigo watakuwa wanaiona kwenye *tv,* lakini jina lake halitajwi humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa *Chief Whip* majibu ya Serikali yameanza kurudi kuwa marefu ni marefu sana, swali mistari mitatu jibu ni *page* nzima, jaribuni kufupisha *short and clear,* tunaelewa mazuri ya Serikali na tunaelewa kazi nzuri mnazozifanya na *details* nyingi sana zinachukua muda wa Kiti. Hapa Kiti tunakwenda kwa *time* na Bunge dini yake ni muda.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja za Serikali sasa namuita Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2023/2024 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu tisa ya Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu Na. 45 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wake, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema

na kutupatia wasaa wa kukutana kwa mara nyingine kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima napenda kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini na kunipa fursa ya kuendelea kusimamia majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango, kwa mara nyingine napenda kumhakikishia kuwa nitaendelea kutumikia kwa weledi dhamana aliyonipa na kusimamia masuala ya uchumi pamoja na bajeti ya nchi ikiwemo fedha na mipango ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba katika kipindi cha uongozi wake nchi yetu imepata mafanikio makubwa kiuchumi, kijamii na kisiasa ambayo kila mmoja wetu anapaswa kujivunia na kumuunga mkono. Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima, busara katika kubadilisha fikra na mifumo ya usimamizi wa maslahi ya wananchi wakiwemo wafanyakazi, wawekezaji, wafanyabiashara, wakulima, wafugaji pamoja na sekta zingine pamoja na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii adhimu pia kumpongeza Mheshimiwa Angellah Jasmine Mberwa Kairuki kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aidha, niwapongeze kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti na Kamati wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Mbunge wa Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu. Ninawaahidi ushirikiano thabiti katika utekelezaji wa majukumu yao ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Mheshimiwa Spika katika kuongoza Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa minajili ya tukio la leo, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi kwa maoni na ushauri wenye tija katika kuboresha usimamizi wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango na maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/2024. Kwa niaba ya Wizara na Taasisi zake, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa tutaendelea kufanya kazi pamoja na viongozi wa Kamati pamoja na Kamati nzima ili kuweza kutoa huduma stahiki wanazotakiwa kupata wananchi katika masuala ya kisera katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba kujielekeza moja kwa moja kwenye hoja iliyo mbele yetu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makuu manne (4) ambayo ni Muhtasari hususani majukumu ya Wizara; mwenendo wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023; vipaumbele vya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2023 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Wizara. Kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 534 la Julai 02, 2021 Wizara ya Fedha na Mipango imekasimiwa majukumu yafuatayo: -

(i) Kusimamia sera za kiuchumi jumla, fedha, ununuzi wa umma na ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

(ii) Kusimamia mipango, mikakati na miongozo ya kitaifa ya maendeleo.

(iii) Kusimamia bajeti ya Serikali.

(iv) Kuratibu upatikanaji wa fedha kutoka taasisi za fedha za kikanda na kimataifa na kusimamia kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

(v) Udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

(vi) Kusimamia matumizi ya fedha na mali za umma.

(vii) Kusimamia mifumo ya uendeshaji wa mashirika na taasisi za umma pamoja na vitengo vya uchumi na Serikali.

(viii) Kusimamia masuala ya fedha pamoja na kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.

(ix) Kusimamia mafao, pensheni na mirathi kwa wastaafu wasio wanachama wa mifuko ya uhifadhi ya jamii.

(x) Kusimamia deni la Serikali.

(xi) Kusimamia mifumo ya udhibi ya michezo ya kubahatisha.

(xii) Kusimamia maendeleo ya sekta ya fedha na;

(xiii) Kusimamia Takwimu rasmi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nawasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/2023 niliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi trilioni 14.94 kwa mafungu tisa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya Wizara na Taasisi zake. Vipaumbele vya matumizi ya kawaida ilikuwa ni: -

(i) Kukusanya, kutafuta na kudhibiti mapato na matumizi.

(ii) Kuhudumia deni la Serikali.

(iii) Kufanya tathmini ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 kwa ajili ya maandalizi ya dira mpya.

(iv) Kufanya tathmini ya mifumo ya maendeleo ili kuwezesha kutungwa kwa Sera za Taifa ya ufuatiliaji na tathmini.

(v) Kufanya tafiti katika sekta za uzalishaji.

(vi) Kuendelea na utekelezaji wa maagizo ya Serikali tafsiri ya Sheria, Wizara na Taasisi zake kwa lugha ya Kiswahili.

(vii) Kuhuisha mwongozo wa Taifa wa usimamizi wa viashiria hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Wizara iliendelea kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu kwenye Bunge. Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu, tusikilize hotuba ya Waziri wa Fedha, Bajeti ya Wizara yake. Wanamajukumu makubwa tusikilize ili tujue wanachokifanya. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika;

(i) Kundaa na kujenga ghala la Takwimu.

(ii) Kuratibu na kusimamia zoezi la Sensa ya Watu na Makazi.

(iii) Kuziwezesha taasisi za Wizara ususani taasisi za elimu, mafunzo kuboresha miundombinu.

(iv) Kujenga na kukarabati Ofisi za Wizara katika Mikoa ya Geita, Njombe, Songwe, Dar es salaam, Morogoro, Kigoma, pamoja na Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yangu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Wizara ya Fedha na Mipango, ilikadiriwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 38.0. Kati ya kiasi hicho, Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 988.3, Hazina shilingi trilioni 37.0, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu Serikali shilingi bilioni 60.1, Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango shilingi bilioni 1.0. Aidha, kati ya kiasi hicho kilichokadiriwa kukusanywa Fungu 21, trilioni 23.6 ni mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi na

yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, shilingi trilioni 4.6 ni misaada na mikopo yenye masharti nafuu, shilingi trilioni 8.8 ni mikopo yenye masharti ya kibiashara ikiwemo hatifungani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili 2023, Wizara imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali pamoja na mali za umma, hatua hizo ni pamoja na:

(i) Kuimarisha doria kwenye mipaka yote nchini ili kudhibiti ukwepaji kodi na biashara za magendo;

(ii) Kuendelea na kuboresha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ili kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato;

(iii) Kuendelea na kampeni mbalimbali za kutoa elimu kwa ajili ya mlipa kodi kupitia semina na makongomano na vyombo vya habari ili kuwezesha uelewa na uhiari wa kulipa kodi na kuendelea kuimarisha mifumo ya ufuataliaji wa vyanzo vya mapato yasiyo ya kikodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na Wizara ni kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kuunganisha Mfumo wa *MUSE* na kuanza kutumika katika Ofisi za Balozi 11 ambazo ni Ubalozi wa Tanzania, Lagos kule Nigeria; *New York* kule Marekani; Ottawa kule Canada; Riyadhi kule Saudi Arabia; Muscat kule Oman; Seoul, Korea ya Kusini; Kuwait kule Kuwait; Kuala Lumpur kule Malaysia; Washington, kule Marekani; Brasilia kule Brazil; na kuboresha Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani ikiwa ni pamoja na kuandaa Mpango Mahususi wa Ukaguzi; kuhakiki madeni ya chakula kwa shule za msingi na sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 45; kuhakiki mikopo inayotolewa na Serikali kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; kuhakiki madeni ya ununuzi wa pamba msimu wa mwaka 2019/2020 pamoja na madeni ya watoa huduma wa pembejeo; kuhakiki fedha za ujenzi wa masoko ya kisasa katika Manispaa ya Morogoro na deni la Mshauri Mwelekezi wa Shirika la Reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine pia ni kufanya ukaguzi wa Mifumo wa Mapato wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro; uhakiki wa madeni ya Soko la Kariakoo; kuhakiki madeni ya wazabuni wa vifaa kwenye miradi ya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru, Jengo la utawala na Kituo cha Afya Mlowa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, uhakiki wa malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma na wastaafu na kuhuisha kumbukumbu za mali za taasisi 537 zenye thamani ya Shilingi 68.891.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhudumia deni la Serikali. Kupitia Fungu namba 001, Bunge lako tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi trilioni 9.1 kwa ajili ya kuhudumia deni la Serikali pindi linapoiva. Hadi Aprili, 2023, Wizara imelipa kwa wakati notisi za madeni yaliyoiva jumla ya shilingi trilioni 7.4, sawa na ufanisi wa 82% ya lengo. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 4.4, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.7 na mtaji shilingi trilioni 2.7. Aidha, deni la nje ni shilingi trilioni tatu, ikijumuisha riba shilingi trilioni 0.8 na mtaji shilingi trilioni 2.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na maandalizi ya Dira 2050, Wizara imekamilisha taratibu za ununuzi wa mtaalamu elekezi kwa ajili ya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambapo mtaalam elekezi amewasilisha taarifa ya awali Aprili, 2023 na anatarajiwa kukamilisha tathmini husika ifikapo Agosti, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na zoezi la tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Wizara inaendelea na taratibu ambapo mchakato rasmi ulizinduliwa Aprili 2023. Aidha, warsha elekezi kwa Wajumbe wa Timu za Uandishi na Uhariri wa Dira ulifanyika Mei, 2023 Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, napenda kumpongeza kwa dhati ya moyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwongozo wake thabiti ambao umetuwezesha kuanza kwa wakati maandalizi ya Dira ya Taifa 2050. Nitoe rai kwa Watanzania wote kuendelea

kutoa maoni pale wanapoulizwa na timu ambayo inaandaa dira hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu liliridhia mapendekezo ya Wizara ya kufanya tathmini ya mfumo na muundo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi pamoja na programu za maendeleo na kubaini kuna uhitaji wa kuandaa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi pamoja na Programu za Maendeleo. Hadi Aprili, 2023, Wizara imefanikiwa kukusanya maoni na mapendekezo kutoka Wizara za kisekta, taasisi na mashirika ya umma, Bunge, vyuo vikuu na vyuo vya kati, taasisi za utafiti na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayoendelea kwa sasa ni kufanya uchambuzi na kuandaa mapendekezo kulingana na maoni ya wadau pamoja na miongozo ya maandalizi ya nyaraka za Serikali. Bunge lako limesema mara kadhaa kwamba sasa ni wakati muafaka kuletwa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na tathmini *(Monitoring and Evaluation)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Wizara ya Fedha na Mipango ilipata ridhaa ya Bunge ya kufanya tafiti mbalimbali kuibua fursa za uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya Serikali. Napenda kutoa taarifa kuwa hadi Aprili, 2023, Wizara imekamilisha tafiti mbili ambazo ni upatikanaji wa huduma ndogo za fedha na mchango wake katika ukuaji wa shughuli za kiuchumi na matokeo yake katika kupunguza kiwango cha umaskini kwa makundi maalum pamoja na utafiti kuhusu ufanisi katika ukusanyaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tafiti zilizokamilika, Wizara ipo katika hatua mbalimbali kukamilisha tafiti zifuatazo: Utafiti kuhusu mnyororo wa huduma za utalii nchini, upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya maendeleo, mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ardhi, na utafiti kuhusu uchumi wa kidijitali na matokeo yake katika matumizi ya fedha taslimu katika ununuzi wa bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara imefanyia kazi mapendekezo ya wadau kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi ambayo hayakuridhiwa na Serikali katika mwaka 2022/2023. Tathmini ya ufanisi wa misamaha ya kodi katika uchumi, mfumo wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Matokeo ya tafiti na tathmini zilizofanyika na tuyatumie katika kuboresha mazingira ya uwekezaji, biashara na mifumo ya usimamizi pamoja na mipango na matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023 Wizara ilipanga kuhuisha miongozo ya usimamizi wa vihatarishi na udhibiti wa ndani ili kuimarisha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi katika sekta ya umma. Hadi Aprili, 2023 Wizara imefanikiwa kuhuisha Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi wa Mwaka 2012, Mwongozo wa Mwongozo wa Usimamizi wa Viashiria na Udanganyifu wa Mwaka 2015 na Mwongozo wa Usimamizi wa Udhibiti wa Ndani ili kuendana na miongozo ya kimataifa. Kazi nyingine inayofanyika ni kuhuisha mwongozo wa ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2023, Mfumo wa Malipo Serikalini *(MUSE)* umeboreshwa na kufungamanishwa na Mfumo wa Taarifa za Watumishi wa Umma *(HCMIS)* ili kusomana na kubadilishana taarifa na kuboresha Mfumo wa *D-Fund* kwa kuunganisha na Mfumo wa Benki Kuu ya Tanzania ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za fedha za miradi zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi na Washirika wa Maendeleo na kuboresha Mfumo wa *GARI–ITS* sambamba na kuhuisha taarifa za taasisi za umma 463.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Wizara ilipanga kuandaa na kujenga ghala la takwimu ili upatikanaji wa taarifa za utekelezaji wa mipango na bajeti ya Serikali. Hadi Aprili, 2023, Wizara imekamilisha hatua ya awali ya kuainisha mahitaji na vyanzo vya taarifa na takwimu zitakazohifadhiwa kwenye ghala. Mahitaji hayo yamewezesha kuanza kazi ya usanifu na ujenzi wa ghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, kulikuwa na agenda ya kitaifa ya Sensa ya Watu na Makazi. Napenda

kutoa taarifa kwenye Bunge lako Tukufu na wananchi kwa jumla kuwa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi lilifanyika kwa mafanikio makubwa sana. Baada ya uzinduzi wa matokeo ya mwanzo ya sensa, ripoti nyingine kumi ya Sensa ya Watu na Makazi zitahitajika katika mgawanyo wa idadi ya watu katika maeneo ya kiutawala, mgawanyo wa idadi ya watu kwa umri na jinsi na mgawanyo wa idadi ya watu katika majimbo ya uchaguzi ambazo zilizinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Zanzibar Aprili 15, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, takwimu za Sensa Watu na Makazi kwa Mwaka 2022 zimetumika katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika mwaka 2023. Hatua inayoendelea ni ya kusambaza ripoti kwa wadau, kutoa elimu kwa umma mahususi ya matumizi ya takwimu za Sensa ya Watu na Makazi, kufuatilia utekelezaji wake na kuendelea kuchakata, kuchambua na kuandaa ripoti nyingine za kisekta kulingana na ratiba ya kutoa machapisho ya Sensa. Kwa niaba ya Serikali, natoa wito kwa wadau wote kufuatilia na kutumia takwimu za Sensa ya Watu na Makazi katika kusimamia mipango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mapinduzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya elimu, ngazi ya elimu ya msingi na sekondari na kusababisha ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo vya elimu ya juu, Wizara ilipata ridhaa ya Bunge lako Tukufu kutumia Shilingi bilioni 19 kupitia bajeti yake ya maendeleo ili kuboresha miundombinu ya kufundishia, kujifunzia taasisi tano za elimu ya juu zilizo chini ya Wizara. Hadi Aprili, 2023, taasisi hizo zimepokea jumla ya Shilingi bilioni 11.83, sawa na 62.27% ya makadirio ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa miundombinu ya Wizara katika mikoa wa Geita, Njombe, Songwe, Dar es Salaam, Morogoro, Kigoma na Ruvuma, katika mwaka 2022/2023, Wizara ilipanga kujenga ofisi katika mikoa ya Geita, Njombe na Songwe na kukarabati majengo ya ofisi katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Kigoma na Ruvuma. Hadi Aprili, 2023, mkataba kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi wa ofisi Geita umethibitishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ujenzi wa ofisi katika mikoa ya Njombe na Songwe umefikia hatua ya Mshauri Mwelekezi na kupewa zabuni kwa ajili ya usanifu wa michoro na kusimamia ujenzi. Vilevile, ukarabati wa ofisi katika mkoa wa Morogoro umekamilika na Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Kigoma umefikia zaidi ya asilimia 90 na asilimia 43 mtawalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2023, Wizara imefanikiwa kufuatilia na kuhakiki fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo Bararaba ya Masasi hadi Mtwara kilomita 160, ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani, Bagamoyo sehemu ya Mkange - Mandamazingira, Reli ya kisasa kutoka Isaka hadi Mwanza, Mabasi yaendayo Haraka Awamu ya Pili Ubungo Kisiwani, Njia za kusafirisha umeme kutoka Chalinze, Morogoro hadi Dodoma, Iringa hadi Sumbawanga, Wilaya ya Monduli hadi Makuyuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imefanikiwa kufanya ufuatiliaji wa tathmini ya miradi ya maendeleo 222 katika mikoa 17 ya Kagera, Kigoma, Geita, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Katavi, Rukwa, Mara, Simiyu, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na Pwani. Kati ya miradi hiyo, miradi nane ya kielelezo ambayo ni Bwawa la kuzalisha Umeme la Mwalimu Julius Nyerere Megawati 2,115; reli ya kisasa ya *standard gauge,* kiwanda cha kusindika sukari, Mkulazi; kufufua Shirika la Ndege la Taifa; mpango wa ununuzi wa meli za uvuvi katika bahari kuu; ujenzi wa bandari ya uvuvi; Bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima, Uganda hadi bandari ya Tanga, Chongoleani; na daraja la Kigongo - Busisi. Vilevile, Wizara imefanya ufuatiliaji wa tathmini ya miradi 16 inayosimamiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa katika mikoa tisa ambayo ni Kilimanjaro, Mwanza, Pwani, Tanga, Ruvuma, Njombe, Dar es Salaam, Arusha na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa usimamizi wa deni la Taifa, Wizara inaendelea kusimamia deni la Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134. Ili kuwa na taarifa sahihi kuhusu udhibiti wa deni la Serikali, wizara imefanya tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali kwa miaka 20 ijayo, kuanzia 2022/2023 hadi 2041/2042. Matokeo ya tathmini

yanaonesha kuwa, deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Aidha, taarifa inaonesha kuwa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa pato la Taifa ni asilimia 31.8 ikilinganishwa na ukomo ambao ni asilimia 55. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, wananchi na wadau wote wa maendeleo kuwa taarifa kamili inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *www.mof.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2023, Wizara imetoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu ili kuwezesha Mamlaka za Serikali kuandaa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa utaratibu wa *PPP*. Ushauri na mafunzo umekuwa na matokeo chanya ambapo Wakala wa Barabara Tanzania umeweza kukamilisha maandalizi ya mradi wa barabara ya haraka *(expressway)* kutoka Kibaha hadi Morogoro, kilomita 205, na hatua za ununuzi wa mbia zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, majadiliano na mbia aliyepatikana kwa ajili ya uendeshaji wa mradi wa mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam yanaendelea. Vilevile, Chuo cha Elimu ya Biashara kinakamilisha taarifa ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa kujenga mabweni ya wanafunzi na Jeshi la Polisi linakamilisha upembuzi yakinifu kwa mradi wa ukaguzi wa lazima wa vyombo vya moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa pensheni na mafao ya wastaafu, Wizara imeboresha mfumo wa usimamizi wa majalada ya wastaafu kwa njia ya kielekroniki ambapo moduli ya ufuatiliaji wa majadala ya wastaafu imeandaliwa ili kuboresha huduma za pensheni na mafao kwa wastaafu wanaohudumiwa na Hazina. Maboresho hayo yamewezesha majalada 148,148 kuingizwa kwenye mfumo. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara imelipa pensheni kwa wastaafu 49,407; mirathi kwa warithi na walezi 1,474; na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi 1,370 walioajiriwa kwa Masharti ya Kudumu na Malipo ya Uzeeni kwa watumishi 1,673 kwa walioajiriwa kwa mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya elimu ya juu, Katika mwaka 2022/2023, taasisi tano za mafunzo na elimu ya juu zilitarajia kudahili jumla ya wanafunzi 73,074, ikijumuisha ngazi za

Astashahada 14,017, Stashahada 19,427, Shahada 37,450 na Uzamili 2,180. Aidha, taasisi hizo zilitarajia kuendeleza wahadhiri 196, ambapo ngazi ya Uzamivu ni 158 na Uzamili 38.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ilikadiriwa kukusanya Shilingi trilioni 23.6 kuhuisha mkakati wa muda wa kati na wa muda mrefu; ukusanyaji wa mapato; kutunga upya Sheria na Kanuni za Ushauri wa Stempu na Bidhaa; kuanzisha Maabara ya Forodha; na kujenga na kutekeleza Mfumo Ulinganifu wa kusimamia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vipaumbele vya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023 ni kama ambavyo tumeviainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii ndani ya Bunge lako Tukufu pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na umma wa Watanzania kwa ujumla kwa kusikiliza hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *www.mof.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, omba pesa kwanza; Makadirio ya mapato na matumizi kwa mafungu ya Wizara pamoja na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Mwaka 2023/2024. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2023/2024, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba ridhaa ya Bunge lako Tukufu kutumia jumla ya Shilingi trilioni 15.94 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa mafungu tisa ya kibajeti. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 15.38 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 564.22 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishe shilingi bilioni 97.13 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Fungu 45 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na kiasi hicho ni shilingi bilioni 87.72 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 9.41 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu la Wizara nimeweka katika jedwali refu ambalo linaleta jumla hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 Utangulizi**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Daniel Baran Sillo – Mbunge wa Babati Vijijini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/23 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu tisa (9) ya Wizara ya Fedha na Mipango, pamoja na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2023/24.

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa umuhimu wake, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutupa wasaa wa kukutana kwa mara nyingine kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/23 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/24.

**3.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa heshima na taadhima, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini na kunipa fursa ya kuendelea kusimamia majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa mara nyingine, napenda kumhakikishia kuwa nitaendelea kutumikia kwa weledi dhamana aliyonipa ya kusimamia masuala ya uchumi, bajeti, fedha na mipango ya Taifa letu. Ni dhahiri kwamba, katika kipindi cha uongozi wake, nchi yetu imepata mafanikio makubwa kiuchumi, kijamii na kisiasa ambayo kila mmoja wetu anapaswa kujivunia na kumuunga mkono. Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima na busara katika kubadilisha fikra na mifumo ya usimamizi wa maslahi ya wananchi wakiwemo wafanyakazi, wawekezaji, wafanyabiashara, wakulima, wafugaji na wadau wa maendeleo.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii adhimu, kumpongeza Mheshimiwa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza kwa dhati ya moyo wangu, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge Viti Maalumu na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge lako Tukufu. Ninawaahidi ushirikiano thabiti katika utekelezaji wa majukumu yao ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika katika kuongoza vikao vya Bunge.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa minajili ya tukio la leo, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake, Mhe. Daniel Baran Sillo – Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Omari Mohamed Kigua - Mbunge wa Kilindi kwa maoni na ushauri wenye tija katika kuboresha usimamizi wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24. Kwa

niaba ya wizara na taasisi zake, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi waliotupa dhamana ya kusimamia masuala ya kisera katika Taifa letu.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja iliyo mbele yetu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makuu manne (4) ambayo ni: Muhtasari kuhusu majukumu ya Wizara; mwenendo wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23; vipaumbele vya wizara na taasisi zake kwa mwaka 2023/24; na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/24.

## 2.0 Majukumu ya Wizara

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 534 la Julai 2, 2021, Wizara ya Fedha na Mipango imekasimiwa majukumu yafuatayo:

i. Kusimamia sera za uchumi jumla, fedha, ununuzi wa umma na ubia kati ya sekta ya umma na binafsi:

ii. Kusimamia mipango, mikakati na miongozo ya kitaifa ya maendeleo;

iii. Kusimamia bajeti ya Serikali;

iv. Kuratibu upatikanaji wa fedha kutoka taasisi za fedha za kikanda na kimataifa kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali;

v. Kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi;

vi. Kusimamia matumizi ya fedha na mali za umma;

vii. Kusimamizi mifumo ya uendeshaji wa mashirika na taasisi za umma pamoja na vitega uchumi vya Serikali;

viii. Kusimamia masuala ya fedha ya pamoja kati ya Tanzania Bara na Zanzibar;

ix. Kusimamia mafao, pensheni na mirathi kwa wastaafu wasio wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

x. Kusimamia deni la Serikali;

xi. Kusimamia mifumo ya udhibiti wa michezo ya kubahatisha;

xii. Kusimamia maendeleo ya sekta ya fedha; na

xiii. Kusimamia takwimu rasmi za kitaifa.

## 3.0 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati nawasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/23, niliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi trilioni 14.94 kwa mafungu tisa (9) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Wizara na taasisi zake. Vipaumbele vya matumizi ya kawaida kwa Wizara tunavyoendelea kutekeleza ni:

i. Kukusanya, kutafuta na kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali;

ii. Kuhudumia deni la Serikali kwa wakati pindi linapoiva;

iii. Kufanya tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa ajili ya maandalizi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo 2050;

iv. Kufanya tathmini ya mfumo na muundo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ili kuwezesha kutungwa kwa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo;

v. Kufanya tafiti katika sekta za uzalishaji ili kuibua fursa za uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya Serikali katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu;

vi. Kuendelea kutekeleza maagizo ya Serikali ya kutafsiri sheria za Wizara na taasisi zake kwa lugha ya Kiswahili; na

vii. Kuhuisha Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Wizara inaendelea kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI);

ii. Kuandaa na kujenga ghala la takwimu (*Data warehouse*);

iii. Kuratibu na kusimamia zoezi la Sensa ya Watu na Makazi;

iv. Kuziwezesha taasisi za Wizara, hususan taasisi za elimu na mafunzo kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia;

v. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli, Mtumba Dodoma;

vi. Kujenga na kukarabati Ofisi za Wizara katika mkoa wa Geita, Njombe, Songwe, Dar es Salaam, Morogoro, Kigoma na Ruvuma.

### 3.1 Mwenendo wa Matumizi hadi Aprili 2023

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, mafungu tisa (9) ya Wizara ya Fedha na Mipango yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 14.94 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 13.62 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.32 ni kwa ajili ya matumizi

ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi trilioni 12.61 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi trilioni 1.01 kwa ajili ya matumizi ya mishahara. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha shilingi trilioni 1.28 fedha za ndani na shilingi bilioni 36.51 fedha za nje.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, fedha zilizopokelewa kwa mafungu yote tisa (9) ya wizara ni shilingi trilioni 11.75 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, sawa na asilimia 78.61 ya makadirio ya mwaka. Matumizi halisi yalifikia shilingi trilioni 11.62, sawa na asilimia 98.95 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo yalikuwa shilingi trilioni 10.07, mishahara shilingi bilioni 438.95 na maendeleo shilingi trilioni 1.12 Mchanganuo wa fedha zilizotumika kwa kila Fungu ni kama inavyoonekana katika **kiambatisho Na.1 – 3.**

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Fungu 45, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi lilipata ridhaa ya Bunge lako Tukufu ya kutumia jumla ya shilingi bilioni 89 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Hadi Aprili 2023, Ofisi imepokea jumla ya shilingi bilioni 76.42, sawa na asilimia 85 ya makisio ya mwaka 2022/23. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 12.66 zimepokelewa kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 60.59 matumizi mengineyo na shilingi bilioni 3.17 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, matumizi halisi ya mishahara yalifikia shilingi bilioni 12.66 matumizi mengineyo shilingi bilioni 57.85 na maendeleo shilingi bilioni 3.17.

### 3.2 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara

#### 3.2.1 Kukusanya, kutafuta na kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango ilikadiriwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 38.0. Kati ya kiasi hicho, Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina lilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 988.3, Fungu 21 – Hazina shilingi trilioni 37.0, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 60.1 na Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango shilingi bilioni 1.0. Aidha, kati ya kiasi kilichokadiriwa kukusanywa na Fungu 21, shilingi trilioni 23.6 ni mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi

yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, shilingi trilioni 4.6 ni misaada na mikopo yenye masharti nafuu na shilingi trilioni 8.8 ni mikopo yenye masharti ya kibiashara ikiwemo hatifungani za Serikali.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 30.24, sawa na asilimia 81.5 ya makadirio ya mwaka 2022/23. Kati ya kiasi hicho, Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina limekusanya shilingi bilioni 704.2, Fungu 21 – Hazina shilingi trilioni 29.37, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 1.2 na Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango shilingi milioni 439.83. Aidha, kati ya kiasi kilichokusanywa na Fungu 21, shilingi trilioni 18.8 ni mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi aliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, shilingi trilioni 4.61 ni misaada na mikopo yenye masharti nafuu na shilingi trilioni 5.96 ni mikopo yenye masharti ya kibiashara ikiwemo hatifungani za Serikali.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2023, wizara imechukua hatua mbalimbali ili kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali pamoja na mali za umma. Hatua hizo ni pamoja na: kuimarisha doria kwenye mipaka yote nchini ili kudhibiti ukwepaji kodi na biashara za magendo; kuendelea kuboresha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA (EFDMS, TANCIS, ITAX) ili kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato; kuendelea na kampeni mbalimbali za kutoa elimu kwa mlipakodi kupitia semina, makongamano na vyombo vya habari ili kuongeza uelewa na uhiari wa kulipa kodi; na kuendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine zilizochukuliwa na wizara kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za umma ni pamoja na kuunganisha Mfumo wa MUSE na kuanza kutumika katika Ofisi za Balozi 11 ambazo ni Ubalozi wa Tanzania Lagos - Nigeria; New York - Marekani; Ottawa-Canada; Riyadhi - Saudi Arabia; Muscat - Oman; Seoul-Korea Kusini; Kuwait - Kuwait; Kuala Lumpur - Malaysia; Washington - Marekani; na Brasilia - Brazil; kuboresha Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani; kuandaa Mpango Mahsusi wa Ukaguzi; kuhakiki madeni ya chakula kwa shule za msingi na sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 45; kuhakiki mikopo

inayotolewa na Serikali kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; kuhakiki madeni ya ununuzi wa pamba msimu wa mwaka 2019/20 pamoja na madeni ya watoa huduma ya pembejeo; kuhakiki fedha za ujenzi wa soko la kisasa katika Manispaa ya Morogoro na deni la mshauri elekezi wa Shirika la Reli; kufanya ukaguzi wa Mfumo wa Mapato wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro; kuhakiki madeni ya Soko la Kariakoo; kuhakiki madeni ya wazabuni wa vifaa kwenye mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Uhuru, Jengo la utawala na Kituo cha Afya Mlowa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino; kuhakiki taarifa za malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma na wastaafu; na kuhuisha kumbukumbu za mali za taasisi 537 zenye thamani ya shilingi trilioni 68.891 kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali.

### 3.2.2 Kuhudumia deni la Serikali

**17. *Mheshimiwa Spika,*** kupitia Fungu namba 001, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi trilioni 9.1 kwa ajili ya kuhudumia deni la Serikali pindi linapoiva. Hadi Aprili 2023, wizara imelipa kwa wakati notisi za madai ya deni lililoiva la jumla ya shilingi trilioni 7.4, sawa na ufanisi wa asilimia 82 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 4.4, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.7 na mtaji shilingi trilioni 2.7. Aidha, deni la nje ni shilingi trilioni 3, ikijumuisha riba shilingi trilioni 0.8 na mtaji shilingi trilioni 2.2.

### 3.2.3 Kufanya tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na maandalizi ya Dira 2050

**18. *Mheshimiwa Spika,*** wizara imekamilisha taratibu za ununuzi wa mtaalamu elekezi kwa ajili ya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambapo mtaalamu elekezi amewasilisha taarifa ya awali Aprili 2023 na anatarajiwa kukamilisha tathmini husika ifikapo Agosti 2023. Sambamba na zoezi la tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, wizara inaendelea na taratibu za maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambapo mchakato rasmi ulizinduliwa Aprili 2023. Aidha, warsha elekezi kwa wajumbe wa timu za uandishi na uhariri wa dira ilifanyika Mei 2023 Jijini Dar es salaam. Kipekee, napenda kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu, Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwongozo wake thabiti ambao umetuwezesha kuanza kwa wakati maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**3.2.4 Kufanya tathmini ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo**

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako Tukufu liliridhia mapendekezo ya Wizara ya kufanya tathmini ya mfumo na muundo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo ili kubaini kama kuna uhitaji wa kuandaa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi na Programu za Maendeleo.

Hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kukusanya maoni na mapendekezo kutoka Wizara za kisekta, taasisi na mashirika ya umma, Bunge, vyuo vikuu na vyuo vya kati, taasisi za utafiti na washirika wa maendeleo. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kufanya uchambuzi na kuandaa mapendekezo kulingana na maoni ya wadau pamoja na miongozo ya maandalizi ya nyaraka za Serikali.

**3.2.5 Kufanya tafiti ili kuibua fursa za uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya Serikali**

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango ilipata ridhaa ya Bunge ya kufanya tafiti mbalimbali ili kuibua fursa za uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya Serikali. Napenda kutoa taarifa kuwa hadi Aprili 2023, wizara imekamilisha tafiti mbili (2) ambazo ni upatikanaji wa huduma ndogo za fedha na mchango wake katika ukuaji wa shughuli za kiuchumi na matokeo yake katika kupunguza kiwango cha umaskini kwa makundi maalumu pamoja na utafiti kuhusu ufanisi katika ukusanyaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na tafiti zilizokamilika, wizara ipo katika hatua mbalimbali kukamilisha tafiti zifuatazo: Utafiti kuhusu mnyororo wa huduma za utalii nchini; upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya maendeleo; mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ardhi; na utafiti kuhusu uchumi wa kidijitali na matokeo yake katika matumizi ya

fedha taslimu katika ununuzi wa bidhaa na huduma. Vilevile, wizara imefanyia kazi mapendekezo ya wadau kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi ambayo hayakuridhiwa na Serikali katika mwaka 2022/23, tathmini ya ufanisi wa misamaha ya kodi katika uchumi na mfumo wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Matokeo ya tafiti na tathmini zilizofanyika yatatumika kuboresha mazingira ya uwekezaji, biashara na mifumo ya usimamizi wa mipango, mapato na matumizi ya Serikali.

### 3.2.6 Utekelezaji wa agizo la Serikali la kutafsiri sheria za Wizara na taasisi zake kwa lugha ya Kiswahili

**22. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2022/23, Bunge lako Tukufu liliridhia mpango wa Wizara wa kuendelea kutafsiri sheria zake kwa lugha ya Kiswahili. Hadi Aprili 2023, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kutafsiri sheria saba (7) ambazo ni Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura 148, Sheria ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286, Sheria ya PPP, Sura 103, Sheria ya Usimamizi ya Ushuru wa Forodha, Sura 147, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197, Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Umiliki wa Magari, Sura 124 na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134.

### 3.2.7 Kuhuisha Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi

**23. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kuhuisha miongozo ya usimamizi wa vihatarishi na udhibiti wa ndani ili kuimarisha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi katika sekta ya umma. Hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kuhuisha Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi wa Mwaka 2012, Mwongozo wa Usimamizi wa Viashiria vya Udanganyifu wa Mwaka 2015 na Mwongozo wa Usimamizi wa Udhibiti wa Ndani ili kuendana na miongozo ya kimataifa. Kazi nyingine iliyofanyika ni kuhuisha mwongozo wa ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu.

### 3.2.8 Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma

**24. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, Mfumo wa Malipo Serikalini - *MUSE* umeboreshwa na kufungamanishwa na Mfumo wa Taarifa za Watumishi wa Umma - HCMIS ili kusomana na kubadilishana taarifa; kuboresha Mfumo wa D-Fund MIS kwa kuunganisha na Mfumo wa Benki Kuu ya Tanzania (*Central Banking Systems -CBS*) ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za fedha za miradi zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi na Washirika wa Maendeleo; na kuboresha Mfumo wa GARI–ITS sambamba na kuhuisha taarifa za taasisi za umma 463. Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma inaendelea kuunda na kujenga mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma ili kuimarisha udhibiti wa fedha za umma. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa moduli ya kusimamia mpango wa ununuzi wa mwaka, moduli ya kuanzisha mchakato wa ununuzi, moduli ya usanifu wa nyaraka za zabuni ndani ya mfumo na usanifu wa nyaraka za kusaini kidijitali ndani ya mfumo, moduli ya uwekaji wa bei kikomo, moduli ya kutumia mfumo wa simu za kiganjani (*Mobile App*) na moduli ya usajili wa zabuni. Vilevile, mfumo umefungamanishwa (integrated) na mifumo mingine tisa (9) ya taasisi za Serikali ikiwemo *TRA TIN, CRB MIS, PLANREP, MUSE, BRELA OTRS, PSPTB MIS, ERB MIS, ERMS*, na *GePG* na unatarajiwa kuanza kutumika Julai 2023.

### 3.2.9 Kuandaa na kujenga ghala la takwimu (*Data warehouse*)

**25. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kuandaa na kujenga ghala la takwimu ili kurahisha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji wa mipango na bajeti ya Serikali. Hadi Aprili 2023, wizara imekamilisha hatua ya awali ya kuainisha mahitaji na vyanzo vya taarifa na takwimu zitakazohifadhiwa kwenye ghala. Mahitaji hayo yamewezesha kuanza kazi ya usanifu na ujenzi wa ghala.

### 3.2.10 Kuratibu na kusimamia zoezi la Sensa ya Watu na Makazi

**26. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, tulikuwa na agenda ya kitaifa ya Sensa ya Watu na Makazi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa jumla kuwa zoezi la Sensa ya

Watu na Makazi lilifanyika kwa mafanikio makubwa sana. Baada ya uzinduzi wa matokeo ya mwanzo ya Sensa, ripoti nyingine kumi (10) za Sensa ya Watu na Makazi zilizojikita katika mgawanyo wa idadi ya watu katika maeneo ya kiutawala, mgawanyo wa idadi ya watu kwa umri na jinsi na mgawanyo wa idadi ya watu katika majimbo ya uchaguzi zilizinduliwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Zanzibar Aprili 15, 2023. Aidha, takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 zimetumika katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023. Hatua inayoendelea, ni kusambaza ripoti kwa wadau, kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu za Sensa ya Watu na Makazi, kufuatilia utekelezaji wake na kuendelea kuchakata, kuchambua na kuandaa ripoti nyingine za kisekta kulingana na ratiba ya kutoa machapisho ya Sensa. Kwa niaba ya Serikali, natoa wito kwa wadau wote kufuatilia na kutumia takwimu za Sensa ya Watu na Makazi kusimamia mipango yao.

### 3.2.11 Kuziwezesha taasisi za Wizara, hususan taasisi za elimu na mafunzo kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunza

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia mapinduzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya elimu, ngazi ya elimumsingi na sekondari na kusababisha ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo vya elimu ya juu, wizara ilipata ridhaa ya Bunge lako Tukufu kutumia **shilingi bilioni 19** kupitia bajeti yake ya maendeleo ili kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika taasisi tano (5) za elimu ya juu zilizo chini ya wizara. Hadi Aprili 2023, taasisi hizo zimepokea jumla ya **shilingi bilioni 11.83,** sawa na **asilimia 62.27** ya makadirio ya mwaka 2022/23.

### 3.2.12 Kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli, Mtumba Dodoma

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, wizara inaendelea na ujenzi wa jengo lake katika Mji wa Magufuli, Mtumba Dodoma. Hadi Aprili 2023, utekelezaji umefikia **asilimia 42.25** ambapo ujenzi unatarajiwa kukamilika Septemba 2023. Kazi zilizokamilika hadi sasa ni ujenzi wa mihimili ya *basement,* mihimili ya sakafu ya chini katika jengo kuu, na mihimili ya ghorofa ya kwanza hadi ghorofa ya tisa pamoja

sakafu na mihimili ya kumbi. Aidha, kazi zinazoendelea ni nakshi ya kuta na sakafu, ufungaji wa viyoyozi, vifaa vya kuzima moto, mifumo ya umeme, majitaka na maji safi pamoja na ujenzi wa jiko, sehemu ya mapokezi na mgahawa.

**3.2.13 Kujenga na kukarabati miundombinu ya Wizara mkoa wa Geita, Njombe, Songwe, Dar es Salaam, Morogoro, Kigoma na Ruvuma.**

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kujenga ofisi katika mikoa ya Geita, Njombe na Songwe na kukarabati majengo ya ofisi katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Kigoma na Ruvuma. Hadi Aprili 2023, mkataba kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi wa ofisi Geita umethibitishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, ujenzi wa ofisi katika mkoa wa Njombe na Songwe umefikia hatua ya mshauri elekezi kupewa zabuni kwa ajili ya usanifu wa michoro na kusimamia ujenzi. Vilevile, ukarabati wa ofisi katika mkoa wa Morogoro umekamilika na mkoa wa Dar es salaam pamoja na Kigoma umefikia asilimia 90 na asilimia 43 mtawalia.

**3.3 Mwenendo wa Utekelezaji wa Majukumu Mengine ya Wizara**

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa vipaumbele vya wizara kwa mwaka 2022/23, kazi nyingine zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu na kutekelezwa kwa ufanisi ni kama ifuatavyo:

**3.3.1 Uandaaji wa Mipango, Sheria na Miongozo ya Kisera**

**31.** ***Mheshimiwa Spika*****,** hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kuandaa mipango, sheria na miongozo mbalimbali ya kisera na kitaalamu ikiwemo: Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24; kuhuisha Mwongozo wa Wizara wa Usimamizi wa Vihatarishi; mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya PPP, Sura 103 ambapo muswada uliwasilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge la Februari, 2023; na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 ambayo yameridhiwa na Baraza la Mawaziri. Aidha, Ofisi

ya Msajili wa Hazina inaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ambapo hatua iliyofikiwa ni kukusanya maoni na mapendekezo ya wadau kuhusu changamoto, udhaifu na fursa za vitega uchumi vya Serikali.

### 3.3.2 Uhakiki, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kufuatilia na kuhakiki fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo Bararaba ya Masasi hadi Mtwara (160km), ujenzi wa barabara ya Tanga-PanganiBagamoyo sehemu ya Mkange-Mandamazingira, Reli ya kisasa kutoka Isaka hadi Mwanza, Mabasi yaendayo Haraka Awamu ya Pili – Ubungo Kisiwani, Njia za kusafirisha umeme kutoka Chalinze, Morogoro hadi Dodoma, Iringa hadi Sumbawanga na Wilaya ya Monduli hadi Makuyuni. Aidha, Wizara imefanikiwa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo 222 katika mikoa 17 ya Kagera, Kigoma, Geita, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Katavi, Rukwa, Mara, Simiyu, Dar es Salaam, Morogoro na Pwani. Kati ya miradi hiyo, miradi nane (8) ya kielelezo ambayo ni: Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere - MW 2,115; Reli ya *Standard Gauge*; Kiwanda cha kusindika sukari – Mkulazi; kufufua Shirika la Ndege la Taifa; mpango wa ununuzi wa meli za uvuvi katika Bahari Kuu; ujenzi wa Bandari ya Uvuvi; Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima, Uganda hadi bandari ya Tanga-Chongoleani na daraja la Kigongo-Busisi. Vilevile, wizara imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 16 inayosimamiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa katika mikoa tisa (9), ambayo ni Kilimanjaro, Mwanza, Pwani, Tanga, Ruvuma, Njombe, Dar es Salaam, Arusha na Morogoro.

### 3.3.3 Kuanzisha Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kuanzisha Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi (*Tax Ombudsman Office*). Hadi Aprili 2023, muundo na mgawanyo wa majukumu ya Ofisi hiyo umeandaliwa na kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha,

watumishi watakaohudumu katika Ofisi hiyo wamepatikana na kuanza kazi rasmi Februari 2023. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kuandaa mifumo ya usimamizi wa malalamiko na taarifa za wadau pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya Ofisi na umuhimu wake katika kuimarisha utawala wa sheria na utawala bora katika tasnia ya masuala ya kodi.

### 3.3.4 Usimamizi wa Deni la Serikali

**34. *Mheshimiwa Spika,*** wizara inaendelea kusimamia deni la Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134. Ili kuwa na taarifa sahihi kuhusu udhibiti wa deni la Serikali, wizara imefanya tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali kwa miaka 20 ijayo, kuanzia 2022/23 hadi 2041/42. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Aidha, taarifa inaonesha kuwa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 31.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, wananchi na wadau wote wa maendeleo kuwa Taarifa kamili inapatikana katika tovuti ya wizara ambayo ni *www.mof.go.tz.*

### 3.3.5 Ushauri wa Kitaalamu kwa Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi

**35. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, wizara imetoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu ili kuziwezesha Mamlaka za Serikali kuandaa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa utaratibu wa PPP. Ushauri na mafunzo umekuwa na matokeo chanya ambapo, Wakala wa Barabara Tanzania umeweza kukamilisha maandalizi ya mradi wa barabara ya haraka ya tozo kutoka Kibaha hadi Morogoro (205 Km) na hatua za ununuzi wa mbia zinaendelea. Aidha, majadiliano na mbia aliyepatikana kwa ajili ya uendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam yanaendelea. Vilevile, Chuo cha Elimu ya Biashara kinakamilisha taarifa ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa kujenga mabweni ya wanafunzi na Jeshi la Polisi linakamilisha upembuzi yakinifu kwa Mradi wa Ukaguzi wa Lazima wa Vyombo vya Moto.

### 3.3.6 Huduma za Pensheni na Mafao ya Wastaafu

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, wizara imeboresha mfumo wa usimamizi wa majalada ya wastaafu kwa njia ya kielekroniki ambapo moduli ya ufuatiliaji wa majadala ya wastaafu imeandaliwa ili kuboresha huduma za pensheni na mafao kwa wastaafu wanaohudumiwa na Hazina. Maboresho hayo yamewezesha majalada 148,148 kuingizwa kwenye mfumo. Aidha, katika kipindi hicho, wizara imelipa pensheni kwa wastaafu 49,407, mirathi kwa warithi na walezi 1,474 na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi 1,370 walioajiriwa kwa masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni kwa watumishi 1,673 walioajiriwa kwa mikataba.

### 3.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Taasisi za Wizara

**37.** ***Mheshimiwa Spika*,** wizara inatekeleza baadhi ya majukumu yake kupitia taasisi zake za elimu na mafunzo, bodi za kitaalamu na kitaaluma, usimamizi wa fedha, kodi, bima, ununuzi na ugavi, michezo ya kubahatisha, uwekezaji na uwezeshaji pamoja na takwimu.

### 3.4.1 Taasisi za Mafunzo na Elimu ya Juu

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23**,** taasisi tano (5) za mafunzo na elimu ya juu zilitarajia kudahili jumla ya wanafunzi 73,074, ikijumuisha ngazi za astashahada 14,017, stashahada 19,427, shahada 37,450 na uzamili 2,180. Aidha, taasisi hizo zilitarajia kuendeleza wahadhiri 196, ambapo ngazi ya uzamivu ni 158 na uzamili 38.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, jumla ya wanafunzi 70,638 wamedahiliwa na taasisi zote tano (5), sawa na asilimia 96.7 ya lengo. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, 13,916 ni ngazi ya cheti, stashahada 16,470, shahada ya awali 37,057 na uzamili 31,195. Aidha, jumla ya wahadhiri 159 wamewezeshwa kujiendeleza katika masomo ambapo 144 ni ngazi ya uzamivu na 15 ni uzamili.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Usimamizi wa Fedha kilipanga kukamilisha ujenzi wa mabweni manne (4) yenye ghorofa moja kila moja yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400, nyumba nne (4) zenye uwezo wa kuhudumia familia nane (8) za wafanyakazi pamoja na maktaba moja (1) katika kampasi ya Geita; kuendelea na ukarabati wa miundombinu katika kampasi ya Dar es Salaam na ujenzi wa jengo la taaluma likijumuisha ofisi zenye uwezo wa kuhudumia wahadhiri 40 na madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,520 kwa wakati mmoja katika kampasi ya Mwanza. Hadi Aprili 2023, ukarabati katika kampasi kuu umefikia asilimia 88 na ujenzi wa mabweni na nyumba za watumishi katika kampasi ya Geita umefikia asilimia 30 na asilimia 68 mtawalia. Aidha, ujenzi wa kampasi ya Mwanza umefikia asilimia 3.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Chuo cha Uhasibu Arusha kilipata ridhaa ya kuendelea na ujenzi wa mabweni manne (4) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,000 katika kampasi kuu Arusha; kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala linalojumuisha madarasa 17 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2210 kwa wakati mmoja, mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na jengo moja (1) la utawala katika kampasi ya Babati; na kufanya mapitio ya mitaala 10. Hadi Aprili 2023, ujenzi wa mabweni katika kampasi ya Arusha umefikia asilimia 30, madarasa asilimia 99 na ujenzi wa jengo la utawala na mabweni katika kampasi ya Babati umefikia asilimia 55 na asilimia 20 mtawalia. Aidha, kazi ya mapitio ya mitaala imekamilika.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kilipanga kufanya tafiti saba (7) na kutoa huduma za ushauri elekezi kwa kuzingatia mahitaji ya wadau; kuwezesha mafunzo kwa watumishi 396; kukarabati nyumba 13 za watumishi katika kampasi kuu Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi na maktaba katika Kituo cha Mafunzo, Kanda ya Ziwa Mwanza. Hadi Aprili 2023, Chuo kimefanikiwa kufanya tafiti saba (7), kutoa huduma elekezi tatu (3), kujengea uwezo watumishi 48, kukarabati nyumba za watumishi mbili (2) na ujenzi wa bweni la wanafunzi na maktaba

katika Kituo cha Mafunzo, Kanda ya Ziwa Mwanza umefikia asilimia 92 na asilimia 15 mtawalia.

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Taasisi ya Uhasibu Tanzania ilipanga kujenga jengo moja la utawala katika kampasi ya Misungwi, Mwanza na kampasi ya Kigoma; jengo moja (1) linalojumuisha ukumbi wa mihadhara, maabara ya kompyuta na maktaba katika Kampasi ya Mbeya; na kuboresha miundombinu na huduma mtandao wa *internet* katika maktaba za kampasi zote. Hadi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi wa jengo la utawala kampasi ya Misungwi, Mwanza umefikia asilimia 72 na Kigoma utekelezaji umefikia hatua ya mkandarasi kukabidhiwa eneo la mradi. Aidha, ujenzi wa jengo katika kampasi ya Mbeya umefikia asilimia 72. Vilevile, maktaba za kampasi zote zimeboreshwa kwa kuunganishwa na huduma ya mtandao wa *internet*.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kilipanga kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala, kuendeleza wahadhiri 28 na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 20. Hadi Aprili 2023, ujenzi wa jengo la utawala umefikia asilimia 34, kuendeleza wahadhiri 28 katika shahada ya uzamivu na kuwajengea uwezo watumishi 9 katika maeneo mbalimbali.

### 3.4.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ilitarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi, kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 6,500 na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000. Aidha, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ilitarajia kusajili wahasibu 1,125 katika ngazi mbalimbali, kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma, kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi 75 na kutoa mafunzo ya stashahada ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha serikalini kwa wahitimu 500.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi imesajili wataalamu 1,790, sawa na asilimia 51.2, kuendesha mafunzo na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa

wataalamu 2,508, sawa na asilimia 38.8 na kuendesha mitihani kwa watahiniwa 2,416, sawa na asilimia 60.4. Aidha, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu imesajili wahasibu na wakaguzi 1,200, kufanya kaguzi za ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi 68 na kutoa mafunzo ya stashahada ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha Serikalini kwa wahitimu 191 na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 6,988. Vilevile, ujenzi wa jengo la Ofisi Dodoma umeanza ambapo mtaalamu mshauri ameanza kazi za kuandaa michoro na upimaji wa mitetemo.

### 3.4.3 Taasisi za Usimamizi wa Kodi

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA ilikadiriwa kukusanya shilingi trilioni 23.6, kuhuisha Mkakati wa Muda wa Kati na Mrefu wa Ukusanyaji Mapato, kutunga upya Sheria na Kanuni za Ushuru wa Stempu na Bidhaa, kuanzisha Maabara ya Forodha, kujenga na kutekeleza Mfumo Unganifu wa Kusimamia Mapato ya Ndani na kuboresha Kituo cha Udhibiti na Ufuatiliaji wa Mifumo. Aidha, Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi zilitarajia kuendelea kusajili, kusikiliza na kutoa maamuzi ya maombi, mashauri na rufaa za kodi ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya shilingi trilioni 18.8, sawa na ufanisi wa asilimia 79.5 ya lengo la mwaka. Aidha, Mamlaka imefanikiwa kukusanya mapendekezo ya kuboresha Mkakati wa Muda wa Kati na Mrefu wa Ukusanyaji wa Mapato, kuandaa rasimu ya mapendekezo ya kufuta na kutunga upya Sheria ya Usimamizi na Viwango vya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147, kuboresha moduli za mfumo jumuishi wa ukusanyaji wa kodi za ndani ikiwemo dirisha moja la walipakodi, moduli ya usajili wa walipakodi na moduli ya marejesho ya kodi.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Rufaa za Kodi imefanikiwa kusikiliza mashauri 423 yenye thamani ya kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi 849,833,566,607.32, kati ya mashauri 1,155 yaliyosajiliwa yenye kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi 7,353,710,702,899.13 na dola za Marekani 5,215,587.43. Kati

ya maamuzi yaliyotolewa, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeshinda mashauri 344 yenye thamani ya kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi 824,127,927,989 na walipakodi kushinda mashauri 79 yenye thamani ya kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi 25,705,638,617.92. Aidha, Baraza la Rufaa za Kodi limefanikiwa kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri 87 yenye thamani ya kodi inayobishaniwa ya shilingi 237,713,052,269.93 na dola za Marekani 2,926,106.65 ikiwa ni sehemu ya mashauri 244 yaliyosajiliwa. Kati ya maamuzi yaliyotolewa na Baraza, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeshinda mashauri 74 yenye thamani ya shilingi 234,202,004,437.38 na walipa kodi kushinda mashauri 13 yenye thamani ya shilingi 3,511,046,832.93 na dola za Marekani 2,926,106.65.

### 3.4.4 Bodi ya Michezo ya Kubahatisha

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ilitarajia kutoa leseni 7,697 kwa waendesha michezo ya kubahatisha, ambapo 1,923 ni leseni mpya na 5,774 ni leseni za kuhuishwa; kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 83; kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Michezo ya kubahatisha; na kurejesha Bahati Nasibu ya Taifa. Hadi Aprili 2023, Bodi imetoa jumla ya leseni 8,778 sawa na asilimia 114 ambapo leseni mpya 3,658 na zilizohuishwa 5,120, kufanya kaguzi 88, sawa na asilimia 106, kuandaa mapendekezo ya mapitio ya Sheria na Kanuni za Michezo ya kubahatisha. Aidha, uteuzi wa kampuni ya kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa upo katika hatua za mwisho na unatarajiwa kukamilika Juni 2023 ambapo uendeshaji utaanza katika mwaka 2023/24.

### 3.4.5 Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipanga kuanza kusimamia masoko ya mitaji kwa kutumia mfumo wa vihatarishi, kupanua wigo wa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa pamoja na kuongeza idadi ya bidhaa katika soko, hususan hisa, hatifungani na vipande katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania lilipanga kutoa elimu

kwa umma na kuboresha mfumo wa mauzo kulingana na mazingira ya bidhaa husika.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2023, Mamlaka imefanikiwa kuanza kutumia mfumo wa vihatarishi katika usimamizi wa masoko ya mitaji, kutoa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji kwa wadau wapatao milioni 1.2 na kuongeza bidhaa mpya 47 katika masoko ya mitaji kutoka 637 na kufikia 684, ambazo zinajumuisha hisa; hatifungani; na mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania limetoa elimu kwa wadau 190,954 katika mikoa ya Manyara, Simiyu, Rukwa, Morogoro, Mbeya, Kagera, Mwanza, Tabora, Mara, Lindi, Songwe na Shinyanga. Vilevile, Soko limeendelea kuboresha mfumo wa biashara kwa njia ya kielekitroniki ili kuwezesha uuzaji wa mazao mapya ikiwemo chai, pamba, mkonge pamoja na mifugo hai na ngozi. Mpaka sasa mfumo una uwezo wa kuwezesha uuzaji na ununuzi wa ufuta, choroko, dengu, korosho, kakao, kahawa na mbaazi.

### 3.4.6 Taasisi za kibenki

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Benki Kuu ya Tanzania ilipanga kuchochea na kudhibiti ustawi wa viashiria vya uchumi jumla, kukuza wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ili kuendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi, kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kudhibiti na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu pamoja na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4). Hadi Aprili 2023, wastani wa ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 17.2 dhidi ya lengo la asilimia 10.3, na mfumuko wa bei ulifikia asilimia 4.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 5 hadi 7. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 22.5 ikilinganishwa na lengo la asilimia 10.7. Mwenendo mzuri wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi umetokana na kuimarika kwa mahitaji ya mikopo mipya kufuatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara na usimamizi imara wa sera za fedha na bajeti. Kiwango cha mikopo chechefu kilipungua kufikia asilimia 5.5 dhidi ya lengo la asilimia 5. Vilevile, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa katika viwango vya

kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi katika kipindi kisichopungua miezi minne (4).

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilitenga shilingi bilioni 36.1 kwa ajili ya mikopo kwa miradi ya kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, shilingi bilioni 77.45 kwa ajili ya mikopo ya utekelezaji wa miradi ya kuzuia upotevu wa mazao baada ya kuvuna na shilingi bilioni 90 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuwezesha ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya kilimo. Aidha, Benki ilipanga kushawishi benki nne (4) za biashara kushiriki katika mfuko wa dhamana ili kuchagiza uwekezaji katika sekta ya kilimo.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Desemba 2022, shilingi bilioni 33.22 zilitolewa kupitia mfumo wa ukopeshaji wa moja kwa moja kwa miradi inayolenga kuongeza tija katika uzalishaji; shilingi bilioni 44.2 zilikopeshwa kwa wakulima wadogo kwa ajili ya miradi ya kuzuia upotevu wa mazao ambapo kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 35.9 zilitolewa kupitia mfumo wa ukopeshaji wa moja kwa moja na shilingi bilioni 8.3 kupitia mfuko wa dhamana. Aidha, shilingi bilioni 97.7 zilikopeshwa kwa wakulima wadogo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuwezesha upatikanaji wa masoko ya mazao ambapo kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 81.3 zilitolewa kwa mfumo wa ukopeshaji wa moja kwa moja na shilingi bilioni 16.4 zilitolewa kupitia mfuko wa dhamana. Vilevile, ili kuchagiza uwekezaji katika sekta ya kilimo, benki ilifanikiwa kushawishi benki moja (1) ya biashara kujiunga katika mfuko wa dhamana wa wakulima wadogo.

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022, Benki ya Maendeleo TIB ilipanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 47 katika sekta ya viwanda, maji, nishati, miundombinu ya viwanda, miundombinu ya serikali za mitaa, madini, mafuta na gesi, huduma, utalii na kilimo; kukuza mizania ya benki kufikia kiasi cha shilingi bilioni 902.63; kupunguza ukwasi kwa kuongeza mtaji wa benki kwa shilingi bilioni 373 na kuuza hati fungani zenye thamani ya shilingi bilioni 300. Hadi Desemba 2022, Benki imefanikiwa kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 13.71 katika Sekta za maji, utalii, nishati/umeme, kilimo, pamoja na huduma za usafiri na mawasiliano. Aidha, mizania ya benki ilikua na kufikia shilingi bilioni

487.75. Hata hivyo, Benki haikuweza kufikia malengo yake kutokana na changamoto ya mtaji, ukwasi na athari ya kiwango cha mikopo chechefu.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022, Benki ya Biashara ya Tanzania ilipanga kuongeza mapato kufikia shilingi bilioni 185.6, kukuza faida ya Benki kabla ya kodi kufikia shilingi bilioni 21.4, kutoa mikopo salama ya shilingi bilioni 709, kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 974, kukuza mali za Benki kufikia shilingi bilioni 1,257 na kukuza thamani ya hisa kufikia shilingi bilioni 128. Hadi Desemba 2022, Benki imeongeza mapato kufikia shilingi bilioni 174, faida kabla ya kodi shilingi bilioni 11.2, mikopo salama shilingi bilioni 842, amana zenye thamani ya shilingi bilioni 987, mali za Benki kufikia shilingi bilioni 1,290 na thamani za hisa kufikia shilingi bilioni 116.

### 3.4.7 Taasisi za Bima

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilipanga: kufanya uchambuzi wa mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 30 za bima nchini; kufanya ukaguzi wa kampuni 30 za bima, madalali 70, benki wakala 26 na mawakala 278; kufanya upekuzi wa kina ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato kwa kampuni 10; kutoa elimu ya bima kwa watu takribani milioni 1.5 kuhusu huduma za bima; na kuhamasisha kampuni za bima kuandaa bidhaa zinazolenga kuchochea kinga dhidi ya vihatarishi vya shughuli za kilimo.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, Mamlaka imefanikiwa kuchambua mikataba 255 ya bima mtawanyo kwa kampuni 32, kufanya ukaguzi wa kampuni 10, madalali 11, mawakala 358 na benkiwakala 10. Aidha, mafanikio mengine yaliyopatikana ni upekuzi wa kampuni 10 za bima, kutoa elimu ya bima kwa wananchi takribani 953,816 kupitia njia mbalimbali ikiwemo semina, maonyesho, mikutano na vyombo vya habari na kuidhinisha bidhaa mpya nne (4) za kinga dhidi ya shughuli za kilimo ambazo ni Mtumbwi Salama (Jubilee Insurance Company), Mkulima (Alliance Insurance Company), *Livestock Insurance* (UAP Insurance Company) na *Agriculture* (Heritage Insurance Company).

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Taifa la Bima lilitarajia kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa huduma zake, kubuni bidhaa mpya nne (4) na kuandaa mfumo wa usimamizi wa vihatarishi. Hadi Aprili 2023, Shirika limetoa elimu kwa kampuni, mashirika na taasisi 63 na kuingiza sokoni bidhaa mpya za BimaLife na Linda Mjengo. Aidha, Shirika limefanikiwa kuandaa mfumo wa kusimamia vihatarishi.

### 3.4.8 Taasisi za Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS ilipanga kuongeza rasilimali za mifuko kwa kiwango cha asilimia 15, kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5 na kuhamasisha taasisi za Serikali, mifuko ya hifadhi za jamii, mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS kujiunga na mifuko ya UTT AMIS. Aidha, Mfuko wa SELF ulipanga kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shillingi bilioni 43.5 kwa wajasiriamali 28,255, kuhakikisha kiwango cha urejeshaji wa mikopo kinafikia asilimia 95 na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wadau au wanufaika 4,000.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, UTT-AMIS imeongeza rasilimali za mifuko kwa shilingi bilioni 465, sawa na ongezeko la asilimia 46.6 ambapo thamani ya mifuko imefikia shilingi bilioni 1,461.5. Aidha, katika kipindi hicho, idadi ya wawekezaji katika mifuko imeongezeka kutoka 201,574 hadi 241,264, sawa na ongezeko la asilimia 19.7. Vilevile, Kampuni inaendelea kutoa elimu kuhusu faida za mifuko ya uwekezaji wa pamoja kwa vikundi vya kijamii ambapo vikundi 239 vimejiunga na mifuko ya *UTT AMIS*.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mfuko wa SELF umetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 34.4 kwa wanufaika 20,528. Aidha, mafunzo kuhusu ujuzi wa biashara, usimamizi wa kumbukumbu za kimsingi na usimamizi wa mikopo binafsi yalitolewa kwa vikundi 2,363 na urejeshaji wa mikopo iliyotolewa na mfuko umefikia asilimia 92.4 ya lengo.

### 3.4.9 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

**64. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipata ridhaa ya Bunge lako Tukufu kukamilisha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi, kufanya utafiti wa Sekta isiyo rasmi na utafiti wa Afya ya Mama na Mtoto na kuendelea kutoa takwimu za msingi za uchumi kila mwezi, robo mwaka na nusu mwaka kulingana na aina ya takwimu. Hadi Aprili 2023, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanikiwa kusimamia kwa weledi zoezi la Sensa ya Watu na Mkazi na matokeo rasmi yalizinduliwa Aprili 15, 2023. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kutoa kwa wakati takwimu za mwenendo wa uchumi ambapo takwimu za Pato la Taifa zimetolewa hadi Desemba 2022 na mfumuko wa bei hadi Aprili 2023. Vilevile**,** Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar imefanya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria kwa Mwaka 2022 katika kipindi cha Februari hadi Julai 2022 ambapo Taarifa ya Viashiria Muhimu kulingana na utafiti huo imetolewa rasmi Januari 2023.

### 3.4.10 Usimamizi na Udhibiti wa Ununuzi wa Umma

**65. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilipanga kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma na ukarabati wa ofisi ya kanda Jijini Dar es Salaam, kuwezesha mafunzo kwa watumishi 940 kutoka katika taasisi nunuzi 170 na wazabuni 1,200 ambao wamejisajili katika mfumo wa TANePS, kufanya mapitio na kuanza ujenzi wa mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao na kufanya kaguzi za ukidhi na thamani ya fedha kwa taasisi nunuzi 180. Aidha, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini ulipanga kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Kigoma, kituo cha mafuta katika mikoa ya Njombe, Pwani, Arusha na Wilaya ya Kahama na ujenzi wa ghala katika Wilaya ya Korogwe, Masasi na Dodoma. Vilevile, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni ilipanga kuandaa mfumo wa kielektroniki wa usajili na usimamizi wa rufaa za ununuzi wa umma na kufanya mapitio ya kanuni za rufaa.

**66. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imeendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao

Makuu Jijini Dodoma ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 49.9. Ukarabati wa Ofisi ya Kanda Dar es Salaam umekamilika na Jengo limeanza kutumika. Aidha, Mamlaka imetoa mafunzo kwa wazabuni 214 na watumishi 691 kutoka katika taasisi nunuzi 113 kuhusu matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma na mafunzo ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, SURA 410 kwa washiriki 1,377 kutoka katika taasisi 210, Vilevile, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni imefanya mapitio ya kanuni za usikilizaji wa rufaa, kanuni hizo zitaanza kutumika baada kukamilika kwa maboresho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na kanuni zake.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini umewezesha ununuzi wa pamoja wa magari 802 na pikipiki 1,103 za Serikali kwa gharama ya shilingi 127,367,937,558.97 na ujenzi wa ofisi mkoa wa Geita pamoja na ukarabati wa kituo cha mafuta Wilaya ya Kinondoni umekamilika. Aidha, ujenzi wa ofisi katika mikoa ya Pwani, Songwe, Simiyu, na Dodoma umefikia asilimia 75 na ukarabati wa ofisi za Wakala katika mikoa ya Singida na Arusha umefikia asilimia 85 ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa mwaka 2021/22. Vilevile, mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa ramani na gharama za ujenzi wa ofisi katika mikoa ya Kigoma, Njombe na Arusha amepatikana.

### 3.4.11 Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi

**68.** ***Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka 2022/23, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu kilipanga kupokea na kuchambua miamala ya fedha na kuandaa taarifa fiche kwa hatua stahiki. Hadi Aprili 2023, Kitengo kimepokea taarifa 7,313 za fedha taslimu zenye thamani ya shilingi trilioni 56.65, taarifa 8,784 za usafirishaji fedha kwa njia ya kielektroniki zenye thamani ya shilingi trilioni 222.81 na taarifa 2,457 zinazohusu usafirishaji wa fedha taslimu na hati za malipo kupitia mipakani. Aidha, Kitengo kimechambua miamala shuku 769 na kuandaa taarifa fiche 314 na kuwasilisha kwenye taasisi za utekelezaji wa sheria kwa hatua za uchunguzi. Vilevile, mfumo wa Kitengo umeunganishwa na mfumo wa Mamlaka ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar pamoja na mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ili kusomana na kubadilishana taarifa.

### 3.4.12 Kusimamia masuala ya pamoja ya fedha kati ya Tanzania Bara na Zanzibar

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kufanya tathmini kuhusu fursa ya mapato kwa kampuni zinazosajiliwa upande mmoja wa Muungano na kufanya biashara pande zote. Hadi Aprili 2023, Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imefanikiwa kufanya stadi kuhusu kubainisha majukumu, mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 3.5 Mwenendo wa utekelezaji wa Vipaumbele vya Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**70.** ***Mheshimiwa spika*,** katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipata ridhaa ya Bunge lako Tukufu ya kuendelea kutekeleza majukumu yake, hususan kufanya kaguzi za hesabu za fedha, miradi ya maendeleo, ufanisi katika usimamizi wa miongozo, uwekezaji wa mitaji ya Serikali, mifumo ya TEHAMA na usimamizi wa mazingira kwa Serikali Kuu, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kufuatilia na kutathmini mwenendo wa utekelezaji wa hoja za ukaguzi; kuimarisha maabara ya ukaguzi; na kukusanya maduhuli ya shilingi 900,000,000.

**71.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2023, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kufanya kaguzi zote kama ilivyopangwa na kuwasilisha Ripoti zake bungeni Aprili 6, 2023. Sambamba na Ripoti za Ukaguzi, Ofisi imewasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Ripoti kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa hoja za ukaguzi. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi 421,912,164 sawa na ufanisi wa asilimia 47 ya lengo la mwaka.

## 3.6 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti na Mikakati ya kukabiliana nazo

### 3.6.1 Changamoto

**72.** ***Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya 2022/23, Wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo:

i. Kasi ndogo ya ujengaji na maboresho ya mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali ikilinganishwa na kasi ya mabadiliko ya TEHAMA duniani na hivyo kuhatarisha ufanisi na usalama wa mifumo ya usimamizi wa fedha za umma; na

ii. Kuongezeka kwa bei na gharama za usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, hususan bidhaa za petroli, mafuta ya kula, mbolea kutokana na athari za vita baina ya Urusi na Ukraine, ukame na UVIKO-19 na hivyo kuongeza gharama katika utekelezaji wa mpango na bajeti, hususan miradi ya maendeleo.

### 5.2. Mikakati ya kukabiliana na changamoto

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto zinazoendelea kujitokeza ikiwa ni pamoja na:

i. Kuwekeza katika tafiti na maendeleo pamoja na mafunzo ili kukuza ubunifu na ujuzi katika kukabiliana na kasi ya mabadiliko ya TEHAMA duniani;

ii. Kuongeza kasi katika utekelezaji wa mradi wa kusambaza gesi viwandani, vituo vya gesi kwa matumizi ya magari na majumbani ili kupunguza msukumo wa uagizaji wa bidhaa za petroli kutoka nje ya nchi; na

iii. Kuongeza kasi ya tafiti za mafuta na gesi ili kuvutia uwekezaji wa kimkakati na hivyo kupunguza uhitaji wa uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

## 4.0 Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2023/24

**74. *Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2023/24 yamezingatia miongozo mbalimbali ya kisera ya wizara, kitaifa, kikanda na kimataifa. Miongozo hiyo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24; Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Uzinduzi wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kanuni zake; Mikakati na makubaliano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu; Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; na masuala mtambuka ikijumuisha jinsia, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabia nchi, na UKIMWI.

## 4.1 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Wizara

**75. *Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo:

i. Kutafuta na kukusanya mapato ya shilingi trilioni 40.8 kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali;

ii. Kuhudumia deni la Serikali;

iii. Kufanya tafiti, tathmini na mapitio mbalimbali ya kitaalamu kuhusu mifumo ya usimamizi wa mipango, uchumi na bajeti ya Serikali;

iv. Kujenga, kuboresha, kufungamanisha na kuhuisha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali;

v. Kujenga uwezo wa watumishi kuhusu usimamizi wa masuala ya sera, uchumi, mipango na fedha;

vi. Kuboresha miundombinu ya ofisi za Wizara na taasisi zake pamoja na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;

vii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo inayotekelezwa na Wizara na Serikali kwa jumla; na

viii. Kukamilisha maboresho ya Sheria ya Msajili wa Hazina.

### 4.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Fungu 45-Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**76. *Mheshimiwa Spika*,** vipaumbele vya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni pamoja na: kufanya ukaguzi wa rasilimali za umma kwa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma; kufanya kaguzi za kiufundi, ufanisi, maalum, kiuchunguzi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA; kuimarisha matumizi ya TEHAMA ndani ya Ofisi; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Ukaguzi mikoani.

### 4.3 Vipaumbele vya Taasisi

**77. *Mheshimiwa Spika*,** kama nilivyoeleza awali, baadhi ya majukumu ya Wizara yanatekeleza kupitia taasisi za elimu, bodi za kitaalamu na kitaaluma, usimamizi na udhibiti wa masuala ya fedha, kodi, bima, ununuzi na ugavi, michezo ya kubahatisha, uwekezaji na uwezeshaji pamoja na takwimu.

### 4.3.1 Taasisi za Elimu

**78. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Fedha na Mipango inasimamia jumla ya taasisi za elimu tano (5) ambazo ni Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Uhasibu Arusha, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika. Kwa mwaka 2023/24, vyuo vyote vinatarajia kudahili jumla ya wanafunzi 77,432, ikijumuisha ngazi ya cheti 14,108, stashahada 18,744, shahada 41,483 na uzamili 397.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kimepanga kukamilisha ujenzi wa Kampasi ya Geita, kuanza ujenzi wa awamu ya pili wa Kampasi ya Simiyu kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu kwa Ajili ya Mageuzi ya Kiuchumi na kuendelea na ujenzi wa jengo la taaluma likijumuisha ofisi zenye uwezo wa kuhudumia wahadhiri 40 na madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,520 kwa wakati mmoja katika kampasi ya Mwanza.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Chuo cha Uhasibu Arusha kinatarajia kuendeleza watumishi 45 katika ngazi ya Shahada, Uzamili na Uzamivu ndani na nje ya nchi, kupitia mitaala 10 pamoja na kuandaa mitaala mipya miwili (2), kufungua kampasi mpya ya Songea mkoani Ruvuma, kuanza ujenzi katika kampasi ya Dodoma, kufanya tafiti mbili (2) na kutoa ushauri wa kitaaluma, kuanza ujenzi wa kituo cha TEHAMA katika kampasi ya Arusha na kuanza ujenzi wa jengo la taaluma na maktaba katika kampasi ya Songea.

**81.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2023/24, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kimepanga kukamilisha ujenzi wa bweni la wanafunzi na ukumbi wa mihadhara na kuanza ujenzi wa jengo la utawala katika kampasi ya Dodoma, kuanza ujenzi wa kituo cha mafunzo katika eneo la Nala Dodoma, kukamilisha ujenzi wa bweni, maktaba na kuanza ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Kituo cha Mafunzo - Mwanza. Aidha, chuo kinatarajia kufanya tafiti 10 na kutoa huduma za ushauri elekezi kwa kuzingatia mahitaji ya wadau.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Taasisi ya Uhasibu Tanzania itaendelea na ujenzi wa jengo moja (1) linalojumuisha ukumbi wa mihadhara, maabara ya kompyuta na maktaba katika Kampasi ya Mbeya, jengo la taaluma Misungwi - Mwanza, vyumba vya madarasa manne (4), maktaba, maabara ya kompyuta na nyumba ya watumishi na hosteli mbili (2) za wanafunzi wa kike na wa kiume kampasi ya Mtwara, jengo la taaluma katika kampasi ya Kigoma na kuanza ujenzi wa jengo la taaluma katika kampasi ya Zanzibar.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kimepanga kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala, kuendeleza wahadhiri 28 na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 20.

**4.3.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu inatarajia kusajili wahasibu 1,350 katika ngazi mbalimbali, kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma, kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi 75, kufanya ukaguzi wa ubora wa kampuni 65 za ukaguzi, kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 12,500 na kutoa mafunzo ya diploma ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha serikalini kwa wahitimu 350. Aidha, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi inatarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi, kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 6,500 na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000.

**4.3.3 Taasisi za Usimamizi wa Masuala ya Kodi**

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajia kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 26.7, kuendelea kuimarisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato, kuwajengea uwezo wafanyakazi, kutoa elimu ya kodi na kuendelea kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato. Aidha, Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Ofisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi zinatarajia kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri, malalamiko na taarifa za kodi kutoka kwa walipakodi na wadau wa kodi. Vilevile, Ofisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zinazotolewa na ofisi hiyo.

**4.3.4 Bodi ya Michezo ya kubahatisha**

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha inatarajia kutoa leseni 11,880 kwa waendesha michezo ya kubahatisha, ambapo 2,273 ni leseni mpya na 9,607 ni

leseni zitakazohuishwa, kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 101 na kusimamia uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa.

### 4.3.5 Taasisi za Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

**87.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2023/24, Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana imepanga kuanzisha bidhaa mpya za masoko ya mitaji, kufanya mapitio ya kanuni na miongozo ya utoaji wa bidhaa katika masoko ya mitaji na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji na bidhaa. Aidha, Baraza la Rufaa za Masoko ya Mitaji linatarajia kuanza kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu migogoro ya masoko ya mitaji. Vilevile, Soko la Bidhaa Tanzania linatarajia kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi Jijini Dar es salaam pamoja na kuendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa soko wa kielektroniki ili kuongeza idadi ya bidhaa zinazouzwa na kununuliwa kupitia mfumo huo.

### 4.3.6 Taasisi za Benki

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24**,** Benki Kuu ya Tanzania imepanga kukuza wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kwa kiwango kisichopungua asilimia 10 ili kuendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi, kuboresha mazingira ya kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kudhibiti na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu pamoja na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2023, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 45.1 kukuza faida ya benki kabla ya kodi ya shilingi bilioni 18.5, kutoa mikopo ya shilingi bilioni 336.7, kukuza mali za benki ili kufikia shilingi bilioni 562.7 na kufuatilia urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wateja shilingi bilioni 62.

**90.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2023, Benki ya Maendeleo ya TIB imepanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 51 kwa miradi ya maendeleo kwenye sekta za maji, nishati na uongezaji thamani mazao ya kilimo, kukusanya shilingi bilioni 39.6 za marejesho ya mikopo kutoka kwa wateja, kukusanya shilingi bilioni 57 za marejesho ya mikopo iliyoshindikana na kuondolewa kwenye mizania ya benki.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023, Benki ya Biashara Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 184.2, kukuza faida ya benki kabla ya kodi ya shilingi bilioni 12.4, kutoa mikopo ya shilingi bilioni 904, kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,121, kukuza mali za benki ili kufikia shilingi bilioni 1,446, kukuza mtaji kufikia shilingi bilioni 123.8 na kuunda mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mikopo inayotolewa na benki.

### 4.3.7 Taasisi za Bima

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inatarajia kufanya uchambuzi wa mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 32, kufanya ukaguzi wa wadau wa bima, kuandaa mwongozo wa bima za kilimo, kuhamasisha kampuni za bima kuandaa bidhaa za sekta ya kilimo pamoja na kupokea na kushughulikia malalamiko ya wateja wa bima. Aidha, Shirika la Taifa la Bima linatarajia kukamilisha taratibu za kupata uthibitisho wa cheti cha ubora cha utoaji huduma kwa wateja (ISO 9001 2015), kuongeza wateja wapya 116 wa bidhaa za taasisi na kubuni bidhaa tatu (3) mpya zitakazokidhi mahitaji ya soko.

### 4.3.8 Taasisi za Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS inatarajia kuongeza rasilimali za mifuko kwa kiwango cha asilimia 15, kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5 na kuhamasisha Taasisi za Serikali, Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS kujiunga na mifuko ya UTT AMIS. Aidha, Mfuko wa SELF unatarajia kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya

shillingi bilioni 44.8 kwa wajasiriamali 38,000, kufuatilia urejeshaji wa mikopo usipungue asilimia 95 na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa au wanufaika 5,500.

### 4.3.9 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inatarajia kusambaza matokeo ya sensa ya watu na makazi, kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu za sensa na kuendelea kuandaa taarifa za sensa za kisekta kulingana na ratiba ya kazi zinazotakiwa kufanyika baada ya zoezi la sensa kukamilika. Aidha, ofisi inatarajia kufanya tafiti za kitaalamu kuhusu watu wenye uwezo wa kufanya kazi, mapato na matumizi ya kaya binafsi, ajira, mapato na ustawi wa watoto katika jamii.

### 4.3.10 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma inatarajia kuendelea na ujenzi wa ofisi za Makao Makuu Jijini Dodoma, ujenzi wa mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao awamu ya pili, kutoa mafunzo kwa watumishi 2,000 kutoka katika taasisi nunuzi 1,000 na wazabuni 5,000 kuhusu mfumo mpya wa ununuzi wa umma kwa njia ya kielektroniki na Sheria ya Ununuzi wa Umma, kufanya kaguzi ya thamani ya fedha katika taasisi nunuzi 85 na kaguzi ya ukidhi wa sheria kwa taasisi nunuzi 300 na kufanya mapitio ya nyaraka zote sanifu za zabuni.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini unatarajia kuanza ujenzi wa ofisi ya mkoa wa Kigoma, ofisi na kituo cha mafuta katika mikoa ya Njombe na Arusha pamoja na Wilaya ya Kahama, Korogwe na Masasi. Aidha, Wakala umepanga kuboresha na kuhuisha mfumo wa GIMIS ili kuwezesha matumizi ya kadi katika huduma za ununuzi wa mafuta na kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini uwezekano na mahitaji ya kuunganisha mfumo wa GIMIS na pampu, pamoja na tanki za mafuta. Vilevile, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni imepanga kutoa mafunzo kwa wajumbe, wafanyakazi wa mamlaka, wazabuni na taasisi nunuzi kuhusu utumiaji wa

mfumo wa kielektroniki wa kusajili na kusimamia rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma.

### 4.4 Makadirio ya Matumizi kwa Mafungu ya Wizara pamoja na Fungu 45-Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2023/24.

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2023/24, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba ridhaa ya Bunge lako Tukufu ya kutumia jumla ya shilingi trilioni 15.94 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu yake tisa (9) ya kibajeti. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 15.38 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 564.22 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi bilioni 97.13 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 87.72 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 9.41 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu la Wizara na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.1.**

**Jedwali Na.1: Mchanganuo wa Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2023/24**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA | | | MATUMIZI YA MAENDELEO | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA | NDANI | NJE | JUMLA YA FEDHA ZA MAENDELEO | |
| 1 | Deni la Serikali | - | 10,480,130,968,000 | 10,480,130,968,000 | - | - | - | 10,480,130,968,000 |
| 6 | Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 1,948,234,000 | 7,618,770,000 | 9,567,004,000 | 360,000,000 | - | 360,000,000 | 9,927,004,000 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 5,229,041,000 | 37,591,275,000 | 42,820,316,000 | 940,000,000 | - | 940,000,000 | 43,760,316,000 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 813,300,000 | 2,650,549,000 | 3,463,849,000 | - | - | - | 3,463,849,000 |
| 13 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | - | 3,861,365,000 | 3,861,365,000 | - | 455,000,000 | 455,000,000 | 4,316,365,000 |
| 21 | Hazina | 1,610,820,134,000 | 745,547,085,000 | 2,356,367,219,000 | 464,263,182,000 | 33,493,393,000 | 497,756,575,000 | 2,854,123,794,000 |
| 22 | Huduma Nyinginezo | 13,065,211,000 | 2,301,774,127,000 | 2,314,839,338,000 | - | - | - | 2,314,839,338,000 |
| 23 | Idara ya | 7,157,764,000 | 51,029,321,000 | | 1,880,000,000 | - | 1,880,000,000 | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mhasibu Mkuu wa Serikali | | | 58,187,085,000 | | | | 60,067,085,000 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 54,120,209,000 | 52,703,766,000.00 | 106,823,975,000 | 22,758,347,000 | 40,075,572,000 | 62,833,919,000 | 169,657,894,000 |
| | **JUMLA YA MAFUNGU YA WIZARA** | **1,693,153,893,000** | **13,682,907,226,000** | **15,376,061,119,000** | **490,201,529,000** | **74,023,965,000** | **564,225,494,000** | **15,940,286,613,000** |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 16,891,720,000 | 70,830,676,000 | 87,722,396,000 | 8,828,000,000 | 583,878,000 | 9,411,878,000 | 97,134,274,000 |
| | **JUMLA YA MAFUNGU YOTE** | | | | | | | **16,037,420,887,000** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

## 5.0 HITIMISHO.

**98.** ***Mheshimiwa Spika***, kabla sijahitimisha hoja yangu, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushauri na ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru watendaji wakuu wa wizara na taasisi zake wakiongozwa na Dkt. Natu E. Mwamba, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bi. Jenifa C. Omolo na Bw. Lawrence N. Mafuru kwa ushauri na usimamizi madhubuti wa majukumu ya wizara na taasisi zake. Vilevile, nawashukuru wakuu wa idara, vitengo na wafanyakazi wote wa wizara na taasisi zake kwa utekelezaji mzuri wa mikakati ya maendeleo, ushauri pamoja na ushirikiano wao mahiri katika kufanikisha majukumu yangu ya kila siku. Asanteni sana na *Kazi Iendelee*.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali inaendelea na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Zoezi hili ni muhimu kwa nchi ili kupata mwongozo thabiti wa kisera utakaosaidia katika uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo kwa Taifa letu katika kipindi cha miaka 25 ijayo baada ya Dira ya sasa kufikia ukomo mwaka 2025. Hivyo, napenda kutoa wito kwa waheshimiwa wabunge kuhamasisha wapiga kura wetu na watanzania wote kwa ujumla, kujitokeza kwa wingi kutoa maoni yao kwa timu zitakazokuwa zinakusanya maoni katika maeneo yao.

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii ndani ya Bunge lako Tukufu pamoja na waheshimiwa wabunge wote na umma wa watanzania kwa ujumla kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *www.mof.go.tz*.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa na kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2023 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi. Kwa mujibu wa kifungu cha 118(1) pamoja na kifungu cha 118(9) cha Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu 9 ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Bajeti imepewa jukumu la kuisimamia Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizopo chini yake Kwa mujibu wa kifungu cha 9(a) cha Nyongeza ya 8 cha Kanuni za Kudumu za Bunge. Vilevile, kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 kinaipa Kamati ya Bunge ya Bajeti jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipitia na kuchambua Taarifa za Fedha na Mipango zilizojumuisha mafungu 9 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kwa kuwa, ni sharti la Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mafungu hayo ni kama ifuatavyo, naomba nisiyataje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo:-

(i) Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, Mafungu yaliyo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(ii) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango Pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24;

(iii) Maoni na Mapendekezo ya Ujumla ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23. Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara Hadi Kufikia Tarahe 30 Aprili, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya mafungu yote ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo kwa ujumla mafungu tisa ya Wizara ya Fedha na Mipango yaliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 15.1 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2023 shilingi trilioni 11.9 zilipokelewa, sawa na asilimia 78.9. Jumla ya matumizi ya kawaida ni shilingi trilioni 13.9 sawa na asilimia 91.3 ya fedha zote. Ambapo hadi kufikia Aprili, 2023 fedha zilizopokelewa ni shilingi trilioni 10.9 sawa na asilimia 79. Kati ya matumizi ya kawaida, mishahara ni shilingi trilioni 1 sawa na asilimia 6.7 ya fedha zote. Hadi kufikia Aprili 30, 2023 fedha zilizopokelewa ni shilingi bilioni 438.9 sawa na asilimia 43.2. Na matumizi mengineyo ni shilingi trilioni 12.8 sawa na asilimia 24 ya bajeti yote. Hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya shilingi trilioni 10.5 zilipokelewa, sawa na asilimia 93. Aidha, kati ya shilingi trilioni 13.9

za matumizi ya kawaida, malipo ya Deni la Serikali yalikuwa ni shilingi trilioni 9.1 sawa na asilimia 59.9 ya bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo zilitengwa shilingi trilioni 1.3 ambazo ni sawa na asilimia 8.7 ya bajeti ya mafungu yote. Fedha hizo, shilingi trilioni 1.3 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 36.5 ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 jumla ya fedha za maendeleo zilizotolewa ni shilingi trilioni 1.1 sawa na asilimia 85.1. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa ni shilingi trilioni 1.1 sawa na asilimia 87.4 na fedha za nje ni shilingi bilioni 2.1 sawa na asilimia 57.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida ya Wizara ya Fedha na Mipango ni makubwa kuliko matumizi ya maendeleo kutokana na matumizi hayo kujumuisha malipo ya Deni la Serikali, michango ya Mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na malipo kwa ajili ya Wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Mafungu. Fungu Namba 01 – Deni la Serikali. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Fungu Namba 01 liliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 9.1 kwa ajili ya kugharamia Deni la Serikali. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 4. ni kwa ajili ya malipo ya Deni la Nje na shilingi trilioni 5.1 ni kwa ajili ya malipo ya Deni la Ndani na shilingi bilioni 6.7 ni kwa ajili ya kuhudumia deni. Kiasi cha shilingi milioni 280 ni kwa ajili ya gharama za matangazo ya minada ya Hatifungani za Serikali. Hadi kufikia Aprili 30, 2023 fungu hili lilipokea kiasi cha shilingi trilioni 7.5 sawa na asilimia 82 ya bajeti iliyotengwa. Muhtasari wa mchanganuo wa fedha zilizotolewa na zilizotumika umeainishwa katika Jedwali Namba 1, ukurasa wa 5 na uchambuzi wa kina katika Jedwali Namba 3, Kiambatisho A.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 06 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali. Kamati inaipongeza Serikali kuanzisha fungu maalumu kwa ajili ya ofisi hii. Mwaka 2022/2023, Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 7.9. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 1.9 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 5.2 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi milioni 760 ni fedha za Maendeleo. Aidha, kati ya fedha hizo za maendeleo shilingi milioni 360 ni fedha za ndani na shilingi

milioni 400 ni fedha za nje. Muhtasari wa mchanganuo wa fedha zilizotolewa na zilizotumika umeainishwa katika Jedwali Namba 1, ukurasa wa 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati imefanya uchambuzi wa kina kuhusu fungu hili na kubaini :-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Upungufu wa Rasilimali watu pamoja na vitendea kazi. Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali inakabiliwa na upungufu wa Wakaguzi wa ndani pamoja na vitendea kazi. Idadi ya Wakaguzi wanaohitajika ni 2,409 lakini waliopo ni 1,462. Upungufu huu umeathiri utendaji wa shughuli za ukaguzi na hatimaye kudhoofisha uimarishaji na udhibiti wa mifumo ya ndani.

Pia kuna upungufu wa vitendea kazi, ili kuwezesha idara hii kufanya kazi vizuri magari 175 na tarakilishi mpakato 590 zinahitajika. Jukumu kubwa la Mkaguzi wa Ndani ni kusimamia vihatarishi vinavyoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti na kuwasilisha Taarifa ya namna ya kuepukana na matumizi mabaya ya fedha wakati wa utekelezaji wa bajeti. Hivyo Ofisi hii kukosa wafanyakazi na vitendea kazi inasababisha kuwepo na hoja nyingi za ukaguzi, kuathiri wigo na muda wa ukaguzi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Uwasilishaji wa Taarifa za Mkaguzi wa Ndani. Muundo wa sasa unamtaka Mkaguzi Mkuu wa Ndani kuwasilisha taarifa kwanza kwa Menejimenti ya Wizara, Idara, Wakala ya Serikali za Mitaa na Afisa Masuuli wa Fungu husika ndiye anawajibika kuwasilisha taarifa hiyo kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali. Hatua hii imekuwa na changamoto mbalimbali, moja ya changamoto ni Menejimenti ilifanye mabadiliko Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani kabla ya kuiwasilisha.

Kamati inashauri Serikali kuruhusu Mkaguzi wa Ndani kuwasilisha Taaarifa yake moja kwa moja kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali na baada ya kuikabidhi Maafisa Masuuli wote ambao watakuwa na hoja za kujibu wajibu kwake. Hatua hii itasaida kuleta ufanisi wa uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 07 – Msajili wa Hazina. Katika Mwaka 2022/2023, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 43.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5.1 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 10.3 ni kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi na shilingi bilioni 27 kwa ajili ya matumizi maalum kama vile kulipa madeni ya mashirika na taasisi za umma na kurekebisha mashirika yenye matatizo ya mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina iliongezeka kutoka shilingi bilioni 47.9 hadi kufikia shilingi bilioni 91.8. Fedha hizo ziliongezeka ili kulipa deni la *Exim* Benki na wadai wa *NASACO,* kuimarisha mtaji wa Benki ya Biashara Tanzania *(TCB),* kugharamia malipo ya wafanyakazi wa kiwanda cha Maturubai Morogoro, kulipa mapunjo na malimbikizo ya wastaafu wa *TTCL* na wasimamizi wa Mirathi. Malipo ya fidia kwa wananchi watatu waliopisha maeneo yao kwa ajili ya Kampuni ya Chai ya Kagera na kugharamia malipo ya *M/S Consolidated Investment LTD (CITL)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023, jumla ya shilingi bilioni 78.4 zilipokelewa na kugharamia matumizi ya kawaida na maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa Ofisi ya Msajili na kubaini yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Upungufu wa Rasilimali kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina. Utofauti wa Ofisi hii na Ofisi nyingine za Umma ni kwamba, ofisi hii inasimamia uwekezaji wa umma na inakusanya marejesho ya mitaji ya umma. Hivyo si sawa ofisi hii kutokuwa na watumishi wa kutosha na ubobezi katika taaluma ya uwekezaji, ufuatialiaji na tathmini, sheria na uhasibu. Mathalani, kati ya watumishi 185 wanaohitajika ofisi ina watumishi 145 tu, hivyo kuna tofauti ya watumishi 40. Hali hii inaathiri utendaji wa kazi wa ofisi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, ofisi hii inapata watumishi wa kutosha na wenye ujuzi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Ajira kwa Makampuni na Mashirika ya Umma ya Kibiashara. Makampuni ya

umma yanayojiendesha kibiashara yamekuwa yakiendeshwa na Wakurugenzi watendaji ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais au Mawaziri wa Sekta husika. Utaratibu huu sio mbaya endapo wana sifa na weledi wa kuendesha kampuni hizo. Kamati inapendekeza kwa kampuni za umma ambazo zinajiendesha kibiashara ni vyema Wakurugenzi Watendaji wakapatikana kwa ushindani. Hatua hii italeta ufanisi katika uendeshaji wa kampuni za Serikali ambazo inazimiliki kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 10 – Tume ya Fedha ya Pamoja. Tume ya Fedha ya Pamoja ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 2.9 katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kati ya fedha hizo shilingi bilioni mbili ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi milioni 934 ni kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 fedha zilizopokelewa na kutumika ni shilingi bilioni 2.1 sawa na asilimia 70 na kati ya fedha hizo, shilingi milioni 566.4 sawa na asilimia 61 ni bajeti ya mishahara na shilingi bilioni 1.5 sawa na asilimia 75 ni fedha za Matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kufanyia Kazi Ushauri wa Tume Unaotokana na tafiti Zilizofanywa. Tume ya Pamoja ya Fedha imekwishafanya tafiti kwenye maeneo makuu mawili, moja ni kuhusu Ukusanyaji wa Mapato ya Muungano yanayotokana na Huduma za Mawasiliano ya Simu, Fedha za Bima kwa kampuni, mashirika yaliyosajiliwa upande mmoja wa muungano na kufanya biashara katika pande zote mbili za muungano. Mfano ukusanyaji wa Kodi za Zuio *(Withholding Tax)* inayotokana na mashirika na kampuni zilizosajiliwa upande mmoja wa muungano na kufanya biashara katika pande zote mbili za muungano na uanzishwaji wa akaunti jumuifu ya fedha. Kwa kuwa, tafiti hizi zimekamilika Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi kikamilifu ili kuondoa kero hiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 470 ni fedha za nje kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, fungu hili liliongezewa bajeti kwa njia ya uhamisho, hivyo jumla ya

bajeti kufikia shilingi bilioni 4.02. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 3.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 470 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Fedha Haramu. Kitengo hiki ili kifanye kazi kwa uhuru ni lazima kiwe na mamlaka Inayojitegemea. Hivi sasa watumishi wanaazimwa kutoka Idara mbalimbali za Serikali jambo ambalo si baya kwa ajili ya usalama na usiri, lakini haiondoi uwezekano wa kuwa na mamlaka kwa sababu zipo taasisi na vyombo katika nchi hii vinajulikana lakini watumishi wake hawajulikani. Hivyo ni vyema Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu kikawa ni mamlaka, ili ifanye kazi kwa kujitegemea kama inavyofanyika katika baadhi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhakikisha Kwamba Kitengo Kinakuwa na Rasilimali Watu wa Kutosha na wa Kudumu. Kwa sasa watumishi waliopo katika kitengo hiki ni wa kuazimwa kutoka taasisi na vitengo vya Serikali. Pamoja na hayo kitengo kina uhitaji wa watumishi 58 na kwa sasa watumishi waliopo ni 29 tu ambao kwa mujibu wa majukumu ya kitengo hawatoshelezi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko kwenye Kifungu cha 7(1) na (3) cha Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423, ili kukiwezesha kitengo hiki kuwa na uwezo wa kuajiri watumishi wake na kuwawezesha watumishi hao kuwajibika kwenye kitengo na sio kwenye taasisi walizotoka kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 21 – Hazina. Katika mwaka 2022/2023, fungu liliidhinishiwa shilingi trilioni 3.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 2.1 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.3 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa, shilingi bilioni 7.1 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa idara na vitengo vya Hazina, shilingi bilioni 257 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2023, fungu lilikuwa limepokea jumla ya shilingi trilioni 2.6 sawa na asilimia 77 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 50 …

**NAIBU SPIKA:** Nenda kwenye Maoni, Ushauri.

**MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Baada ya Kamati kuchambua na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu husika kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Utendaji wa Kazi wa Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko ya Kodi. Ofisi hii ilianzishwa kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali za kikodi kutoka kwa wadau. Ofisi ya mpokea malalamiko ya kodi ilianzishwa kwa lengo la kupokea, kuchakata na kutoa mapendekezo kwa Waziri wa Fedha juu ya malalamiko yote yanayohusu Kodi. Ni wazi kwamba, ofisi hii haijaweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, ofisi hii bado haijajulikana kwa wananchi wengi zaidi, ili itimize majukumu yake kama yalivyobainishwa katika Kifungu Na. 28A cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha ofisi hii inatekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kuhakikisha inajulikana na kujitangaza kwa wadau wa kodi wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma na Makampuni Yaliyo Chini ya Msajili wa Hazina. Uwepo wa bodi kwenye mashirika na makampuni ya umma ni jambo la msingi katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na ufanisi katika kazi na utawala bora. Kamati imebaini kwamba, kuna baadhi ya mashirika na kampuni ambazo hazina bodi, hivyo kukosekana kwa utawala bora katika uendeshaji wake. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa mashirika na makampuni ya umma yanakuwa na wajumbe wa bodi ili mashirika hayo yajiendeshe kwa ufanisi na kwa kufuata misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutofautisha Majukumu ya Mamlaka za Udhibiti *(Regulatory Authority)* Katika Ukusanyaji wa

Mapato na Utoaji wa Huduma. Kamati ya Bajeti inatambua umuhimu wa mamlaka mbalimbali za udhibiti ili kuleta ufanisi katika sekta mbalimbali. Hata hivyo uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mamlaka hizi zimegeuka kuwa ni wakusanya faini, ada na tozo kutokana na sekta wanazozisimamia kuliko kutekeleza majukumu yake ya Msingi. Kwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ndio yenye jukumu la kusimamia mapato ni wakati sasa umefika wa kupitia mamlaka zote za udhibiti ili kuangalia uhalali na ulazima wa mamlaka hizo kutoza ada, faini na tozo mbalimbali ili kuziangalia endapo zinafaa na kuendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Misamaha ya Kodi Kwenye Miradi ya Maendeleo. Utaratibu wa misamaha ya kodi unaratibiwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba, kumekuwa na ucheleweshaji wa uwasilishaji wa maombi ya msamaha kutoka Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, basi Kamati inawataka maafisa masuuli wote kuhakikisha kwamba, wanawasilisha maombi ya misamaha ya kodi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa wakati, ili kutokwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuondoa mlundikano wa bidhaa za Serikali Bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali. Mfumo huu hausomani na mifumo mingine ya Serikali, mfano mfumo wa malipo wa *GePG*. Aidha, mfumo huu umekuwa na mapungufu kadhaa kama vile mfumo kushindwa kutambua kiasi, idadi na hali za mali za Serikali zilizopo isipokuwa zile zilizopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, Kamati inashauri kwamba, mfumo huu uboreshwe ili uweze kusomana na mifumo mingine ya Serikali. Na ni wazi kwamba, maboresho ya mfumo huu yataondoa changamoto kwa Idara ya Msimamizi wa Mali za Serikali kutumia gharama kubwa kukagua mali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yako wakati wa utendaji wa kazi wa Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, ambaye ni wewe

hapo, Naibu Spika, kwa kuendelea kusaidia kuliongoza vyema Bunge Tukufu. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ya Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niwashukuru na kuwapongeza Dkt. Natu El-maamry Mwamba kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ndugu Emmanuel Tutuba kwa kuteuliwa kuwa Gavana wa Benki Kuu. Kamati imepata ushirikiano mkubwa katika kipindi hiki cha Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Charles Kichere, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Ndugu Alphayo J. Kidata na wakuu wote wa taasisi na idara na vitengo pamoja na watalaamu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili Bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango yanayojumisha mafungu tisa yaliyo chini yake pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**7 JUNI, 2023**

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 118(1) pamoja na kifungu cha 118(9) cha Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/23 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu 9 ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bunge ya Bajeti imepewa jukumu la kuisimamia Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizopo chini yake Kwa mujibu wa kifungu cha 9(a) cha Nyongeza ya Nane cha Kanuni za Kudumu za Bunge. Vilevile, kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 kinaipa Kamati ya Bunge ya Bajeti jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipitia na kuchambua Taarifa za Wizara ya Fedha na Mipango zilizojumuisha mafungu 9 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kuwa ni sharti la Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na Mafungu hayo ni kama ifuatavyo:-

i. **Fungu 001** – **Deni la Serikali**
ii. **Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali**
iii. **Fungu 007 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**
iv. **Fungu 010 – Tume ya Pamoja ya Fedha**
v. **Fungu 013 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**
vi. **Fungu 021 – Hazina**
vii. **Fungu 022 – Huduma za Mfuko Mkuu**
viii. **Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**
ix. **Fungu 050 – Wizara ya Fedha na Mipango**
x. **Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo: -

i. Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, Mafungu yaliyo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23;

ii. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2023/24;

iii. Maoni na Mapendekezo ya Ujumla ya Kamati.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Namba 1 linaonyesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti kwa mafungu yote 9 yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango hadi kufikia 30 Aprili 2023.

**Jedwali Na. 1 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango Mafungu 9 kwa mwaka 2022/23**

| Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2022/23 | Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2023 | Asilimia ya Bajeti Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| **01. Deni la Serikali** | | | |
| Riba ya deni la Nje | 1,100,802,002,000 | 840,680,732,000.00 | 76 |
| Riba ya deni la ndani | 1,770,159,000,000 | 1,730,603,060,000.00 | 98 |
| Mtaji Deni la nje | 2,916,041,492,000 | 2,169,560,604,000.00 | 74 |
| Mtaji Deni la Ndani | 3,300,000,000,000 | 2,747,331,133,000.00 | 83 |
| Kuhudumia Deni | 6,702,200,000 | 4,332,471,000.00 | 64 |
| Matangazo | 280,000,000.00 | 123,101,000.00 | 68 |
| **Jumla Fungu 01** | **9,093,984,694,000** | **7,492,631,101,000.00** | **82** |
| **06. Idara ya Mhasibu wa Ndani Mkuu wa Serikali** | | | |
| Mishahara | 1,981,784,000.00 | 275,557,400.00 | 13.9 |
| Matumizi Mengineyo | 6,961,845,872.29 | 4,236,602,505.47 | 60.85 |

| Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2022/23 | Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2023 | Asilimia ya Bajeti Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| Maendeleo Ndani | 360,000,000.00 | 355,600,600.00 | 98.78 |
| Maendeleo Nje | 400,000,000.00 | 0 | 0 |
| **Jumla Fungu 06** | **9,703,629,872.29** | **4,867,760,505.47** | **50.16** |
| **07. Msajili wa Hazina** | | | |
| Mishahara | 5,142,226,000.00 | 3,890,966,181.30 | 75.67 |
| M Matumizi ya Ofisi | 10,229,786,000.00 | 6,820,707,018.00 | 66.67 |
| M Matumizi Maalum | 74,813,977,399.92 | 73,774,550,175.03 | 98.61 |
| Maendeleo Ndani | 997,900,000.00 | 991,300,000.00 | 99.34 |
| Maendeleo Nje | 650,000,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| **Jumla Fungu 07** | **91,833,889,399.92** | **85,477,523,374.33** | **93.08** |
| **10 Tume ya Pamoja ya Fedha** | | | |
| Mishahara | 934,163,000.00 | 566,383,345.48 | 61 |
| Matumizi mengineyo | 2,048,142,000.00 | 1,531,374,157.97 | 75 |
| **Jumla Fungu 10** | **2,982,305,000.00** | **2,097,757,503.45** | **70** |
| **013 Kitengo cha udhibiti fedha haramu** | | | |
| Matumizi mengineyo | 3,555,391,000.00 | 2,371,813,387.00 | 66.7 |
| Maendeleo Ndani | - | - | - |
| Maendeleo Nje | 470,000,000.00 | 220,139,708.00 | 46.8 |
| **Jumla Fungu 13** | **4,025,391,000.00** | **2,591,953,095.00** | **64.4** |
| **021 Hazina** | | | |
| Mishahara | 945,178,117,000 | 382,896,816,619.49 | 40.51% |
| Matumizi mengineyo | 1,181,695,401,000 | 1,122,588,952,092.85 | 95% |
| Maendeleo Ndani | 1,257,970,257,000 | 1,108,744,874,192.66 | 88.14 |
| Maendeleo Nje | 29,784,942,000 | 1,584,835,888.00 | 5.32 |
| **Jumla Fungu 21** | **3,414,428,717,000** | **2,615,815,478,793.00** | **77** |
| **022 Huduma ya Mfuko Mkuu** | | | |
| Mishahara | 9,452,132,000.00 | 7,776,460,240.20 | 85.91 |

| Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2022/23 | Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2023 | Asilimia ya Bajeti Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| Matumizi mengineyo | 2,214,379,800,000 | 1,519,305,769,419.20 | 68.61 |
| **Jumla Fungu 22** | **2,223,831,932,000** | **1,527,082,229,659.40** | **68.67** |
| **23.Idara ya Mhasibu Mkuu** | | | |
| Mishahara | 6,361,101,000.00 | 5,447,742,085 | 85.64 |
| Matumizi mengineyo | 39,551,734,000.00 | 31,513,214,395.00 | 79.68 |
| Maendeleo Ndani | 1,880,000,000.00 | 1,357,230,000.00 | 72.19 |
| Maendeleo Nje | 964,792,000.00 | 93,000,000.00 | 9.64 |
| **Jumla Fungu 23** | **48,757,627,000.00** | **38,411,186,480.00** | **78.78** |
| **50.Wizara ya fedha na mipango** | | | |
| Mishahara | 46,285,234,600.00 | 38,102,573,619.24 | 82.32 |
| Matumizi mengineyo | 203,183,454,549.99 | 192,255,155,381.64 | 77.07 |
| Maendeleo Ndani | 29,628,291,333.00 | 16,096,499,625.34 | 54.33 |
| Maendeleo Nje | 4,240,863,000.00 | 210,202,800.00 | 4.96 |
| **Jumla Fungu 50** | **283,337,843,482.99** | **208,561,857,806.98** | **73.61** |
| **JUMLA KUU** | **15,172,886,028,755.20** | **11,977,536,848,217.60** | **78.94** |

***Chanzo**:Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali*

## 2.1. *Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hadi kufikia 30 Aprili 2023*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya mafungu yote ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 ambapo kwa ujumla mafungu tisa (9) ya Wizara ya Fedha na Mipango yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi trilioni 15.1** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Hadi kufikia 30 Aprili 2023 **shilingi trilioni 11.98** zilipokelewa sawa na **asilimia 78.94**. Jumla ya matumizi ya kawaida ni **shilingi trilioni 13.85** sawa na **asilimia 91.25** ya fedha zote, ambapo hadi kufikia 30 Aprili 2023 fedha zilizopokelewa ni **shilingi trilioni 10.89** sawa na **asilimia 79**. Kati ya matumizi ya kawaida, mishahara ni **shilingi trilioni 1. 02** sawa na **asilimia 6.7** ya fedha zote. Hadi kufikia Aprili 30, 2023 fedha zilizopokelewa ni **shilingi bilioni 438.96** sawa na **asilimia 43.23**, na matumizi

mengineyo ni **shilingi trilioni 12.84** sawa na **asilimia 24.63** ya bajeti yote, na hadi kufikia April 2023 jumla ya **shilingi trilioni 10.45** zilipokelewa sawa na **asilimia 93**. Aidha, kati ya **Shilingi trilioni 13.85** za matumizi ya kawaida, malipo ya Deni la Serikali yalikuwa ni **Shilingi trilioni 9.1** sawa na **asilimia 59.93** ya bajeti yote ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo zilitengwa jumla ya **shilingi trilioni 1.333** ambazo ni sawa na **asilimia 8.7** ya bajeti ya mafungu yote. Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 1.29** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 36.5** ni fedha za nje. Hadi kufikia 30 Aprili 2023, jumla ya fedha za maendeleo zilizotolewa ni **shilingi trilioni 1.13** sawa na **asilimia 85.11**. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa **shilingi trilioni 1.127** sawa na **asilimia 87.35** na fedha za nje ni **shilingi bilioni 2.11** sawa na **asilimia 57.74.**

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya kawaida ya Wizara ya Fedha na Mipango ni makubwa kuliko matumizi ya maendeleo kutokana na matumizi hayo kujumuisha malipo ya Deni la Serikali, michango ya Mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na malipo kwa ajili ya Wastaafu.

## 2.2. *UCHAMBUZI WA MAFUNGU*

### 2.2.1. Fungu 01 – Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2022/23, Fungu 01 liliidhinishiwa jumla ya **shilingi trilioni 9.09** kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali. Kati ya fedha hizo, **shilingi trilioni 4.02** ni kwa ajili ya malipo ya Deni la nje, **shilingi trilioni 5.07** kwa ajili ya malipo ya Deni la ndani, **shilingi bilioni 6.7** ni kwa ajili ya kuhudumia deni, na kiasi cha **shilingi milioni 280** ni kwa ajili ya gharama za matangazo ya minada ya Hatifungani za Serikali. Hadi kufikia 30 Aprili, 2023 Fungu hili lilipokea kiasi cha **shilingi trilioni 7.49** sawa na **asilimia 82** ya bajeti iliyotengwa. Muhtasari wa mchanganuo wa fedha zilizotolewa na zilizotumika umeainishwa katika Jedwali Na. 1 (ukurasa wa 5) na uchambuzi wa kina katika Jedwali Na. 3, Kiambatisho A.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejiiridhisha kuwa deni la Serikali ni himilivu kwa vigezo vyote vya kimataifa.hata hivyo, Kamati

inaendelea kuishauri Serikali ihakikishe kuwa mikopo yote inayokopwa na Serikali inaelekezwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2023/24 malipo ya deni la Serikali ni **asilimia 31.03** .Hivyo ni muhimu wakati wote mikopo kuelekezwa kwenye miradi inayosaidia kukuza uchumi na kuongeza mapato ya Serikali.

**2.2.2. Fungu 06 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Fungu maalumu kwa ajili ya Ofisi hii. Katika Mwaka 2022/23, Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 7.89**. Kati ya kiasi hicho **shilingi bilioni 1.9** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi bilioni 5.15** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na **shilingi milioni 760** ni fedha za Maendeleo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo **shilingi milioni 360** ni fedha za ndani na **shilingi milioni 400** ni fedha za nje. Aidha, Fungu liliongezewa bajeti kwa njia ya uhamisho hivyo jumla ya bajeti kufikia **shilingi bilioni 9.70**. Hadi 30 Aprili 2023 Fungu hili lilipokea kiasi cha **shilingi bilioni 4.87** sawa na **asilimia 50.16** ya bajeti baada ya uhamisho. Kati ya fedha iliyopokelewa **shilingi milioni 275** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi bilioni 4.24** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi milioni 355** kwa ajili ya fedha za maendeleo. Muhtasari wa mchanganuo wa fedha zilizotolewa na zilizotumika umeainishwa katika Jedwali Na. 1 (ukurasa wa 5) na uchambuzi wa kina katika Jedwali Na. 2, Kiambatisho A.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa Kina kuhusu fungu hili na kubaini masuala yafuatayo:-

**a) Upungufu wa Rasilimali watu pamoja na vitendea kazi**

**Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mkaguzi wa ndani Mkuu wa Serikali inakabiliwa na upungufu wa Wakaguzi wa ndani pamoja na vitendea kazi. Idadi ya Wakaguzi wanaohitajika ni 2,409 lakini waliopo ni 1,462. Upungufu huu unaathiri utendaji wa shughuli za ukaguzi na hatimaye kudhoofisha uimarishaji wa udhibiti wa mifumo ya ndani. Pia kuna upungufu wa vitendea kazi, ili kuwezesha idara hii kufanya kazi vizuri magari 175 na Tarakilishi Mpakato 590 zinahitajika. Jukumu kubwa la Mkaguzi wa Ndani ni

kusimamia vihatarishi vinavyoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Bajeti na kuwasilisha Taarifa ya namna ya kuepukana na matumizi mabaya ya fedha wakati wa utekelezaji wa Bajeti. Hivyo Ofisi hii kukosa wafanyakazi na vitendea kazi inasababisha kuwepo na hoja nyingi za Ukaguzi, kuathiri wigo na muda wa ukaguzi.

**b) Muundo wa Uwasilishaji wa Taarifa za Mkaguzi wa Ndani**

**Mheshimiwa Spika,** Muundo wa sasa unamtaka Mkaguzi Mkuu wa ndani kuwasilisha Taarifa kwanza kwa Menejimenti ya Wizara, Idara, Wakala au Serikali za Mitaa na Afisa Masuuli wa Fungu husika ndiye anawajibika kuwasilisha Taarifa hiyo kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali. Hatua hii imekuwa na changamoto mbalimbali moja ya changamoto ni Menejimenti kuifanyia mabadiliko Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa ndani kabla ya kuiwasilisha. Kamati inashauri Serikali kuruhusu Mkaguzi wa ndani kuwasilisha Taaarifa yake moja kwa moja kwa Mkaguzi Mkuu wa ndani wa Serikali na baada ya kuikabidhi Maafisa Masuuli wote ambao watakuwa na hoja za kujibu wajibu kwake. Hatua hii itasaida kuleta ufanisi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma.

**2.2.3. Fungu 07 – Msajili wa Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 43.962** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 5.142** zilitengwa kwa ajili ya mishahara, **shilingi bilioni 10.229** kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi na **shilingi bilioni 27** kwa ajili ya matumizi maalumu kama vile kulipa madeni ya Mashirika na Taasisi za Umma na kurekebisha Mashirika yenye matatizo ya mitaji. Kwa upande wa fedha za matumizi ya maendeleo fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 1.647** kati ya fedha hizo **shilingi milioni 997** ni fedha za ndani na **shilingi milioni 650** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina iliongezeka kutoka **shilingi bilioni 47.872** hadi kufikia **shilingi bilioni 91.834**. Fedha hizo ziliongezeka ili kulipa deni la Exim Benki na Wadai wa

NASACO; kuimarisha mtaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB); kugharamia malipo ya wafanyakazi wa kiwanda cha Maturubai Morogoro; kulipa mapunjo na malimbikizo ya Wastaafu wa TTCL na wasimamizi wa Mirathi; malipo ya fidia kwa Wananchi watatu waliopisha maeneo yao kwa ajili ya Kampuni ya chai Kagera na kugharamia malipo ya M/S Consolidated Investmnet LTD (CITL).

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2023, jumla ya **shilingi bilioni 78.410** zilipokelewa kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida na maendeleo, sawa na asilimia **85.38** ya bajeti ya Fungu. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 3.89** zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia **75.67** ya bajeti ya mishahara, **shilingi bilioni 5.236** kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi sawa na **asilimia 51.18** ya bajeti ya matumizi hayo na **shilingi bilioni 68.687** kwa matumizi maalumu sawa na **asilimia 93.10** ya bajeti ya matumizi maalumu. Aidha, **shilingi milioni 596.582** zimetumika kugharamia matumizi ya maendeleo sawa na **asilimia 59.78** ya bajeti ya maendeleo. Muhtasari wa mchanganuo wa fedha zilizotolewa na zilizotumika umeainishwa katika Jedwali Na. 1 (ukurasa wa 5) na uchambuzi wa kina katika Jedwali Na. 3, Kiambatisho A.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa Utendaji wa Ofisi ya Msajili na kubaini masuala yafuatayo:-

**a) Upungufu wa Rasilimali kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina.**

**Mheshimiwa Spika,** Utofauti wa Ofisi hii na Ofisi nyingine za Umma ni kwamba Ofisi hii inasimamia uwekezaji wa Umma na inakusanya marejesho ya mitaji ya umma. Hivyo si sawa Ofisi hii kutokuwa na watumishi wa Kutosha na ubobezi katika taaluma za uwekezaji, ufuatialiaji na tathmini, sheria na uhasibu. Mathalani kati ya watumishi 185 Wanaohitajika Ofisi ina watumishi 145 tu hivyo kunatofauti ya watumishi 40 . Hali hii inaathiri utendaji kazi wa Ofisi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Ofisi hii inapata watumishi wa Kutosha wenye ujuzi unaohitajika ili itekeleza majukumu yake kikamilifu na kufanya Taasisi na Makampuni ya Serikali kuwa shindani.

**b) Mfumo wa ajira kwa Makampuni na Mashirika ya Umma ya Kibiashara**

**Mheshimiwa Spika,** Makampuni ya umma yanayojiendesha kibiashara yamekuwa yakiendeshwa na Wakurugenzi watendaji ambao ama wameteuliwa na Rais au na Mawaziri wa Sekta husika. Utaratibu huu sio mbaya endapo wana sifa na weledi wa kuendesha Kampuni hizo. Kamati inapendekeza kwa Kampuni za umma ambazo zinajiendesha kibiashara ni vyema Wakurugenzi Watendaji wakapatikana kwa ushindani. Hatua hii italeta ufanisi katika uendeshaji wa kampuni za Serikali ambazo inazimiliki kwa asilimia 100**.**

**2.2.4.Fungu 10: Tume ya Fedha ya Pamoja**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Fedha ya Pamoja ilitengewa jumla ya **Shilingi bilioni 2.98** katika mwaka 2022/23 kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 2.05** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na **Shilingi milioni 934** kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 fedha zilizopokelewa na kutumika ni **Shilingi bilioni 2.097** sawa na asilimia **70** ya Bajeti. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 566.38** sawa na asilimia **61** ni bajeti ya mishahara na **Shilingi bilioni 1.53** sawa na asilimia **75** ni fedha za Matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Bajeti ya Fungu hili Kamati ina maoni na ushauri ufuatao;

**a) Serikali kufanyia kazi ushauri wa Tume unaotokana na Tafiti zilizofanywa.**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya pamoja ya Fedha imekwisha fanya tafiti kwenye maeneo makuu mawili moja ni kuhusu Ukusanyaji wa Mapato ya Muungano yanayotokana na Huduma za Mawasiliano ya Simu, Fedha na Bima kwa kampuni/mashirika yaliyosajiliwa upande mmoja wa Muungano na kufanya Biashara katika Pande Zote Mbili za Muungano mfano ukusanyaji wa Kodi ya Zuio (Withholding Tax) inayotokana na Mashirika na Kampuni zilizosajiliwa upande mmoja wa Muungano na kufanya biashara katika pande zote mbili za Muungano, na uanzishwaji wa Akaunti jumuifu ya fedha. Kwakuwa tafiti hizi zimekamilika Kamati

inaishauri Serikali kuzifanyia kazi kikamilifu ili kuondoa kero hiyo ya Muungano.

**2.2.5.Fungu 13: Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/23, Fungu hili liliidhinishiwa kutumia kiasi cha **shilingi bilioni 3.385** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 2.916** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi milioni 470** ni fedha za nje kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Fungu hili liliongezewa bajeti kwa njia ya uhamisho, hivyo jumla ya bajeti kufikia shilingi **bilioni 4.025.** Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 3.555** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi milioni 470** fedha za nje kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia 30 Aprili, 2023 Fungu hili lilikuwa limetumia kiasi cha **shilingi bilioni 2.592** ambazo shilingi **bilioni 2.372** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi milioni 220.14** ni fedha za nje kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa kina wa fedha zilizotumika kwa kila kifungu umeoneshwa katika jedwali namba 1. Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo kwa fungu hili;

**a) Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Fedha haramu**

**Mheshimiwa Spika,** ili Kitengo hiki kifanye kazi kwa uhuru ni lazima kiwe Mamlaka Inayojitegemea. Hivi sasa watumishi wanaazimwa kutoka Idara mbalimbali za Serikali jambo ambalo si baya kwa ajili ya usalama na usiri lakini haiondoi uwezekano wa kuwa na Mamlaka kwa sababu zipo Taasisi na vyombo katika nchi hii vinajulikana lakini watumishi wake hawajulikani. Hivyo ni vyema Kitengo cha Kudhibiti Fedha haramu kikawa ni Mamlaka ili ifanye kazi kwa kujitegemea kama inavyofanyika katika baadhi ya nchi.

**b) Kuhakikisha kwamba Kitengo kinakuwa na rasilimali watu wa kutosha na wa kudumu**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa watumishi waliopo katika kitengo hiki ni wa kuazimwa kutoka Taasisi na Vitengo vya Serikali. Pamoja na hayo kitengo kina uhitaji wa watumishi 58 na kwa sasa Watumishi waliopo ni 29 tu ambao kwa mujibu wa majukumu ya Kitengo hawatoshelezi. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko

kwenye Kifungu cha 7 (1) na (3) cha Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423 ili kukiwezesha kitengo hiki kuwa na uwezo wa kuajiri watumishi wake na kuwawezesha Watumishi hao kuwajibika kwa Kitengo na sio kwenye Taasisi walizotoka kama ilivyo hivi sasa.

**2.2.6.Fungu 21: Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2022/23, Fungu hili liliidhinishiwa **shilingi trilioni 3.415** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 2.127** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 1.288** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa, **shilingi bilioni 7.136** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa idara na vitengo vya Hazina, **shilingi bilioni 257.051** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Taasisi zilizo chini ya Fungu, **shilingi bilioni 680.991** ni marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma, **shilingi trilioni 1.182** ni matumizi mengineyo kwa ajili ya idara, vitengo na Taasisi zilizo chini ya Fungu hili. Aidha, kati ya fedha za matumizi mengineyo, **shilingi bilioni 990.168** ni kwa ajili ya matumizi maalumu ya Kitaifa na mahitaji ya dharura yanayojitokeza katika mafungu mbalimbali wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Kati ya **shilingi trilioni 1.288** za bajeti ya matumizi ya maendeleo, **shilingi trilioni 1.258** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 29.785** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi 30 Aprili 2023, Fungu hili limepokea jumla ya **shilingi trilioni 2.616,** sawa na **asilimia 77** ya bajeti iliyoidhinishwa**.** Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 5.092** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa idara na vitengo vya Hazina, **shilingi bilioni 210.331** mishahara ya Taasisi, **shilingi bilioni 167.473** marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa Umma, **shilingi bilioni 35.206** matumizi mengineyo kwa Idara na vitengo vya Hazina, **shilingi bilioni 139.703** matumizi mengineyo kwa Taasisi, **shilingi bilioni 947.680** matumizi maalum ya Kitaifa, na fedha za maendeleo **shilingi trilioni 1.110.** Kati ya fedha za maendeleo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **shilingi trilioni 1.109** zikijumuisha **shilingi bilioni 796.950** matumizi maalum ya kitaifa na fedha za nje **shilingi bilioni 1.585.** Muhtasari wa mchanganuo wa fedha zilizotolewa na zilizotumika umeainishwa katika Jedwali Na. 1

(ukurasa wa 5) na uchambuzi wa kina katika Jedwali Na. 4, Kiambatisho A

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi Kamati ilibaini kwamba bado Serikali haijaweza kuanzisha Mfuko wa Dharura (Contigency Fund). Utakumbuka kwamba imekuwa ni rai ya Kamati kwa Serikali kuanzisha Mfuko wa Dharura kama kifungu cha 35 hadi 38 cha Sheria ya Bajeti sura ya 439 kinavyoelekeza. Pamoja na kuwa Mfuko huo haujaanzishwa rasmi Serikali imekuwa ikitenga fedha za dharura kwa ajili ya maafa au matukio mbalimbali takribani **shilingi bilioni 100** kila mwaka kupitia Fungu 21. Hivyo, kuna haja ya Bunge lako Tukufu kupata msimamo wa Serikali juu ya uanzishwaji wa Mfuko huu ambao upo kisheria. Hata hivyo, Kamati inaona umuhimu wa Mfuko huu na hivyo inaishauri Serikali badala ya kutenga fedha za dharura kupitia Fungu 21, fedha hizo zitengwe katika Mfuko Mkuu na kulegeza masharti ya kisheria juu ya matumizi ya Mfuko ili kuruhusu Mfuko huu kuanzishwa.

**2.2.7.Fungu 22: Huduma za Mfuko Mkuu**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2022/23, Fungu 022 liliidhinishiwa jumla ya **shilingi trilioni 2.224.** Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 9.452** ni kwa ajili ya mishahara ya maafisa wa umma wanaolipwa kupitia Fungu 022, na **shilingi trilioni 2.214** ni kwa ajili ya Huduma za Mfuko Mkuu ambazo ni michango ya mwajiri kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, bima ya afya, mfuko wa fidia kwa wafanyakazi, malipo ya pensheni kwa wastaafu. Hadi Aprili 30,2023, Fungu 022 lilipokea kiasi cha **Shilingi trilioni 1. 527** sawa na **asilimia 68.67** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 7.348** ni mishahara ya maafisa wa umma na **shilingi trilioni 1.418** ni kwa ajili ya Huduma ya Mfuko Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kufanya marejeo ya Viwango vya Pensheni ya Wastaafu kabla ya Miaka ya 1990 kabla ya kuanzishwa kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili viendane na hali halisi ya sasa hasa ukizingatia mfumuko wa bei uliopo. Hivyo ni vyema Serikali ikalifanyia kazi suala hili ili kuhakikisha viwango vya sasa vinaakisi uhalisia wa maisha ya sasa.

### 2.2.8. Fungu 23: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 48.758.** Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 2.845** ni fedha za Maendeleo na **shilingi bilioni 45.913** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, **shilingi bilioni 39.552** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi bilioni 6.361** ni kwa ajili ya Mishahara kwa watumishi wa Idara. Aidha, kati ya fedha za maendeleo **shilingi bilioni 1.880** ni fedha za ndani na **shilingi milioni 964** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia 30 Aprili, 2023 jumla ya **Shilingi bilioni 38.411** zimetolewa. Kati ya kiasi kilichotolewa **shilingi bilioni 36.961** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha Mishahara **shilingi bilioni 5.448** na matumizi mengineyo **shilingi bilioni 31.513**. Kwa upande wa fedha za Maendeleo **shilingi bilioni 1.450** zimetolewa ambapo kati ya kiasi hicho **shilingi bilioni 1.357** ni fedha za ndani na **shilingi milioni 93** ni fedha za nje. Muhtasari wa mchanganuo wa fedha zilizotolewa na zilizotumika umeainishwa katika Jedwali Na. 1 (ukurasa wa 5) na uchambuzi wa kina katika Jedwali Na. 5, Kiambatisho A.

**Mheshiwa Spika,** Pamoja na kwamba fungu hili lina Ofisi Mikoa yote Tanzania bara lakini ni fungu ambalo lina Bajeti ndogo ukilinganisha na majukumu yake. Fungu hili lina majukumu makubwa yafuatayo:- Kusimamia Sheria ya Fedha za Umma SURA 348, Kuandaa Miongozo ya Uhasibu (Accounting Manual), Nyaraka za Uhasibu (Accounting Circulars) na Nyaraka za Hazina (Treasury Circulars), kutathmini utekelezaji wake katika kuhasibu mapato, matumizi na mali za Serikali na kuratibu maboresho ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 na Kanuni zake, Kushauri na kutoa ufafanuzi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na kamati ya kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusiana na masuala ya usimamizi wa Fedha za Umma pamoja na kulipa kiinua mgongo na pensheni kwa wastaafu wanaolipwa kupitia Hazina. Bado fungu hili limekuwa halipati Bajeti ya Kutosha, Hivyo kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaliongezea fungu hili fedha ili litekeleze majukumu yake kikamilifu.

### 2.2.9. Fungu 50: Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2022/23, Fungu 50 liliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 107.795**kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Hata hivyo, fungu hili liliongezewa bajeti kwa njia ya uhamisho na kufanya jumla ya bajeti kufikia **shilingi bilioni 283.33.** Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 249.467** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 25.999** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa idara, vitengo na taasisi zilizo chini ya Fungu. Nyongeza ya bajeti kwa Fungu 050 ni kwa ajili ya malipo ya fidia na utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya ujenzi wa Mfumo mpya wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma wa (National e-Procurement System of Tanzani-NEST).

**Mheshimiwa Spika,** Hadi 30 Aprili 2023, jumla ya **shilingi bilioni 208.562** zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, sawa na **asilimia 73.61** ya bajeti ya mwaka baada ya uhamisho. Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 192.255** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 16.307** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa idara, vitengo na taasisi zilizopo chini ya Fungu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba Mchakato wa uuzaji wa Mali chakavu za Serikali umekuwa ukichukua muda mrefu hivyo kusababisha mlundikano wa mali hizo katika Ofisi za Umma. Hali hii imesababisha Ofisi za Umma kugeuka kuwa maeneo ya maegesho ya magari chakavu, samani na vifaa vya tehama. Aidha, changamoto hii imeendelea kuwa kubwa katika Balozi zetu nje ya nchi ambazo haziwezi ama kuharibu au kuuza mali ambazo hazitumiki mpaka Wataalamu kutoka Idara hii watakapothibitisha ambapo Afisa Mhakiki mali husafiri kwenda hadi Ubalozini kwenda kuhakiki mali za thamani ndogo ili ziuzwe. Kamati inashauri Serikali kupitia upya utaratibu wake wa kuuza mali chakavu ambapo Idara ya Mhakiki Mali za Serikali iwasilishe ripoti za utendaji kazi wake kila baada ya miezi 3. Vilevile, Serikali iangalie uwezekano wa kupitia upya Kifungu cha 6 cha Sheria ya Usimamizi wa fedha Sura ya 438 ili kuwapa majukumu Wakaguzi wa ndani na Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kushirikiana na Idara ya Mhakiki Mali za Serikali kuuza mali chakavu za Serikali.

## 3.0. UCHAMBUZI WA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele (c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 ina jukumu la kujadili kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Ndg. Charles Kichere Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili.

### 3.1. *Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Fungu 45*

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 iliidhinishiwa Jumla ya **Shilingi bilioni 90.32.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi bilioni 14.7** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi bilioni 63.7** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi bilioni 7.8 ni** fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka ndani na **shilingi bilioni 3.09** ni fedha za nje**.** Aidha, fungu hilo liliidhinishiwa kukusanya jumla ya **shilingi milioni 900** kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia Aprili, 2023 Ofisi imepokea jumla ya **shilingi bilioni 76.423** sawa na asilimia **85** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 73.257** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **shilingi bilioni 3.166** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2023 Ofisi ilikuwa haijapokea fedha za nje za Miradi ya Maendeleo.

**Jedwali Na 2: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi zilizotolewa hadi 30 Aprili 2023**

| MAELEZOYA BAJETI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA2022/23 | FEDHA ZILIZOPOKELE WAHADI 30 APRILI, 2023 | % YA FEDHA ZILIZOPOKELEWA | MATUMIZI HADI 30 APRILI,2023 | % MATUMIZI YA FEDHA ZILIZOPOKELEWA |
|---|---|---|---|---|---|
| **1. MATUMIZI YA KAWAIDA** | | | | | |
| Mishahara | 14,757,479,000 | 12,664,724,889 | 86 | 12,664,724,889 | 100 |
| Matumizi Mengineyo | 63,738,739,000 | 60,592,766,716 | 95 | 57,852,845,529 | 95 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida** | **78,496,218,000** | **73,257,491,605** | **93** | **70,517,570,418** | **96** |
| **FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO** | | | | | |
| Fedha za Ndani | 7,828,000,000 | 3,165,950,490 | 40 | 3,165,950,490 | 100 |
| 2.2 Fedhaza Nje | 3,098,935,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla ya Miradi ya Maendeleo** | **10,926,935,000** | **3,165,950,490** | **29** | **3,165,950,490** | 100 |
| **JUMLA FUNGU** | **89,423,153,000** | **76,423,442,096** | **85** | **73,683,520,908** | **96** |

***Chanzo**: Randama Fungu 45*

### 3.2. *Masuala ya Msingi yaliyobainika katika Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali*

**Mheshimiwa Spika,** Katika majadiliano masuala yafuatayo yalibainika:-

i. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haina rasilimali watu ya kutosha. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuongeza Watumishi katika Ofisi hii ili kuendelea kuimarisha utendaji kazi wake.

ii. Ofisi ina ukosefu wa fedha za maendeleo na hivyo kusababisha wakaguzi wa ofisi hii kuendelea kukaa kwenye ofisi za wakaguliwa jambo ambao lina athiri uhuru wa ofisi;

iii. Ofisi ya CAG haina uhuru wa kuajiri Wataalamu wenye ujuzi na taaluma inayohitajika katika Ofisi hiyo na badala yake ajira bado zinaamuliwa na Tume ya Ajira;

iv. Kuongezeka kwa maeneo ya ukaguzi kutokana na kukua kwa Sekta ya Umma hapa nchini. Maeneo hayo ni pamoja na Ukaguzi wa Sekta ya uziduaji, ukaguzi wa miradi ya ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi, ukaguzi wa mazingira, na ukaguzi wa usimamizi wa majanga na mabadiliko ya tabianchi ukilinganisha na rasilimali watu na fedha inazopatiwa ofisi hii;

v. Ofisi ya CAG inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa mifumo ya ukaguzi pamoja na maabara za kiuchunguzi na kiufundi; na

vi. Upungufu Mkubwa wa vitendea kazi ikiwemo tarakilishi mpakato na magari kwa ajili ya kaguzi mbalimbali kama vile kaguzi za Ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ndio jicho la Bunge katika kusimamia matumizi ya fedha za umma ni lazima Serikali itenge rasilimali za kutosha kwa ajili ya Ofisi hii. Kamati inaamini Ofisi hii ikiwezeshwa kikamilifu itapunguza ubadhilifu wa fedha za umma, kuziba mianya ya upotevu wa mapato, kuleta uwajibikaji na ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Serikali.

## 4.0. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

### 4.1. *Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu Tisa ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2023/24*

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi trilioni 15.94** kwa mafungu yote tisa (9). Kati ya kiasi hicho, **Shilingi trilioni 15.376** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 564.225** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 490.2** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 74** ni fedha za nje. Matumizi ya kawaida yanajumuisha **shilingi trilioni 1.693** kwa ajili ya mishahara na **shilingi trilioni 13.682** kwa ajili ya matumizi mengineyo**.**

***4.2. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24***

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza vipaumbele vyake imepanga kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 97.134** katika mwaka wa fedha 2023/24. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 87.722 ni** fedha za Matumizi ya Kawaida na **shilingi bilioni 9.412** ni fedha za maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 8.828** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 584** fedha za nje. Aidha, Ofisi hii imeidhinishiwa kukusanya **Shilingi milioni 900** fedha za Maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa ujumla bajeti ya Fungu hili imeongezeka kwa **asilimia 8.623** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ilifanya majadiliano na Serikali kuhusu bajeti ya Fungu hili na kubaini kwamba zilihitajika **shilingi bilioni 3** kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara ya kiufundi na kiuchunguzi. Kufuatilia majadiliano hayo Serikali ilikubali kuongeza kiasi hicho kwa ajili ya kutekeleza kazi husika. Muhtasari wa kina wa mchanganuo wa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/24 umeainishwa katika Jedwali Na. 6, Kiambatisho A.

**Jedwali Na. 3: Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mipango Mafungu yaliyochini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2023/24**

| FUNGU | MATUMIZI MENGINEYO | MISHAHARA | MIRADI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | 10,480,130,968,000 | - | - | 10,480,130,968,000 |
| 06 | 7,618,770,000 | 1,948,234,000 | 360,000,000 | 9,927,004,000 |
| 07 | 37,591,275 | 5,229,041,000 | 940,000,000 | 43,760,316,000 |
| 10 | 2,650,549,100 | | - | 3,463,849,000 |
| 13 | 3,861,365,000 | - | 455,000,000 | 4,316,365,000 |
| 21 | 745,547,085,000 | 1,610,820,134,000 | 497,756,575,000 | 2,854,123,794,000 |
| 22 | 2,301,774,127,000 | 13,065,211,000 | - | 2,314,839,338,000 |
| 23 | 51,029,321,000 | 7,157,764,000 | 1,880,000,000 | 60,067,085,000 |
| 50 | 52,703,766,000 | 54,120,209,000 | 62,833,919,000 | 169,657,894,000 |
| **JUMLA** | **13,682,907,226,100** | **1,693,153,892,900** | **564,225,494,000** | **15,940,286,613,000** |
| 45 | 70,830,676,000 | 16,891,720,000 | 9,411,878,000 | 97,134,274,000 |
| **JUMLA KUU** | **13,753,737,902,100** | **1,710,045,612,900** | **573,637,372,000** | **16,038,320,887,000** |

***Chanzo:*** *Randama za Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya CAG.*

## 5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kuchambua na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2023/24. Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

### 5.1. *Utendaji kazi wa Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko ya Kodi (Tax Ombudsman)*

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi hii ilianzishwa kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali za kikodi kutoka kwa wadau. Ofisi ya mpokea malalamiko ya kodi ilianzishwa kwa lengo la kupokea, kuchakata na kutoa mapendekezo kwa Waziri wa Fedha na Mipango juu ya malalamiko yote yanayohusu Kodi pamoja na usimamizi wake. Ni wazi kwamba Ofisi hii haijaweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, Ofisi hii bado haijajulikana kwa wananchi wengi zaidi ili itimize majukumu yake kama yalivyobainishwa kwenye kifungu cha 28A cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha Ofisi hii inatekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kuhakikisha inajulikana na kujitangaza kwa wadau wa kodi wote nchini kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo.

### 5.2. *Mashirika ya Umma na Makampuni yaliyo chini ya Msajili wa Hazina*

**Mheshimiwa Spika,** Uwepo wa Bodi kwenye Mashirika na Makampuni ya Umma ni jambo la msingi katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na ufanisi katika utendaji kazi na utawala bora. Kamati imebaini kwamba **kuna** baadhi ya Mashirika na Kampuni za Umma ambazo hazina Bodi na hivyo kukosekana kwa utawala bora kwenye uendeshaji wake. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa Mashirika na Makampuni ya Umma yanakuwa na Wajumbe wa Bodi ili mashirika hayo yajiendeshe kwa ufanisi na kwa kufuata misingi ya utawala bora.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto inayokabili mashirika kampuni na mashirika ya umma ni ukosefu wa mitaji ili yajiendeshe kibiashara. Katika shauri ufuatao:-

i. Kampuni na Mashirika hayo ya umma yajiorodheshe katika soko la mitaji kwa lengo la kupata mtaji badala ya kutegemea mitaji kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali; na

ii. Mashirika yanayotoa huduma yawezeshwe ili yaweze kujiendesha kibiashara kama vile Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

### 5.3. *Kutofautisha majukumu ya Mamlaka za Udhibiti (Regulatory Authority) katika ukusanyaji wa mapato na utoaji wa Huduma*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti inatambua umuhimu wa Mamlaka mbalimbali za Udhibiti ili kuleta ufanisi katika sekta mbalimbali. Hata hivyo uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Mamlaka hizi zimegeuka kuwa wakusanya faini, ada na tozo kutoka kwa sekta wanazosimamia kuliko kutekeleza majukumu yake ya Msingi. Kwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ndio yenye jukumu la kimuundo la kusimamia ukusanyaji wa mapato ni wakati sasa umefika wa kupitia Mamlaka zote za udhibiti ili kuangalia uhalali na ulazima wa Mamlaka hizo kutoza ada, faini na tozo mbalimbali ili kuangalia endapo zinafaa kuendelea kuwepo.

### 5.4. *Misamaha ya kodi kwenye Miradi ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika,** Utaratibu wa misamaha ya kodi unaratibiwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kumekuwa na ucheleweshaji wa uwasilishaji wa maombi ya msamaha kutoka kwa Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo basi Kamati inawataka maafisa masuuli wote kuhakikisha kwamba wanawasilisha maombi ya msamha ya kodi Wizara ya Fedha na Mipango kwa wakati ili kutokwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuondoa mlundikano wa bidhaa za Serikali Bandarini.

### 5.5. *Uhakiki na Ulipaji wa Hati za Madai*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kumekuwepo na ucheleweshaji wa madai ya wakandarasi, wazabuni na watoa huduma mbalimbali Serikalini hali inayosababisha kuongezeka kwa madeni ya wakandarasi, wazabuni na watoa huduma hao

kutokana na riba za madeni yao. Ucheleweshaji huu hutokana na uhakiki wa muda mrefu wa madeni hayo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inapitia upya utaratibu wa uhakiki wa hati za madai ili malipo ya wakandarasi, wazabuni na watoa huduma yafanyike kwa wakati. Hii itasaidia kuondoa ongezeko la gharama linalotokana na riba za madeni hayo.

### 5.6. *Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS)*

**Mheshimiwa Spika,** mfumo huu hausomani na mifumo mingine ya Serikali mfano mfumo wa malipo wa GePG. Aidha, mfumo huu umekuwa na mapungufu kadha wa kadha, kama vile mfumo kushindwa kutambua kiasi, Idadi, na hali za mali za Serikali zilizopo isipokuwa zile zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuwa mfumo huu hautumiwi na Mamlaka na Taasisi nyingine za Serikali, ugumu katika kutambua mali za Serikali zilizochakaa na zinazotakiwa kuondolewa katika matumizi ya Serikali pamoja na kutokuwa na uwazi katika uuzaji na ugawaji wa mali za Serikali zilizo chakaa. Hivyo, Kamati inashauri kwamba mfumo huu uboreshwe ili uweze kusomana na mifumo mingine ya Serikali. Ni wazi kwamba maboresho ya mfumo huu yataondoa changamoto kwa Idara ya Msimamizi wa mali za Serikali kutumia gharama kubwa kukagua mali zenye thamani ndogo.

### 5.7. *Mapendekezo ya Financial Action Task Force (FATF)*

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ilifanyiwa Tathmini ya mifumo ya nchi ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi pamoja na ufadhili wa silaha za maangamizi. Tathmini hiyo ilifanywa na Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Kupambana na Utakasishaji wa Fedha Haramu (ESAAMLG-East and Southern Africa Anti Money Laundering Group) mwaka 2021. Matokeo ya tathmini yalibainisha mapungufu katika mifumo ya utakasishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na silaha za maangamizi pamoja na matumizi ya teknolojia mpya katika uhalifu. Mapungufu hayo yalitokana na Tanzania kutotekeleza kikamilifu mapendekezo ya kikosi kazi kilichoundwa maalum kwa ajili ya kuweka viwango vya kimatiafa vinavyopaswa kutekelezwa na nchi 190 mwanachama udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu (Financial Action Task Force -FATF). Kutokukidhi kikamilifu kwa utekelezaji wa Mapendekezo ya FATF kuliiweka nchi katika uangalizi wa FATF kwa mwaka mmoja hadi Juni 2022 na

kusababisha nchi kuwekwa chini ya uangalizi mpaka pale itakaporekebisha upungufu huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali Kuandaa Sera na Mikakati ya kitaifa ya kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi itakayobainisha maeneo yenye vihatarishi ili kuweka Mpango wa Kitaifa na hatua za kuchukua. Aidha, Serikali iendelee kujenga uwezo kwa mamlaka zinazosimamia kuweza kutekeleza Mpango wa utekelezaji, pia Kuwajengea uwezo wataalam ili waweze kugundua, kuchunguza, na kupunguza matukio ya utakatishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi kwa kushirikiana na vyombo vingine vinavyohusika. Vilevile, kuna umuhimu wa kuunda na kutumia mifumo kwa ajili ya kuratibu ufanisi wa utekelezaji wa Maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa – (United Nations Security Council Resolutions – UNSCR) yanayohusiana na ufadhili wa kigaidi na silaha za maangamizi. Hatua hizi zitasaidia nchi kuendana na viwango vya Kimataifa vinavyotaka uwepo wa Sera na Sheria kuliko ilivyo hivi sasa ambapo kuna sheria tu. Hivyo ni vyema kuharakisha uandaaji wa Sera. Pia Serikali iongeze kasi katika kurasimisha Sekta isiyo rasmi ambayo ni takribani asilimia 60 ya uchumi wa nchi. Hatua hii itasaidia upatikanaji wa Taarifa ambazo ni muhimu katika kubaini na kuzuia utakatishaji wa Fedha Haramu na ufadhili wa ugaidi na silaha za maangamizi

## 6.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt Tulia Akson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yako wakati wa utendaji kazi wa Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, kwa kuendelea kukusaidia kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2022/23 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/24 ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yaliyo chini yake. Aidha, niwashukuru na kuwapongeza Dkt. Natu El-maamry Mwamba

kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ndg. Emmanuel Tutuba kwa kuteuliwa kuwa Gavana wa Benki Kuu, Kamati imepata ushirikiano mkubwa katika kipindi hiki cha Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndg. Charles Kichere, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Ndg. Alphayo J. Kidata na Wakuu wote wa Taasisi na Idara na Vitengo pamoja na watalaamu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Zainab Katimba, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** nimshukuru pia Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kazi ya uchambuzi na uwezeshaji wa Kamati ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inatambua na kuenzi mchango wa Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe akishirikiana na Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi pamoja na Makatibu wa Kamati kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalam.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango yanayojumisha Mafungu tisa (9) yaliyo chini yake pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2023/24 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**Daniel Baran Sillo,**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
07 Juni, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kusoma vizuri. Waheshimiwa kabla hatujaanza kuchangia, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikuombe, takribani mwezi mmoja uliopita kulikuwa na taharuki kubwa sana nchini, na hasa kwenye nyumba za wapangaji wa *National Housing* kutokuweza kununua LUKU kutokana na malimbikizo ya *property tax* ambayo ni jukumu la *National Housing.*

Wananchi hawa wakapewa adhabu ya kutokupata umeme kwa kosa ambalo si lao. *For three days* nyumba zote za ghorofa za *National Housing* wale ambao luku zao zilikuwa za chini walikosa umeme. Nikakufwata, nakushukuru sana ukaliona, ukazungumza na Waziri wa Ardhi, ukazungumza na Kamishna Mkuu wa *TRA* namshukuru sana, Ndugu Kidata, tukashirikiana na *National Housing.*

*National Housing* wameshaji-*commit,* wanataka deni hili au makato haya wafanye wao, uwezo huu wanao. Lakini sheria hairuhusu, sheria inasema mpangaji ndiye atakayelipa kodi ya majengo kwa bili yake ya umeme. Nikuombe na hili nalo ujaribu kulitazama kwenye *Finance Bill* ujaribu kulifanyia marekebisho haraka. Illimradi *National Housing* wameji-*commit,* ndio mwenye nyumba, aendelee kulipa yeye, na mwananchi aendelee kula starehe za nchi hii, asipate bugudha. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, wajiendae Mheshimiwa King na Mheshimiwa Sillo.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na heshima ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika bajeti hii ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuendelea kutupa uhai na afya ili kuendelea kuitumikia nchi yetu kupitia Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza mchango wangu, nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipenzi chetu, mama yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan; Waziri mwenye dhamana na viongozi wote wanaomsaidia Rais katika Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu leo tunaposimama hapa kuzungumza na kutathmini kazi ya Wizara ya Fedha tunayo furaha kwamba miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa sababu Wizara hii imesimama imara, lakini watumishi wa umma wanalipwa mishahara na stahiki zao kwa sababu Wizara hii imesimama imara; tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuanzia kwenye hali ya fedha nchini. Na hili kwa sababu sitapata nafasi ya kuchangia kwenye Bajeti Kuu, nimeamua hivyo, sitachangia kwenye Bajeti Kuu, kwa hiyo mchoko wangu wote unaohusu Wizara ya Fedha nataka niumalizie hapahapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni suala la hali ya fedha. Taarifa inaonesha kwamba katika mzunguko wa fedha mpaka Desemba, 2022 mzunguko wa fedha ulio rasmi katika nchi yetu, fedha zinazopita kwenye benki na zinazopita kwenye *mobile wallets,* yaani hizi M-Fedha, Tigo Fedha na nini, ni kiasi cha shilingi 30 kati ya 100. Katika kila shilingi 100 ni shilingi 30 tu ndiyo inayoonekana kwenye benki na kwenye hizi *mobile wallets*. Shilingi 70 nzima iko mikononi mwa watu, haijulikani iko wapi. Nyingine inaweza ikawa iko nje, nyingine imefichwa. Waziri wa Fedha analifahamu hili vizuri. Nilitaka kujua Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Wizara yake wamejipangaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu hawakuacha fedha nyumbani bila sababu, wana sababu. Sababu ya kwanza ni hii Sheria yenu ya *Anti-Money Laundering*. Mtu akipeleka fedha milioni 10 tu vyombo vyote vimemtolea macho. Wameamua ya nini, wanaweka nyumbani, wanatulia wanakuwa salama kuliko kufuatwafuatwa. Namna gani ata-*harmonize* hii hali ili watu waweze kuleka fedha benki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni tozo za *transactions* na za kikodi zilizoko kwenye benki; mtu anaona ya nini, acha niweke fedha zangu ndani. Wafanyabiashara wameweka fedha zao ndani. Kati ya kila shilingi 100 ni shilingi 30 tu ndiyo inayoonekana kwenye vyombo vya fedha, zote nyingine hizi ziko huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hilo tu, kingine wanataka kuelimishwa tu, kuna *ignorance* katika masuala ya fedha. Wako watu kwenye minada ya mifugo wanataka wapate fedha *cash,* wapo watu kwenye migodi, hasa wachimbaji wadogo wanataka wapate fedha *cash,* kwa hiyo fedha inatembea huko mikononi; wapo watu katika kuuza mazao wanataka waone fedha *cash*. Tutafanya nini, tuawahamasisha namna gani watu? Maana yake hali hii si nzuri. Benki zetu nyingi sasa zimepoteza *liquidity,* hali ya *liquidity* kwenye benki imekuwa ni mbaya kiasi ambacho sasa benki nyingi zinashindwa kukopesha. Ukienda benki wanakuzungusha miezi miwili, miezi mitatu, wanashindwa kukopesha, *liquidity* hakuna. Fedha iko nyumbani kwa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya nchi ukifika ukianza kushuka kwenye asilimia kama hii kadri unavyokwenda ndiyo unaitisha sasa fedha zote zirudi Benki Kuu ubadili fedha kwa sababu watu wanaficha fedha. Na hili nataka niseme, ni lazima sisi kama nchi kupitia Wizara yetu ya Fedha tufike mahali tukae na wafanyabiashara wakubwa na wa kati kuwahamasisha, kuwaeleza sasa nchi ni salama, hakuna matishio ya fedha zao ili waweze kuruhusu fedha zirudi benki. Hali si nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unapokuwa na shilingi 30 kati ya mia ndizo inayozunguka, hata kodi za Serikali unakusanya kwenye shilingi hizi 30, kwa hiyo na Serikali nayo inapoteza. Lazima utueleze tunafanyaje kutoka hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linahusu sera za kikodi; hili ni letu sote. Sera za kikodi zimechangia sana kuua biashara. Leo hii mmekwenda mpaka na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutatua matatizo Kariakoo. Kariakoo imekufa kwa sera za kifedha ambazo sisi wote tunahisika, sitaki kuwatupia lawama ninyi peke yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka sera nyingine za kulinda viwanda ambavyo havipo. Na viwanda vingine tulivyoamua kuvilinda wala vyenyewe havijilindi, vinachukua *raw material* asilimia 90 kutoka nje zinasema hizi zinaingia kwenye mnyorro wa thamani kumbe wanachukua majora kutoka nje wanakuja ku-*print* hapa. Kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba sera za kikodi zemechangia sana. Leo biashara ya vitenge ilikuwa nchi zote jirani walikuwa wanakuja kuchukua vitenge Tanzania, sasa vitenge tunakwenda kuchukua Malawi, tunakwenda kuchukua Zambia kwa sababu kontena la futi 40 hapa nchini kodi yake ni milioni 378, lakini Zambia ni milioni 30, Kenya ni milioni 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi unafikiri ukishafika mahali ukawa na sera za kikodi za namna hiyo unachotaka ni nini? Kinachotokea ni kwamba unavutia biashara kwa wenzio unaua biashara ndani, ndiyo yale yanayotokea pale Kariakoo. Tunataka kwenda kuwakamua watu wachache wanaoingiza kidogo, inashindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lazima niesme kwamba kwa sababu sitachangia kwenye Bajeti Kuu, nataka nilieleze hili kwamba sera zetu za kikodi ni lazima tuzitazame ili zituwezeshe kufika mahali kufanya sekta hii binafsi ambayo inaajiri watu wengi iweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilieleze ni suala la maamuzi tunayoyafanya hapa Bungeni ikiwa ni pamoja na kupitisha bajeti. Mheshimiwa Waziri wewe unakumbuka bajeti iliyopita tulipokaa hapa umetangaza kushusha kodi inayoitwa *hotel levy* inayotozwa na halmashauri zetu kwa kila mpangaji anayelala kwenye *guest house*. Ukatoa kwenye asilimia 10 kuleta kwenye asilimia tano. Lakini nataka nikwambie zipo halmashauri nyingi mpaka sasa zinaendelea kutoza asilimia 10 na watu wanalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa na Serikali ambayo huku juu wakisema chini hawatekelezi, ukiwauliza – maana sisi ni wawakilishi wa wananchi – unawauliza wanasema hayo yalisemwa huko hatuna waraka. Mimi nilifika mahali mpaka baadhi ya watendaji wa Serikali nikawauliza hivi ingekuwa imepandishwa mngesubiri waraka? Lakini kwa sababu imeshushwa mnasubiri waraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri, unapofika mahali ukatoa maelekezo hapa ya kifedha katika nchi, na wewe ndio Waziri wa Fedha, toa waraka kwenda kwenye vyombo vyote vinavyohusika kusimamia utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii najiuliza sasa wale wanaoendelea kutozwa asilimia 10 mpaka sasa Serikali itawarudishia? Na nitakuomba utakapokuwa unafanya majumuisho hapa ueleze, maana nisije nikaonekana labda mimi nasema uongo. Lakini ninachosema ni sahihi, kodi ya *hotel levy* ilishushwa kutoka asilimia 10 kuja asilimia tano lakini zipo halmashauri mpaka sasa zinaendelea kutoza asilimia10…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu umekwisha eeh? Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa King, jiandae Mheshimiwa Sillo.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa hii nafasi na uwezo wa kusimama hapa, lakini pamoja na wewe kunipa nafasi hii kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ilikuwa nizungumze kidogo kwa rafiki yangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hapa, naona leo alikuwa yuko doro doro kwa sababu jana Yanga ilitoka *draw* halafu Simba kashinda saba, ndiyo maana alikuwa yuko mnyonge mnyonge, ule ndio unyonge wake. Lakini sasa mimi nataka nimtoe unyonge na ninataka achangamke kutokana na haya ambayo nayaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *paragraph* ya 36 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameelezea pale huduma za pensheni na mafao ya watumishi ambapo kwenye randama tumekwenda kuangalia katika Fungu 23 ambayo ni Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye pensheni mimi nina hoja mbili, ya kwanza, wazee ambao walishastaafu wanapata taabu kupata pensheni zao na kupata viinua mgongo vyao, hususan wa kutoka Zanzibar. Hawa wa kutoka Zanzibar ni lazima wafunge safari waje zao Dodoma ili kuja kufwata mafao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo wanakwenda, wanarudi mafao yale hawayapati, mwisho kinachotokea wanafanya maamuzi ya kusamehe. Kwa maana hiyo naweza nikasema kwamba Wizara ya Fedha inawadhulumu wazee wetu wastaafu wa Jamhuri ya Muungano ambao wanaishi Zanzibar kwa sababu baadaye mwisho wanaamua kusamehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo majina hapa, na mimi mwenyewe nimeshughulikia kesi hizi moja baada ya nyingine. Kuna jina la mzee Mohamed Seif Maftaha ambaye ni marehemu, urithi wake unashughulikiwa na na Bi. Pili Ramadhani Saidi. Huyu nimekuja mpaka nimegonga mwamba, mpaka leo mafao yake hajapata, pia kuna Bi. Zuleha; hajapata; kuna Bi. Ruzuna. Hawa wote nimewaleta mimi nimewaweka hapa Dodoma, hawakupata. Tatizo liko wapi Mheshimiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa au kanda zote kuna ofisi ndogo ya Hazina, lakini kwa nini Zanzibar hamuweki ofisi ya Hazina kuondosha huu usumbufu? Ingekuwepo Ofisi ya Hazina hawa watu wangelishughulikia kulekule, ingekuwa ni rahisi. Kwa hiyo tunawatesa wazee na tunawadhulumu fedha zao. Lakini mimi naahidi hapa nitaendelea kuwafuatilia hawa wazee. Na Mheshimiwa angalia sana katika pensheni, angalia sana katika sehemu hiyo, watu wanadhulumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili kwa Mhasibu Mkuu; tulitembelewa hapa na Jumuiya ya Wazee Wastaafu. Jumuiya hii wana malalamiko mengi, yanafika hata 30, lakini kubwa wanalosema ni kwamba pensheni zao wanalipwa siyo kwa mujibu wa sheria, sheria haifuatwi, Sheria ya *PSSF* haifuatwi, na ile nyongeza iliyotoka Hazina nayo pia haifatwi. Kwa maana hiyo wazee wanadhulumika. Ombi lao wanasema Mheshimiwa Waziri uunde *task force* uwasikilize malalamiko yao; usipounda *task force* hawa wazee nao wataendelea kudhulumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mfano mmoja. Kuna mzee mmoja alisema analipwa pensheni ndogo, tukazungumza na maafisa wako, siku ya pili alipewa pensheni anayostahili na akapewa malimbikizo yake. Sasa wazee kama hawa wako wengi. Kwa hiyo tunaomba hawa wazee uwashughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 10; kwa mujibu wa Katiba fungu hili linasimamia uhusiano wa kifedha. Uhusiano huu wa kifedha hapa nimekusudia kuzungumzia mikopo ya nje. Mikopo ya nje ambayo inaingia katika nchi hii inastahili kwamba Zanzibar mgao wake ni 4.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya tafiti kupitia taasisi hizi zifuatazo; Wizara ya Fedha yenyewe, *IMF, World Bank, African Development Bank, Tanzania Coalition on Debt and Development (TCDD)* na taasisi nyingine. Nimegundua kwamba hata asilimia mbili Zanzibar katika ile mikopo ya kutoka nje hapati. Na mikopo ya nje ni suala la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukitaka kujua kwamba ni suala la Muungano, akikorofisha Zanzibar mkopo unazuiliwa. Kulikuwa kuna mkopo hapa wa *NCC* ambao ulikuwa unakuja kwenye *REA* lakini ilivyotokea vurugu kule Zanzibar mkopo huu ulizuiliwa kwa sababu mkopo ni Muungano. Sasa hii asilimia nne utakaposimama Mheshimiwa Waziri, ninaomba utupe majibu ya kutosha hii asilimia nne ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, nimefanya utafii kupitia *IMF* sasa hivi ni kigezo kipi kinatumika katika kupata mikopo Zanzibar. Nimeona *document* ya Tanzania kwenye *IMF* kwamba mnatumia *financing gap* ili ku-*finance* au kupata mikopo ya nje. *Finance gap* ya mwaka 2021/22 ilikuwa 866. Sasa je, tunatumia *financing gap,* hiyo *financing gap* mnachukua na *financing gap* ya Zanzibar au mishatumia hiyo *financing gap,* kwamba mnatafuta 4.5, na hapa tutazame. Hiki kigezo kimewekwa tangu mwaka 1994 wakati wa mzee Malecela katika tume yake, sasa je, bado ni *valid* ibakie hiyohiyo 4.5? Na sasa hivi kuna *variables* nyingi sana zimebadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dk.t. Mwigulu, atakapokuja hapa nataka anipe ufafanuzi katika suala hili la 4.5 katika mambo mawili, je, ilikuwa ikilipwa kwa mikopo yote? Kwa sababu kuna mikopo ya *basket fund* tunajua haziwezi kuhusika. Lakini cha pili, je, hii *rate* ya 4.5 ni *valid?* Mbona mkienda *IMF* mnatumia *financing gap*. Ninataka uje utupe ufafanuzi, kama hatukupata ufafanuzi sisi Wabunge ambao tunatoka upande wa pili kule hatuwezi kuomba maji hapa, hatuwezi kuomba elimu hapa, hatuwezi kuomba afya, tunashughulikia huu uhusiano. Kwa hiyo uje utuambie uhusiano huu ukoje na nini kinapatikana katika uhusiano huu, kipi kilistahili kupatikana katika uhisiano huu; lakini je, bado *factor* hii ipo, na mnatumia sasa *variables* nyingine kwenda kukopea. Sasa tunataka Mheshimiwa uje utupe

ufafanuzi, kama sitaridhishwa na majawabu yako nimekusudia nikamate shilingi. Nitakamata shilingi ili tupate ufafanuzi kwa sababu hakuna uwazi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mikopo inatoka *World Bank* ilikuwa inashughulikia masuala ya utoaji wa haki, zikajengwa mahakama Tanzania nzima. Lakini mkopo ule wa *World Bank* kule Zanzibar haukufika. Kuna mikopo ilikuwa ikishughulikia kutatua msongamano katika miji mikuu, msongamano ule tukajenga madaraja maeneo chungu nzima, mkopo ule kule Zanzibar haukwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika hii *REA* tunayozungumzia, *portion* ya *REA* tunatoa fedha ambazo nyingine unachangia kutokana na tozo ya mafuta, lakini nyingine tunachangia kutokana na mkopo. Sasa huu mkopo unatoka nje na haukuja kwenye basi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili hiyo.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja endapo nitapata ufafanuzi, vinginevyo nitashikilia shilingi. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sillo, jiandae Mheshimiwa Reuben.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara yetu hii ya Fedha na Mipango. Awali ya yote, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa letu. Tunamwombea afya njema ili aendelee kututumikia. Pia niwapongeze Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri pamoja na Timu nzima ya Wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya kusimamia fedha na sera za fedha za kikodi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na Wajumbe kwa kazi kubwa tuliyofanya katika kukamilisha taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia mambo machache. La kwanza ni mfumo wa TEHAMA wa ukusanyaji wa mapato ya *TRA* pamoja na *TPA*. Sisi wote ni mashahidi kwamba mifumo ya ukusanyaji mapato ni ya muhimu sana katika kukusanya mapato ya Taifa letu. Mifumo yetu hii ina changamoto zifuatazo:-

(i) Mfumo wa kodi za ndani bado haujakamilika, unasuasua;

(ii) Mfumo wa kodi za ndani kutokusomana na mfumo wa kodi za forodha; na

(iii) Mfumo wa forodha kutosomana na mfumo wa *TOS* wa *TPA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokamilika kwa mfumo wa kodi za ndani ni *risk* kubwa sana katika kupotea kwa mapato ya Taifa letu. Kwa hiyo niombe sana Wizara ya Fedha kuhakikisha inasimamia kukamilisha mfumo wa kodi za ndani ili kuweza kuimarisha mapato yetu ya ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote ni mashahidi kwamba asilimia 40 ya mapato yote ya *TRA* yanakusanywa kwenye Idara ya Forodha, lakini kutokusomana kwa mfumo wa kodi ya forodha na Bandari ni changamoto kubwa sana ya upotevu wa fedha hapa nchini. Kwa hiyo nishauri sana Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango wahakikishe mifumo yetu ya mapato inasomana ili kuboresha mapato ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa Tatu wa Miaka Mitano wa Mwaka 2021/2022-2025/2026 yako mambo ambayo yameainishwa. Kwanza, mchango wa kodi kwenye pato la Taifa kufikia asilimia 13, lakini bajeti yetu ya Serikali karibu asilimia 60 inategemea mapato ya kodi zetu hapa nchini, lakini Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2025 ukisoma ukurasa wa 16 imezungumzia kuboresha mapato ya Taifa letu. Ili

kufikia malengo haya ni lazima kuwekeza katika mifumo ya ukusanyaji mapato hapa nchini ili nchi yetu iweze kufikia hatua hii ya asilimia 13 ya pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu kwenye nchi zinazotuzunguka, mchango wa kodi kwa Nchi ya Kenya kwa pato la Taifa ni asilimia 16.9, mchango wa kodi pato la Taifa kwa Nchi ya Rwanda ni asilimia 14.1, lakini sisi Tanzania asilimia 11. Kwa hiyo kama nchi tuna kazi ya kufanya kuhakikisha kwamba tunaimarisha mifumo yetu ili tufikie malengo haya kwa manufaa makubwa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ni mikataba ya kutokutoza kodi mara mbili, yaani *double taxation agreement* na nchi yetu na nchi mbalimbali. Mwaka jana nilichangia jambo hili pia na narudia tena. Nchi yetu iliingia mikataba ya kutotoza kodi mara mbili na nchi mbalimbali kwa lengo la kuondoa vikwazo vya kibiashara lakini na kuongeza biashara baina ya nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba ilikuwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi yetu na *Canada* kwenye *income and capital tax treatment* ya mwaka 1995, *Finland* na *Tanzania Income tax and Capital tax* ya mwaka 1976, *Denmark* na *Tanzania Income and Capital Tax* ya mwaka 1976, India na Tanzania Income Tax Treaty ya Mwaka 1979, *Italy* na *Tanzania Income Tax Treaty* ya mwaka 1973, *Norway* na *Tanzania Income and Capital Tax Treaty* ya mwaka 1976, *South Africa* na *Tanzania Income Tax Treaty* ya mwaka 2005 na *Sweden* na *Tanzania Income and Capital Tax Treaty ya* mwaka 1976 na Zambia na *Tanzania Income Tax Treaty* ya mwaka 1968.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba hii tunajua ni muhimu lakini ya muda mrefu sana. Aina ya biashara leo zimebadilika, mazingira ya biashara yamebadilika, teknolojia imekua na tuko kwenye *digital economy*. Kwa hiyo kutokana na mazingira niliyotaja hapo juu ni muhimu sana mikataba yetu hii ya kikodi ikarejewa ili kuona nchi zetu zote zinapata manufaa ya mapato yanayostahili ya kikodi katika nchi zetu hizo. Kwa hiyo naomba

jambo hili, Wizara ya Fedha walichukue kwa umakini mkubwa. Mikataba hii ni ya muda mrefu, mikataba ya miaka 50. Tuna kila sababu ya *ku-review* kuangalia ni namna gani nchi yetu inanufaika kupata kodi stahili katika mikataba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu. Ndani ya uongozi wa miaka miwili imesaidia mikataba hii ya kikodi ya tozo mara mbili ya Nchi za Falme za Kiarabu pamoja na Oman, kwa hiyo hatua hii ni muhimu, itaongeza uwekezaji hapa nchini lakini itapanua wigo wa kodi na kwa kukuza uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo tunaipongeza Serikali kwa hatua hii nzuri na Wizara ya Fedha waendelee kusimamia jambo hili kubwa la kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni kuboresha Kitengo cha Ukaguzi wa Kodi *(Tax Audit)*. *Tax Audit* ni kitengo ambacho kinasaidia sana:-.

(i) Kuimarisha ulipaji wa kodi ya hiari *(voluntary tax compliance);*

(ii) Kuongeza mapato ya Taifa letu; na

(iii) Inatoa elimu kwa walipakodi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lazima liende sambamba na hawa wakaguzi wenyewe, lazima wapate *exposure* kwa maana ya kupata mafunzo ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo. Leo hii tuko kwenye teknolojia ya hali ya juu. Elimu imebadilika biashara zinafanywa kidigitali, kwa hiyo ni lazima na wataalam wetu tuwafundishe, wapate ujuzi wa kutosha. Ziko nchi zilizoendelea zaidi katika eneo hili la ukaguzi. Waende kule wakajifunze kwa ajili ya manufaa makubwa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na nashukuru sana ka kupata nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante. Mheshimiwa Ruben, jiandae Mheshimiwa Zaytun, angefuatiwa na Mheshimiwa Simon ambaye ana dharura.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu, Wizara ya Fedha. Mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati yetu ya Bjeti, Kamati ambayo ina dhamana ya kuisimamia Wizara hii ya Fedha. Kwenye majukumu yetu pamoja na maeneo mengine tunasimamia Mafungu mbalimbali kwenye Wizara hii likiwemo Fungu la Hazina, Huduma za Mfuko wa Jamii, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Msajili wa Hazina, Deni la Serikali, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu, Tume ya Pamoja ya Fedha na Wizara ya Fedha yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo nataka nizungumzie Fungu moja katika haya. Fungu namba sita, Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali. Bajeti zetu hizi ambazo tumekuwa tukizijadili hapa mara tu baada ya kuzipitisha, Serikali inakwenda kutekeleza bajeti hizi na kule zinakokwenda jicho letu pekee ambalo tunalitegemea ni Wakaguzi Wakuu wa Ndani kwenye Halmashauri zetu lakini na kwenye Taasisi mbalimbali za Serikali zinazopokea fedha kutoka kwenye bajeti hii tunayopitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana 2022/2023 kwa maana ya mwaka huu wa fedha unaokwisha. Fungu hili Na.6 kwa maana ya Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali tulimpa fedha bilioni saba, milioni mia nane na themanini na tisa, laki moja na themanini na nne na mwaka huu tumempitishia bilioni tisa, imeongezeka kidogo na tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuliwezesha Fungu hili kwa kuliongezea fedha ili likafanye kazi zake za ukaguzi. Tumewapa bilioni tisa, milioni mia tisa ishirini na saba na elfu nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukafanye mapinduzi kwenye Idara hii ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali ili jicho letu kwenye fedha za umma likaongezeke. Lazima tuifanyie mapinduzi idara hii ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali. Mapinduzi ya kwanza ambayo tunatakiwa tuyafanye ni ya

kimuundo, lazima tubadilishe muundo. Nitatolea mfano, Wakaguzi wetu ambao wako kwenye halmashauri zetu wakishafanya ukaguzi wao, wakamwandikia Mkurugenzi, akajibu na Wakuu wake wa Idara, wakapeleka kwenye Kamati ya Ukaguzi na wakapeleka kwenye Kamati yao ya Fedha, ripoti yao moja kwa moja wakiiandika inakwenda *straight* kwa Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba ukichukua ripoti zote za nchi nzima zikapelekwa moja kwa moja kwa mtu mmoja pamoja na kwamba ni taasisi, hawezi kuwa na uwezo wa kuyachakata yote na kutupa majibu. Hawezi kuwa na uwezo wa kuyachakata yote na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachopendekeza na ninachoshauri hapa huu muundo lazima tuubadilishe. Lazima tuwe na Mkaguzi Mkuu wa Ndani ngazi ya Mkoa ili sasa wale wa Wilaya wakishachakata taarifa zao na kuziandikia, taarifa ikatue pale Mkoani. Ukishakuwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwenye kila Mkoa, *definitely* itakulazimisha kuwa na ofisi za kanda. Kwa hiyo wa Mkoa atazichakata za Mkoa mzima halafu ata-*submit* kwenye kanda yake halafu wale wa kanda ndio wapeleke kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali. Kwa kufanya hivyo…

**MHE.ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anaendelea kuchangia vizuri sana. Nataka nimpe tu taarifa hapo anapopaona kwamba patengenezwe au pawe na Wahasibu Wakuu, Wakaguzi Wakuu wa Ndani wa Mikoa. Nataka nimpe taarifa hawa wapo kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ni Makatibu Tawala Wasaidizi, Ukaguzi wa Ndani wa Mkoa, lakini hawana kazi hiyo. Wana kazi ya kukagua wilayani na Ofisi ya *RAS* tu, kwa hiyo wapo hao. Wapewe majukumu ya kwenda kusaidia watendaji hao wa halmashauri kwenye ukaguzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruben taarifa hiyo?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa. Ninachokisema hapa, nataka tufanye marekebisho kidogo yule *Chief Internal Auditor* kwenye Ofisi ya Mkoa, aendelee kubaki pale kwa sababu kila Afisa Masuhuli lazima awe na *Internal Auditor,* yeye abaki pale afanye mambo yake hayo ya kumwangalia *RAS,* afanye mambo ya kumwangalia *DAS*. Sisi tunamtaka Mkaguzi wa Ndani Mkuu Mkoani ajitegemee kabisa *separate* na yule wa pale kwa *RAS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kwamba, yeye a-*consolidate* zile zote za wilaya zote ndani ya Mkoa na kuzichakata na kwa muundo huo tukishakuwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani kila Mkoa, *definitely* itatupeleka kwenye ofisi za kanda ambazo nazo zitachakata, halafu ndio zimpelekee sasa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali. Tukifanya hivyo tuna-*ensure* mambo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kwenye ukaguzi kinacho *matter* ni ubora wa taarifa. Tukifanya hivyo tutakuwa tumepata *quality assurance* lakini tutakuwa tumepata *quality control,* lakini sivyo hivyo tutakuwa tumeifanya kazi ya Mkaguzi Mkuu, *CAG* yule kazi yake itakuwa ni rahisi sana anapopita na kazi yake ikiwa rahisi itakuwa *accurate,* lakini wakati huo huo fedha zetu za wananchi tutakuwa tumezilinda. *CAG* akishakuwa na kazi ndogo tutataka sasa Serikali imwongezee fedha nyingi ili yeye awe anafanya *real time audit*. Tukifanya hivyo tutakuwa tumefanikiwa kuzuia majambazi yote yaliyopo ndani ya mfumo wa Serikali ambayo yanaiba fedha zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tumefanikiwa kuzuia watu wote ambao sio waaminifu ambao wanaiba fedha zetu na kwa maana hiyo taarifa ya *CAG* itakuwa inakuja ikiwa safi na fedha za wananchi zikiwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa taarifa wa Wakaguzi wetu wa Ndani; moja ya eneo ambalo lazima tulifanyie maboresho, kwamba Mkaguzi wa Ndani mathalani Halmashauri ya Handeni Mjini anaandaa taarifa yake halafu anaipeleka moja

kwa moja kule kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu. Taarifa yake anaipeleka moja kwa moja halafu Mkaguzi Mkuu yuko chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Kwenye ukaguzi huu tunapokagua kuanzia kwa Wakaguzi wa Ndani tunamkagua na huyo Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Haiwezekani wewe uwe unajikagua mwenyewe, unajiletea mwenyewe halafu taarifa unakaa nazo

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna tabia ya watu wakipelekewa hizi taarifa za ukaguzi wanazipiga *polish* wanazing'arishang'arisha hivi, zinawafurahisha furahisha halafu wanakaa nazo. Haitakiwi kuwa hivyo, tunachotaka, taarifa ikitoka kwa *Internal Audit* wetu wa halmashauri, iende kwa yule *Internal Auditor* wa Mkoa. Ikitoka kwa yule wa mkoa, iende kwenye kanda, halafu iende kwa Katibu Mkuu Kiongozi, *Pay Master General* yeye apewe taarifa tu, kwa sababu ndiye anayekaguliwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanye hayo mapinduzi, wasipofanya haya tutaamini kwamba wana nia ovu ya kuendelea kufuja fedha za Watanzania. Taarifa zote za kikaguzi na taarifa mbalimbali za wachambuzi wa mambo ya kikodi, ya kikaguzi, ya fedha za wananchi, zimekuwa zikionesha kwamba tumekuwa tukipoteza trilioni nne mpaka tano kila mwaka kwa kuibiwa kwa sababu ya mifumo kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi ya pili ambayo nataka tuyafanye, ni kuwawezesha wakaguzi kuwa *conversant* kuijua mifumo inayotumika kwenye taasisi zetu. Mifumo kama vile *GePG*, mifumo kama vile *PlanRep, MUSE,* ule unaotumika kwenye afya *TANePS* na sasa tunaubadilisha kuwa *NeST* na ule wa *TAUSI* na mifumo mingine mingi ambayo inatumika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Reuben, mfumo wa *time* uko tayari. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simon ajiandae.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara muhimu, bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze sana na nimshukuru Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuendeleza miradi mbalimbali ya kimkakati na nimshukuru pia katika Mkoa wa Arusha tumeona miradi mbalimbali ya maendeleo ikitekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Wizara ya Fedha wakiongozwa na Waziri wetu, Naibu wake pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii wamekuwa wakiipa Kamati ya Bajeti ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala moja la mifumo yetu ya ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa mapato yetu hususan mapato ya ndani. Natambua jitihada kubwa sana zinazofanywa na Mamlaka yetu ya Serikali Mtandao yaani *e-GA* katika kuratibu na kusimamia mifumo ya TEHAMA Serikalini, lakini bado changamoto ni nyingi na wana kazi kubwa ya kufanya katika kuhakikisha basi mifumo yetu ya matumizi mbalimbali ya Serikali inatumiwa kwa usahihi ili kuondokana na hizi changamoto nyingi ili basi tuweze kudhibiti makusanyo yetu tunayopata.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za mifumo hii bado ni nyingi, utakuta makusanyo mengi yanafanyika nje ya mifumo. Mifumo yetu bado haisomani kama walivyosema wenzangu, lakini vile vile hata mapato yale inayokusanya yanacheleweshwa kupelekwa benki, lakini vile vile mengine hayaendi benki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya bajeti imeweza kukutana na Wizara mbalimbali pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali na moja ya changamoto walizonazo ni makusanyo hafifu ya mapato ya taasisi hizo. Hii imetokana na ukosefu wa mifumo imara ya kuhakikisha makusanyo yetu yanadhibiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii imetokana kwa kiasi kubwa na bajeti finyu inayotengwa kwa ajili ya kuhakikisha tunakuwa na mifumo imara ya kudhibiti na kusimamia mapato yetu ya Serikali. Ukiangalia hadi Aprili 2023 ni taasisi 968 tu zimeunganishwa na mfumo wa *GePG,* bado taasisi nyingi sana hazijaunganishwa na mfumo huu wa *GePG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali *(GAMIS)* bado haisomani na mifumo mingine, lakini bado mifumo ya forodha haisomani na mifumo ya bandari na hii inaleta changamoto kubwa sana ya Serikali yetu kupoteza mapato kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kamati ilivyoshauri basi ni lazima Serikali ije na mipango mikakati na mipango mahsusi ya kuweza kuwa na mifumo imara, mifumo inayosomana ili tuweze kudhibiti mapato yetu tunayopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia tu kwenye uwiano wa kodi kwa pato la Taifa yaani *Tax to GDP Ratio* utaona kabisa Tanzania bado tuko chini sana ya wastani ukilinganisha na kanda zingine ambazo tumejiunga nazo kama Kanda ya Afrika Mashariki na Kanda ya *SADC*. Hadi Aprili, 2023 Tanzania tuna wastani wa asilimia 11.7 tu. Ukiangalia wastani wa Afrika Mashariki ina wastani wa asilimia 13, *SADC* asilimia 24 na hii inatupa tafsiri gani? Inatuonesha kwamba ukusanyaji wa mapato bado uko chini ukilinganisha na ukuaji wa pato la Taifa. Kwa hiyo ukusanyaji wa mapato ya ndani bado hautoshelezi Serikali kukidhi mahitaji yake ambayo yanaongezeka kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo niliyosema, naungana na maoni ya Kamati kwamba Wizara hii iweze kufanya kazi na iweze kuja na mpango mahsusi katika kuhakikisha kwamba

tunakuwa na ukusanyaji wa mapato imara, lakini tunadhibiti mapato ambayo tunayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba sana Waziri wakati anahitimisha hapa tusichukulie suala la mifumo ni kawaida, naomba sana tuondoke kwenye masuala ya kawaida tuje kwenye mpango mkakati basi ili Wizara zote ziweze kuwa na mifumo imara tuweze kuongeza mapato yetu. Tukiweza kuongeza mapato yetu kupitia mifumo hii, tutaweza pia kuwezesha bajeti yetu kwenye mapato ya ndani kwa kiasi kikubwa kuliko sasa hivi tunavyotegemea kuwezesha bajeti yetu kwa mapato ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Simon Songe, jiandae Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia Wizara hii ya Fedha. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anazoendelea kufanya pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyoendelea kusimamia Wizara yetu ya Fedha na kuhakikisha kwamba Sera zinatekelezwa vizuri kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo moja au mawili ambayo natamani kuyazungumza siku ya leo kuishauri hii Wizara. Kuna sehemu aliyochangia kaka yangu Mheshimiwa Mbunge wa Handeni, habari ya Kitengo cha *Internal Audit* katika Halmashauri zetu pia kwenye Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna shida ipo kwenye kitengo hiki. Kwanza kabisa, lazima tufahamu kwamba bado kuna tatizo kubwa sana la uhuru. Wakaguzi wetu wa Ndani hawana uhuru kwa sababu wanaripoti moja kwa moja, sehemu kubwa wanawezeshwa na Maafisa Masuuli. Unakuta Afisa Masuuli huyo ndiyo anaeombwa gari kwa ajili ya Mkaguzi wa Ndani kwenda kufanya ukaguzi *site*. Akipenda anaweza akatoa gari, asipopenda anaweza asitoe gari, *at the same time* Mafungu

bado yapo kwa Afisa Masuuli kwa sababu kazi hizi zinafanywa na mapato ya ndani lakini pia na mapato ya *OC* kutoka Serikali Kuu. Sasa hapa uhuru lazima ukosekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshauri Mheshimiwa Waziri sasa, kuhakikisha kwamba wanatengeneza *vote*, mwaka jana tulipitisha hapa tukakubaliana kwamba watengeneze *vote* kwa ajili ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani ili aweze kupeleka rasilimali huku chini kwa Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri lakini Wakaguzi wa Ndani wa Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kitakachopatikana hapa? Wakaguzi wa Ndani watakuwa na uhuru wa kufanya kazi zao bila kumtegemea Afisa Masuuli. Afisa Masuuli atakuwa anapewa taarifa za kiukaguzi kama Meneja wa sehemu husika kwa sababu ndiye anayetakiwa kujibu zile hoja za Mkaguzi wa Ndani. Tukilifanya hilo tutawapa uhuru mkubwa kwa sababu sasa hivi hawana uhuru wa kusema wakati wanatekeleza majukumu yao ya ukaguzi wa fedha zetu ambazo tunapeleka fedha nyingi kwenye Halmashauri na tunapeleka fedha nyingi kwenye Wizara zetu lakini Wakaguzi hawa wa Ndani hawana ule uhuru wa kutekeleza majukumu yao kwa sababu Maafisa Masuuli ndiyo wanaowawezesha kutekeleza yale majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawawezi kufanya kwa sababu Afisa Masuuli huyo huyo unamwandikia kwenda kukagua mradi wakati anajua mradi huo una matatizo, atakuchenga wala hatakupatia fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo. Fedha zitoke moja kwa moja kwa *Vote* ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani zishuke chini ili waweze kufanya kazi kwa uhuru mkubwa na tutaweza kuona matokeo ya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuziimarishe hizi Kamati za Ukaguzi za taasisi husika. Mheshimiwa Waziri, kuna sehemu nyingine hata hizi Kamati hazipo, kuna baadhi ya Halmashauri hata hizi Kamati hazipo, hazijaundwa. Ukisoma *Public Finance Act* ya Mwaka 2010 *Cap.* 348 inaeleza vizuri kabisa lakini kuna baadhi ya sehemu Kamati hizi hazipo, sasa ufanisi wao unakosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili ufanisi wao upatikane ni lazima pia mzifuatilie Kamati hizi na kuona kama zinafanya kazi. Vilevile, nazo pia bado zinakumbwa na tatizo la uhuru kwa sababu Kamati zinategemea posho kutoka kwa Afisa Masuuli, ni lazima tutengeneze vizuri hapa ili tuweze kufanya vizuri zaidi kwa ajili ya hizi Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni rasilimali watu. Bado Wakaguzi wa Ndani ni wachache, ongezeni Wakaguzi wa Ndani kwenye Taasisi za Serikali ili tuweze kupata ufanisi wa kazi ambazo wao wanazifanya. Unakuta kwenye Halmashauri kuna Mkaguzi wa Ndani mmoja lakini kazi ziko nyingi, atafanyaje kuhakikisha kwamba hizi kazi zinafanyika na kudhibiti huu ubadhirifu unaoendelea katika kazi zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nimekiona na kimekuwa kikija kwenye Kamati na nimekiona ni kizuri ambacho kinafanywa na *CAG* na tunatamani pia kifanywe na Idara hii ya Ukaguzi wa Ndani, ni zile kaguzi za *performance audit (Value for money)* lakini pia *real time audit.* Kaguzi hizi zikifanyika kwa wakaguzi wa ndani zitatusaidia pia kuhakikisha kwamba tunalinada rasilimali zetu tulizo nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninataka kuomba nini? Mheshimiwa Waziri sasa ni lazima mfikirie kuajiri *professionals* nyingine zaidi ya *professional* za kihasibu katika hizi kaguzi zetu za ndani, lazima pia tuwe na *Engineers* kwenye Idara ya Ukaguzi wa Ndani ili anapokwenda kukagua miradi awe anajua anakwenda kufanya nini, kwa sababu kinachofanyika sasa hivi Mkaguzi wa Ndani ni Mhasibu anakwenda kukagua kwenye jengo fulani, anapokuwa anafanya kazi za *value for money,* inabidi sasa kwa sababu anakuwa hajui chochote kuhusu *Engineering* amuulize *Engineer* wa halmashauri kwamba hivi ilitakiwa kuwa nondo ngapi? Wakati huyo *Engineer* ndiye mkaguliwa! Sasa hii haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuweke *professional* zingine kwa hiki kitengo cha *internal audit* ili kiweze kufanya kazi vizuri. Vilevile Mheshimiwa Waziri tuwape mafunzo. Mambo yanabadilika lakini bado hatuwapi mafunzo. Tuwape mafunzo

Wakaguzi wa Ndani, Wahasibu wa Halmashauri na Wahasibu wa Taasisi zetu ili waweze kufanya kazi sawa sawa na miongozo mipya pamoja na miongozo ya kiuhasibu inayotoka ili watekeleze majukumu yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta Mhasibu yuko Halmashuri miaka 15 anaandika *voucher, voucher* kila siku halafu unaita tuna Mhasibu! Hapana. Uhasibu siyo kuandika *voucher* tu peke yake, afanye na majukumu mengine. Mpelekeni kwenye *training*, mpelekeni kwenye mafunzo ili ajue ni mabadiliko yapi ya kiuhasibu ambayo yanatokea katika miaka mbalimbali ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukiangalia kama sikosei ni mwaka 2022 au 2021 kuna mabadiliko ya hizi *IPSAS,* Hisa na vitu vingine lakini ukuwauliza wale Wahasibu walioko kwenye Halmashauri na walioko kwenye Wizara kuna wengine hawajui kabisa kama kuna mabadiliko lakini mabadiliko yapo. Unakuta kuna mabadiliko ya watu kusaini, kuna mabadiliko mbalimbali ya kifedha lakini wao wanatengeneza vitabu vyao vya hesabu ukilinganisha na sera zilizokuwepo toka mwanzo bila kufuata mabadiliko ambayo yametokea hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nikuombe tenga fungu kwa ajili ya mafunzo kwa *Internal Auditors*, tenga fungu kwa ajili ya mafunzo kwa Wahasibu ili waweze kuendana na kasi ambayo inatakiwa na kuweza kufanya kazi katika nchi yetu na kazi zenye ufanisi. Tunataka kuona kazi zenye ufanisi katika Halmashauri zetu, tunataka kuona kazi za ufanisi katika Wizara zetu ili tumrahisishie *CAG,* muda mwingine tunampa *CAG* kazi kubwa bila sababu wakati kuna Wakaguzi wa Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasunga jiandae Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya, niwapongeze pia Watendaji wote wa Wizara na taasisi zote zilizoko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, wanafanya kazi vizuri na sisi sote tunaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Wizara ya Fedha ni kubwa na wao wenyewe wameidadavua katika ripoti yao katika taarifa ambayo wamewasilisha ni nyingi na ni kubwa na wanafanya vizuri, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo kama mawili au matatu ambayo nitajaribu kuzungumzia kwa kifupi. Jambo la kwanza nataka nianzie kwenye eneo la bima. Bima, kuna bima ya lazima na kuna bima za hiyari. Hasa kwenye eneo la bima hapa, katika nchi yetu yapo magari ya Serikali hayana bima, yapo majengo ya Serikali hayana bima, yapo majengo ya kibiashara hayana bima, matokeo yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ajali nyingi zinazotokea barabarani nyingine nyingi zinasababishwa na madereva wanaoendesha magari ya Serikali. Sasa matokeo yake magari yale yanawagonga watu, yanagonga mali za watu binafsi, yanasababisha hasara kubwa. Kwa utaratibu wa nchi zote gari ikikugonga au ikagonga mali au ikaleta hasara yoyote, yule anayepata hasara anatakiwa afidiwe na bima. Kwa utaratibu wa sasa hivi wa magari ya Serikali ambayo hayana bima maana yake nini? Wale wanaogongwa wanapata hasara hawana mahali pakujitetea wala pakuomba fidia. Sasa hili siyo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Serikali zetu mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar. Zanzibar wameliona na wamerekebisha sheria, magari yao yote ya Serikali yanalipa bima ya lazima ili yakisababisha hasara watu waweze kufidiwa. Tanzania Bara bado, sisi huku bado. Nadhani umefika wakati tuangalie hili, watu wanaathirika, watu wanaumia, watu wanapata majanga mengi na hakuna fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumeshuhudia kwenye jengo la kibiashara la hifadhi ya jamii pale Dar es Salaam, *lift* imedondoka na watu wamekwenda mpaka chini wameumia, hawana mahali pa kuomba fidia! Sasa hili lazima Wizara ilitazame na ione kwamba kuna haja ya kuja na mfumo wa kuhakikisha kwamba magari yote ya Serikali, majengo ya kibiashara na mengine yote yaweze kupata bima ya lazima ili kujikinga na majanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri ulifanya kazi nzuri na tulikupongeza kabisa. Mwaka jana katika Bunge hili, aya ya 113 kwenye Sheria ya Bima Sura 394 ulisema hivi: "Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bima kwa kuongeza wigo wa bima ya lazima *(mandatory insurance)* kwa kujumuisha masoko ya umma, majengo ya biashara, bidhaa zote zinazoingizwa kutoka nje, vyombo vya baharini na vivuko. Hatua hii ina malengo ya kuimarisha ushirikishwaji wa kifedha *(financial inclusion)* na kuleta matumizi sawia ya bima". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili ulileta zuri tukakupongeza Mheshimiwa Waziri, toka *Financial Bill* ile imepitishwa mwaka jana mpaka leo hii hamjaanza kuifanyia kazi, Kanuni bado hazijatoka kwa nini? Sasa kazi tuliyoifanya mwaka jana mpaka sasa hivi bado hamjaleta Kanuni! Sasa Kanuni hizi tungependa Mheshimiwa Waziri mzilete mzifanyie kazi. Mwaka umemalizika maana yake hii Sheria haijaanza kufanya hii kazi, kwa hiyo, ni vizuri mkaifanyia kazi, ikaanza kufanyakazi ili sasa ndiyo pale nasema tuongeze magari yote ya umma yanayosababisha ajali barabarani yawe na bima ya lazima ili nayo hiyo sasa wananchi waweze kunufaika, ile hasara wanayoipata waweze kufidiwa. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo mimi nimeona ni la msingi sana na ni muhimu mkalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ningependa Wizara ya Fedha mlifanyie kazi, ni kuiangalia upya Sheria ya Fedha za Umma Sura 348. Sheria ile Mheshimiwa Waziri ilitungwa mwaka 2011 na kuna marekebisho kadhaa yamefanyika mpaka mwaka 2020. Marekebisho yale yote ukiyaangalia Sheria ile inasema, lengo la Sheria ni kuleta usimamizi mzuri wa makusanyo na matumizi ya fedha za umma na kulipa Bunge madaraka ya kusimamia fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, sasa tulipofika sasa hivi ukiitafsiri maana ya ile ni kwamba inazungumzia *cash budget,* inazungumzia fedha taslim. Sasa, sasa hivi uwanja mpana tunaouzungumzia kwenye usimamizi wa fedha za umma, tunazungumzia kwa mapana *(financial management)* siyo *cash financial management. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *financial management* ni zaidi ya hii sheria hii inavyosema. *Financial management* kwangu mimi ninavyoona Sheria hii sasa tuiongezee meno, tuiongezee upana, tuitazame upya ili sasa *financial management* iwe ndiyo msingi wa hii sheria ambayo tunaizungumzia ya mwaka 2001. Maana yake sasa miaka 23 imeshapitwa na wakati ni wazi mambo mengi yamebadilika. Kwa hiyo, sheria hiyo inatakiwa iangalie uandaaji na usimamizi wa bajeti ya nchi, hii sheria inatakiwa iseme. Pia sheria hii inatakiwa iseme usimamizi wa mapato na matumizi ambayo ndiyo inasema sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inatakiwa inagalie mipango ya kodi mbalimbali na usimamizi wa mali zake, hii sheria lazima iseme. Sheria hii inatakiwa pia kubainisha na kuangalia namna tutakavyoitumia katika kudhibiti hali ya baadae *(forecasting)* tuta–*forecast* mambo mbalimbali yanayojitokeza kwenye dunia. Mabadiliko mbalimbali yanayojitokeza hii sheria inatakiwa iwe ndiyo msingi wa kuweza ku – *forecast* kuangalia nini tunatakiwa kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo kutafuta vyanzo vipya vya mapato, sheria inatakiwa ituoneshe, zaidi ya hapo kufanya maamuzi ya ushirikiano yaani kuangalia kama *major* na *acquisition* na mambo mengine mengi kama kuangalia madeni ya Taifa na mali za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja lakini naamini Mheshimiwa Waziri ataenda kuiangalia hii sheria ili iwe ya muhimu zaidi, ahsante sana, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nusrat, jiandae Mheshimiwa Zainab Katimba, jiandae Mheshimiwa Jumanne Kishimba.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri pia nimesoma maoni na mapendekezo ya Kamati, ninakubaliana na maoni na mapendekezo ya Kamati kwa vitu walivyoshauri namna bora ambavyo tunaweza tukaboresha mfumo wetu *especially* wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia eneo moja tu na ni kwa wema sana, kwa sababu mimi naamini namna bora ambazo tunaweza tukafanya kusaidia nchi yetu ni pamoja na kujengea uwezo Wizara hii, kwa sababu Wizara hii kila Wizara nyingine zote tukilia hakuna barabara, tukilia hakuna maji, tukilia kuna shida hatuna madawati, hatuna madarasa, bado tutanyooshea mikono, tutawanyooshea vidole Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami siamini kama kweli Serikali haina mapenzi na wananchi wake, siamini kabisa. Kwa hiyo, ninaamini sana Wizara hii pamoja na Serikali lengo lake ni kuhakikisha kwamba wanajenga uwezo wa Watanzania kukusanya kodi wenyewe, ili baadaye wakitaka kuzitumia wazitumie kwa kuona maendeleo ambayo walikusanya kodi leo barabara inapitika, mimi naamini hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na makandokando yote lakini kama Wizara ya Fedha kwenye kitengo cha kukusanya kodi, itakusanya kodi kama inavyostahili sidhani kama kaka yangu Mwigulu kama ambavyo muda wote amekuwa akisimama humu akiambiwa sasa peleka pesa, peleka pesa sidhani kama wanazo fedha halafu hawataki kupeleka, siamini kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitazungumzia mwenendo wa ukusanyaji wa kodi na upotevu wa mapato kwenye Taifa letu. Kwanza hazijabadilika sana, takwimu

hazijabadilika sana za wanaolipa kodi mpaka sasa hivi tunavyozungumza hazijabadilika sana, bado *range* haijafika milioni tano, yaani hapo haizidi hapo kama imezidi haizidi hapo. Kwa hiyo bado tuna *tax base* ndogo mno ambayo tunalazimika kuwaminya wachache ambao ndiyo tunaowahesabu kama ndiyo walipa kodi. Kwa hiyo, bado hoja yangu ya kuongeza *tax payers,* kuongeza *tax base* idadi ya walipa kodi kwenye nchini kwetu ni hoja ambayo nitaendelea kuizungumza, kwa sababu naamini tukilipa kodi wengi tutakuwa tunaminyana kidogo kwa sababu tuko wengi tunachangia, tofauti na mkiwa na walipakodi wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna nchi nyingine jirani na tukisema tunataja majirani siyo kwa sababu kwetu hatuthamini, tunajaribu kwa sababu kama tuko kwenye uwanda mmoja, kama tuko *African Community* pamoja, ninaamini tunajifunza humu kwa sababu kuna *agreements* nyingi tunaingia vikao pamoja mpaka miaka ya fedha tumeirudisha nyuma, wote wameirudisha nyuma nchi zao, tumekuwa pamoja tunamaliza Juni 30, Mwaka wa Fedha unaanza tarehe 01 Julai, *East Africa* yote, ndiyo maana tunasema kama ni mifano ambayo haihusiani na Malaysia huko na wapi, basi ya humu pia tuisikie kwa sababu ni *East African community.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nchi kama Kenya ambayo *tax base* yao ni angalau ni watu milioni saba wanalipa kodi *plus,* Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, amezungumza pia hata namna ambavyo *GDP* Kenya, Rwanda mchango wa mapato ya kodi kwenye *GDP* sisi ni asilimia 11, natamani sasa tuone namna gani tunaweza tukaboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma taarifa ya Wizara ukurasa wa tano ambayo ameeleza mwenyewe Mheshimiwa Waziri, miongoni mwa vipaumbele vyake, Mwaka wa Fedha uliopita na Mwaka wa Fedha huu ni kukusanya, kudhibiti upotevu wa kodi na kuhakikisha kwamba wanadhibiti matumizi bora ya fedha za umma, *which is* nzuri sana, lakini ukienda kwenye mikakati yake kwenye kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali

anasema kufanya doria kwenye mipaka, lakini pia kidhibiti mifumo ya TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shida yangu iko hapo kwenye Mifumo ya Tehama, kwa sababu kama tunazungumza *digital economy* na hatuzungumzi namna bora ya kudhibiti upotevu wa fedha; kwa sababu takwimu zilizotajwa na Viongozi wa Serikali ni kwamba tunapoteza shilingi milioni 500 mpaka shilingi bilioni moja kwa siku kwenye mifumo ya Tehama. Nataka niwaambie hizo ni takwimu zilizotajwa na Serikali. Nawapa *benefit of doubt,* lakini tukienda *into details,* ni zaidi ya hizo fedha tunazopoteza kwenye mifumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko tayari kuwasaidia Serikali. Kama kweli hatuna *resources*, tuna vyuo, tume-*train* vijana wetu, wana uwezo, wana elimu kubwa ya *cyber security,* tumeshindwa kutumia *investments* zetu za shule, tumeshindwa kusomesha vijana kwenye vyuo ambavyo tunaweza kusema tunaviamini ili wazuie upotevu wa fedha, tuko tayari. Mimi nipo tayari kusaidiana na Waziri tukutafutie wataalam *the best,* na ni Watanzania. Wengine wamechukuliwa na nchi nyingine kwenda kusaidia kudhibiti upotevu wa fedha. Sisi tunao watu wetu ambao ukiongea nao wanakwambia wewe Mchaga gani hupendi hela? Watu wana mipango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana, *probably* kuna *possibility* kubwa sana ya kwamba wanaopiga hizo pesa ni watu wa kwenye mifumo huko huko. Ndiyo maana hawatafuti suluhisho la kudumu la kuzuia upotevu wa fedha. Watanzania sio wapuuzi kwenda kuweka fedha zao kwenye mifuko ya rambo nyumbani kwao. Siyo kwamba hawapendi nchi yao, hawataki kulipa kodi ndiyo maana wanapeleka huko, usalama wa fedha zao ni changamoto. Tunaweza tukatumia fedha ndogo sana kutengeneza mfumo ambao utatusaidia kuwa na *strong cyber security* ili kuwe na uhakika wa fedha za watu wetu, ziwe na usalama wa kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima waangalie *how best* tunaweza tukatumia teknolojia, tukatumia *investment* zetu zote na *resources* zetu zote kuweka mfumo wa

udhibiti wa upotevu wa mapato ya kidigitali. Sasa hivi dunia haizungumzi mapato, magendo eti mpakani yaani mpaka naona vibaya kwamba kwa nini nipo kwenye…, kwa sababu naona kama tunazungumza miaka ya 1980 huko. Kwa nini hivi vitu bado vipo? Siyo sawa. Naona kama tunafikiri kurudi nyuma, badala ya kufikiri kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, tangu Bunge la Kumi, Bunge la Kumi na Moja, Bunge la Kumi na Mbili tunazungumza hivi hivi kwamba mifumo haioani, yaani mifumo haisomani, na tuna kitengo cha teknolojia. Eti hatuna kompyuta, hatuna *laptop*. Yaani bado tunazungumza hivi vitu hii nchi! Mimi nafikiri siyo sawa. Ifike hatua sasa habari ya mifumo haioani iishe. Kwa sababu mimi naamini kwamba hivi vitu ni vidogo vidogo ambavyo mnaweza mka-*deal* navyo kwenye Wizara huko huko. Kwa sababu kama una Wizara nzima ina-*deal* na masuala ya teknolojia, kwa nini bado unahangaika eti mifumo haioani? Sioni kama ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingine kama ya Kariakoo ambayo inajitokeza pale, ni vitu ambavyo mimi naamini, kaka yangu wewe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri wa Fedha, hivi vitu unaweza kuvi-*clear* kabisa. Watu wataona hawaumii sana kama wanalipa kodi wengi. Ningekushauri, natamani kuiona Tanzania ambayo hatutumii fedha tena, yaani tumeenda *cashless* kabisa, kwa sababu ndiyo dunia inapoenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza nikakushauri kwamba ukitangaza leo unabadilisha fedha, utaona fedha zitakakotoka kuja *BOT*. Kwa sababu unahitaji kuwekeza kwenye kuwapa watu elimu waone hawapigwi, yaani hawapigwi. Ndiyo dunia inavyotaka twende. Halafu jipe *time*, wekeza kwenye kuelimisha watu. Kwa sababu Watanzania wanatamani tuongee hivi taratibu, yaani kwa sauti ndogo tu kwamba ni wajibu wa kila Mtanzania kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hawaelewi, tutumeni sisi wengine. Mimi nitajitolea hata kwenda kuwa Balozi. Jamani, usipolipa kodi barabara haipitiki, hatutapita. Tukisema hakuna madarasa, maana yake tunategemea tulipe kodi sisi. Bila hivyo, tutaendelea kwenda kuomba huko misaada huko nje na kila siku

tunalalamika deni la Taifa linakua, lakini tukilipa kodi wenyewe, tunachagua wenyewe cha kufanya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Unga mkono hoja basi. Unga mkono hoja. Mheshimiwa Nusrat, mbona huungi mkono hoja!

Mheshimiwa Waziri, anayosema Mheshimiwa Nusrat ni maneno muhimu sana. Nimeona vilevile kwenye bajeti ambazo wakati mwingine mnatenga. Mifumo hii, pesa mnazotengea ni nyingi mno; Dola milioni 200, Dola milioni 300, wala haihitaji pesa kama hizo. Kwa hiyo, inaelekea ninyi huko mnaingizwa mkenge na mashirika mbalimbali ya kuwadanganya gharama ni kubwa, wakati hakuna gharama kubwa kama hizi. Hakuna kabisa. Kwa hiyo, ni lazima na ninyi mrudi nyuma, mjaribu ku-*scout* bei ya chini lakini *proper competent company* ambayo inaweza ikawasadia kukusanya. Huna haja ya kutoa Dola milioni 200 kabisa.

Sasa nilishamwita Mheshimiwa Katimba, namwita Mheshimiwa Kishimba halafu Mheshimiwa Vuma.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya katika kuhangaika kuwaletea maendeleo wananchi wake. Tuendelee kumuombe afya, umri na uwezo zaidi wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu na timu yake nzima ya Wizarani kwa kazi kubwa anayofanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutimiza malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka kuanza kuzungumzia suala muhimu sana ambalo lipo kwenye Sheria ya Manuuzi *(Public Procurement Act)*. Sheria hii ya Manunuzi inataka kwamba Maafisa Masuuli wote watenge asilimia 30 ya Manunuzi ya Taasisi zao wanazozisimamia ziende kwenye makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria haijaishia hapo. Sheria chini ya Kanuni zake, kwenye Kanuni ya 30(c)(2), inasema kwamba, Maafisa Masuuli watakaoshindwa kutekeleza Sheria ya kutenga asilimia 30 watoe maelezo kwa nini wameshindwa kutekeleza? Haiishii hapo, inasema kwamba Maafisa Masuuli ambao hawatasimamia sheria hii watapewa adhabu, yaani watawajibishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze leo hii kwamba utekelezaji wa Sheria hii uko vipi? Maafisa Masuuli wangapi wametoa maelezo na wangapi wamewajibishwa? Tupate ripoti ya utekelezaji wa sheria hii. Kwa sababu sheria zimetungwa na Bunge, inabidi zisimamiwe. Kanuni imeenda kukazia na kuweka msisitizo. Hii ni sehemu ambayo Mheshimiwa Rais anataka kuwasaidia wananchi wake, anatengeneza mazingira ya kuwawezesha, kila siku anazungumza. Sasa fursa kama hizi ambazo zimewekwa vizuri kwenye sheria, kwa nini hatusimamii utekelezaji wa sheria zetu ili tuweze kuwanufaisha wananchi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, nataka kuzungumzia maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan. Tumemsikia katika majukwaa tofauti tofauti, katika mikutano tofauti tofauti akisisitiza na akiweka mkazo kabisa anataka wananchi waweze kutengenezewa mazingira mazuri ya kufanya biashara ili waweze kujitengenezea kipato. Imefika hatua tulimsikia Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara amesema kwamba Mheshimiwa Rais ametoa ruhusa ya msamaha wa kodi kwa biashara mpya zilizo kuanzia miezi sita mpaka mwaka. Tunataka kufahamu utekelezaji kwenye suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa kulipa kodi ya mapato ni kufanya biashara na kupata faida. Ile faida ndiyo inatozwa kodi

ya mapato. Sasa mtu anayeanza biashara, kabla tu hajaanza biashara, anapopewa makadirio ya kodi, anaambiwa aanze kulipa kwanza robo ya kwanza ya yale makadirio, kabla hata hajafanya biashara, atumie mtaji wake kulipa kodi, msingi wa hiyo kodi unatokana na nini? Kwa sababu sheria inataka kodi ya mapato itokane na faida. Ndivyo sheria inavyosomeka leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anatengeneza mazingira mazuri sana ya kuwawezesha wananchi wake, mbona hatuoni sheria zikiletwa zifanyiwe marekebisho?

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nami naomba nimpe taarifa mchangiaji, Mheshimiwa Zainab Katimba, kwamba siyo tu huyo mfanyabiashara anatakiwa akadiriwe hiyo kodi wakati anaanza, lakini pia atatakiwa kufanyiwa mahesabu na wahasibu, nao anatakiwa awalipe kabla hajaanza hata hiyo biashara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa taarifa yake, naipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, msingi wa hayo maboresho yote ni kwamba tunataka tutengeneze mazingira rafiki na mepesi ya kufanya biashara ili watu wengi waweze kuingia katika mfumo rasmi, warasimishe biashara zao, tuongeze wigo wa walipa kodi, na tuongeze mapato ya Serikali. Kwa hiyo, naomba nisikie kutoka kwa upande wa Waziri kwenye eneo hili, wamejipanga vipi? Kwa sababu hapo tayari ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusiana na Mfumo wa Usimamizi wa Mali za

Serikali *(Government Asset Management Information System - GoMIS)*. Kwanza Sheria ya Manunuzi *(Public Procurement Act)* na *Public Finance Act* inaeleza bayana kabisa kwamba Mlipaji Mkuu wa Serikali ndiye ambaye amepewa dhamana ya usimamizi wa mali zote za Serikali. Utaratibu mzuri wa usimamizi wa mali za Serikali umewekwa kwenye sheria hizi nilizotaja na pia kwenye mwongozo ule wa *Public Asset Management Guideline* ya 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo uko vizuri, lakini kwenye eneo moja la kuuza mali chakavu zile za Serikali, mfumo wa kitehama upo, lakini mfumo ule bado haujaweza kusomana na mifumo mingine muhimu. Kwa mfano mfumo wa malipo ya *GePG* lakini bado mfumo ule kuna Maafisa Masuuli ambao hawajapewa *access,* hawawezi kuutumia. Kwa hiyo, inapofika wakati wa mali chakavu za Serikali, inabidi ziuzwe, kuna hatua moja ambayo *Pay Master General* inabidi amwelekeze mhakiki aende akafanye *verification* ya zile mali kwamba ni chakavu ili utaratibu wa kuziuza zile mali/wa kuzi-*dispose* uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *process* hiyo ndiyo tayari kuna mkwamo, kwa sababu mfumo huu wa Tehama hauna teknolijia ya kuweza kufanya *verification* kwa kutumia Tehama. Tumeona hapa, sisi tumeanza hapa Bungeni tukiwa tuko kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapo nje, tumeweza kuona Bwawa la Mwalimu Nyerere *live,* utafikiri tuko huko *site*. Kwa nini? Kwa sababu tumetumia Tehama, ile teknolojia ya *virtual reality*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tehama imefikia katika hatua ambayo kuna vitu vingi vinaweza kufanyika bila kuhitaji mtu kufika yeye mwenyewe *site*. Kwa hiyo, naomba waboreshe mfumo huu kwanza uweze kusomana na mifumo muhimu na hasa mfumo huu wa *GePG*, pia waweze kutumia teknolojia hii kama za Tehama ili kuweza kurahisisha utaratibu wa *verification* wa uhakiki wa zile mali ili kuondoa mlundikano wa mali za Serikali Tanzania nzima ambazo zinasubiri kuuzwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Baada ya mchango huo, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 30 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri kwa Kilimo, ambao ni viongozi wa Chama na Serikali kutoka Mtaa wa Swaswa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Askofu Gwajima kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 28 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mwalimu Nyerere UVCCM kutoka Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Kuna wageni 100 wa Mheshimiwa Rose Busiga ambao ni walimu na wanafunzi kutoka *Blessed Mabuba Secondary School* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 110 kutoka Chama cha Skauti tawi la Shule ya Awali na Msingi ya *Greenbelt* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kishimba, halafu wajiandae Mheshimiwa Vuma na Mheshimiwa Komanya.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Bajeti ya Wizara ya Fedha. Nami namshukuru Mheshimiwa Rais, Waziri wa Fedha na timu yake nzima kwa kuleta bajeti kwa ajili ya Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza Mheshimiwa Kilumbe hapa akiongea suala la dola na pia kulikuwa na swali asubuhi. Sisi kwetu kwenye majimbo yetu ndipo yalipo masoko ya dhahabu. Soko langu la dhahabu kwenye Mji wa Kahama, kutoka benki zilipo ni mita 50. Sasa najaribu kujiuliza, hivi kweli unaweza kuwa una soko la dhahabu inayochimbwa na wenyeji na ukasema

tena hauna dola kwenye mita hizo hizo? Inatupa wakati mgumu sana wa kufikiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Mtemi Mirambo wakati Waarabu wanakwenda kuchukua pembe, wakija na pembe kumi, alikuwa anachukua mbili. Wakitoka huko na bunduki, anachukua bunduki mbili na yeye, badaye wanabadilishana. Sasa wewe unachukua dhahabu, unai-*charge* shilingi. Milambo alikuwa anachukua pembe kumi. Kwa nini usikate hata kipande cha dhahabu ukapata dola? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tulie kabisa kwamba hatuna dola? Soko la Geita linaongoza leo kwa dhahabu, lakini dhahabu ni dola. Kuna tofauti gani wewe unanunua ndege, inafuata watalii China, inawaleta mpaka Ngorongoro, wanakuja unawatengenezea na chakula, ndiyo wanakupa dola, lakini unakataa dola inayochimbwa kama mihogo kuja nyumbani kwako, unakataa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri alifikirie kwa mapana sana. Maana yake kwa muda tunao-*delay* inaweza ikatuweka kwenye matatizo makubwa, maana watu wanapata riba wakati wanasubiri dola. Pale kwangu Kahama mimi mwenyewe nimetafuta Dola 1,000 nimeshindwa kupata, lakini *opposite* yake kuna tani za dhahabu. Tuombe tu wenzetu wa Wizara ya Fedha waondoe huo uoga. Wanaogopa nini? Huwezi kuwa na dhahabu ukasema huna dola, haiwezekani. Kwa kweli ni kitu ambacho kinatuhuzunisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la *share*. *Share,* ni Wazungu walikaa miaka 100 iliyopita kule Ulaya wakatengeneza huo utaratibu. Utaratibu huo ulivyo sasa hivi, kuna migogoro mingi sana. Nitatoa mfano. Shirika la Ndege la *Precision* watu wamenunua *share,* watu wamenunua *share* hata za *Voda,* za *Tanzania Oxygen*, lakini mpaka leo hakuna pa kuuza hata kama unaumwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndege ya *Precision* inakwenda Mwanza, ina nafasi kumi ambazo hazina watu. Kwa nini mimi mwenye *share* siruhusiwi kukata *against share* kwenye ile tiketi ili

wakakata kwenye ile *share*? Kama wewe unasema kwamba mali hii ni ya kwangu, unakataaje? Mimi nina *share* kwako, kwani mimi nikinunua ng'ombe kwako, si zinagongwa tu mhuri kwamba hizi ni za fulani, akija saa yoyote mpatie. Haiwezekani! Maana yake mtu amenunua *share.* Leo *Voda* anachenga hapa wakati alichukua hela za watu, sasa kama hawezi kuuza *share,* si tukate kwenye vocha? Awe anatukata kwenye vocha, yeye anachukua zile *share*? Ni kama vile tulimkopesha. Hilo nafikiri, pamoja na kwamba inaonekana utaratibu ni mgumu, lakini wenzetu lazima walifikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, pana suala gumu sana hapa, Mheshimiwa Dkt. Kimei anafahamu. Sisi na Mheshimiwa Dkt. Kimei tumeteuliwa kwenye Kamati ya kuanzisha Benki ya Wachimbaji, lakini kuna mgogoro ndani ya hili suala. Kule Mwanza tulianzisha *Mwanza Community Bank,* ikatayarishwa vizuri na tukachanga zaidi ya Shilingi bilioni mbili na kitu, lakini ilivyokuja Sheria ya Benki Kuu, inasema wewe kama huna elimu au hukusoma elimu hii ya fedha huruhusiwi kuwa *Body of Directors* kwenye ile benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nimekusanya Shilingi milioni 500, halafu nimetoa kwenye benki kama nanunua *share,* naambiwa siruhusiwi kuwa kwenye *Body of Directors*. Sasa kwani kupata Shilingi milioni 500, kwa nini usiandike hizo *CV* zangu kwamba aliuza miwa, mihogo akauza hiki, akapata Shilingi milioni 500! Kwa nini usii-*convert* hiyo ikawa ni *degree* au elimu, ukaniruhusu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikupe Shilingi milioni 500, wewe uje na tai na cheti cha *degree,* nikukabidhi fedha zangu, itawezekana kweli! Tukajitoa na Simiyu *Community Bank* na yenyewe hivyo hivyo wote tukajitoa, tukasema haiwezekani, lazima mbadilishe, mturuhusu tusimamie fedha zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo najaribu kumwuliza Mheshimiwa Waziri, tutafanya nini kwenye hii benki ya wachimbaji? Mtawapata wachimbaji wenye *degree!* Mmeshawaambia au mtazua mgogoro tena! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wameshachanga zaidi ya bilioni mbili juzi Arusha lakini mmeshawaambia kwamba sheria ya kuwemo kuja kuchunga hela zako lazima uwe na cheti cha *degree* ni sahihi kuchunga hela zako. Haiwezekani lazima wenzetu wa Benki Kuu waangalie kabisa, mbona nyie benki zenu ambazo zinaangaliwa na wasomi si nazo zinaongoza kwa ku-*collapse*, hazi *collapse* za wasomi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimeweza ku-*raise* hela sasa hawa wachimbaji wame-*raise* hela za Mheshimiwa Doto, wame-*raise* hela zao, halafu wewe hela ziko tayari unaniambia hauruhusiwi kukanyaga humu, sisi tutakuwa tunakula nyie mnatitizama kule, itawezekana kweli? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamuomba Mheshimiwa Waziri na Gavana walifikirie kwa mapana sana ili waruhusu watu waingie wenye hela zao, kwenye *board of directors* kwenda kuchunga pesa zao. Kwa hiyo, nitakuwa na hela kweli Mheshimiwa Lusinde nishindwe kusaini kujua kwamba huyu ni mwizi na huyu ni mtapeli hatarudisha hela, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, narudia tu kumpongeza Mheshimiwa Waziri nashukuru sana naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Profesa. Mheshimiwa Vuma, jiandae Mheshimiwa Leah, jiandae Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye Bajeti hii ya Fedha. Awali ya yote nikupongeze Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu na Naibu Waziri lakini pia na Kamishna wa Kodi, Ndugu yangu Kidata kwa sababu ya kazi kubwa ambayo mnafanya katika Taifa hili ya kukusanya kodi. Kimsingi iko wazi kwamba ni ngumu sana mkusanya kodi kuwa *popular* kwa hiyo, wakati mwingine mkipigwa mawe mvumilie tu, Taifa linajua kazi kubwa ambayo mnaifanya na tunatambua kwamba mmebebeshwa mzigo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nipende kuanza na suala la *microfinance*; suala la *microfinance* huko kwa wananchi ni tatizo kubwa sana. Nakumbuka kama miaka miwili iliyopita ilikuja sheria hapa tutarekebisha sheria ili kupunguza angalau makali, kuanzia kwenye riba ambayo *microfinance* wanachaji kwa wananchi lakini pia na *procedure* mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tatizo ni kubwa, wananchi bado wanachajiwa riba kubwa na *microfinance* lakini pia hata ile *procedure* yenyewe, wanaweza wakapunguza bei ya kiasi cha riba lakini ile *procedure* ambayo ni *application fee* ni gharama kubwa kuliko hata riba yenyewe. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri suala la *microfinance* tuendelee kulifanyia kazi, kwa sababu huko ndiko wananchi wetu wengi wanapata mikopo kwa ajili ya biashara lakini pia na shughuli mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilikuwa naangalia napitia bado tofauti kati ya bidhaa za kutoka nje hasa kwenye vinywaji, tofauti ya kodi kati ya bidhaa za kutoka nje na ndani ni ndogo sana. Hii bado naamini tunayo nafasi ya kufanya marekebisho kama ni kushusha kodi ya bidhaa za ndani au kupandisha ya nje, lengo ili tuweze kuwainda ipasavyo na kwa vitendo viwanda vya nchi yetu. Huwezi ukaweka tofauti labda ikawa ni 200 au 100 kwa lita halafu utegemee kwamba utapata matokeo ambayo ni mazuri sana, kwa hiyo, lazima hili liwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Nchi za wenzetu unakuta tofauti ni kubwa sana kiasi kwamba mtu akitaka kwenda kununua bidhaa ya nje kama ni kinywaji anafikiria mara mbili mara tatu kwa sababu bei inakua ni kubwa sana wakati mwingine inakuwa hata mara mbili ya kile cha nyumbani. Kwa hiyo, ni lazima tuliangalie tusiogope kufanya maamuzi kwa ajili ya kulinda viwanda vya ndani na ukiwabana sana hata hawa ambao wana viwanda nje hata vifaa tunapata kwa kodi kubwa wanakuja kujenga hapa hapa kwetu, wakija kujenga hapa maana yake sasa vijana wetu wanapata ajira, tunachukua kodi zaidi na tunapata wawekezaji kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Wizara ya Fedha pia kutokana na utaraibu wake wa usimamizi wa stempu za kodi zile za *ETS*. Utaratibu huu umeendelea kuongeza kodi, umeendelea kuongeza kodi kwa nchi yetu lakini pia umeendelea kutupa taarifa hasa za uzalishaji maana wakati wa zamani wakati tunatumia zile stempu ambazo sio za kieletroniki kulikuwa na tatizo kubwa sana. Ilikuwa ni ngumu kuweza kujua kwa sababu *forgery* ilikuwa ni kubwa, ilikuwa ni ngumu kuweza kujua hasa uzalishaji ni kiasi gani lakini pia hata kodi ilikuwa ni ngumu kuweza kukusanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mnafanya kazi nzuri sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hongera sana katika hili na usirudi nyuma wakati mwingine yanaweza yakaja manung'uniko yanaweza yakaja malamiko kwa sababu kama nilivyokuambia mkusanya kodi ni ngumu kuwa *popular*. Kwa hiyo, kanyaga na hata *vetting* mnayofanya kupata kampuni ambayo inafanya shughuli ile ya *SICPA,* mmefanya vizuri sana kwa sababu ni kampuni ambayo ukiangalia iko Dunia nzima. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hapa Kingu niko…

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mzuri sana unaotolewa na mchangiaji Kaka yangu Mheshimiwa Vuma, nilikuwa naomba nimpe taarifa kwamba pamoja na kwamba amesifia mpango mzuri wa stempu za eletroniki bado Serikali inaweza kuwa na nafasi ya kukaa na mzabuni wa *SICPA* kuona namna gani wanaweza wakapunguza bei, ambayo imekuwa

ikionekana kidogo kwamba imeonekana kwamba ni changamoto ili kusudi Serikali ikaingia *partnership* na huyu mwekezaji ili Serikali iwe sehemu ya kumiliki teknolojia hii…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kingu hiyo ni taarifa au unachangia.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, …na baada kuwasaidia Watanzania kupata teknolojia.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea taarifa kwa mikono miwili, kwa nini? Kwa sababu nataka niseme, kabla hatuajanza mfumo huu Serikali imepoteza mapato mengi sana na nashauri tusiiishie tu hapo kwenye stempu hizi, tusiishie kwenye bidhaa ambazo zinatozwa kodi, hata bidhaa ambazo hazitozwi kodi nashauri tubandike stempu hizi ili tuweze kujua takwimu halisi kwamba tuna zalisha kiasi gani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu usirudi nyuma kanyagia hapo hapo. Tunahitaji fedha kwa ajili ya maji majimboni, tunahitaji fedha kwa ajili ya vitu mbalimbali, tunahitaji fedha kwa ajili ya barabara vijijini. Endelea kukusanya kodi na hii kampuni kama alivyonipa taarifa Mheshimiwa Kingu ni vizuri tuendelee kushirikiana vizuri kwa sababu sio kila mtu anaweza kufanya kazi hii. Kuna kampuni chache ambazo zinaweza kufanya kazi hii. Kwa hiyo, tujitahidi tuwe makini, tusirudishe nyuma, kanyagia hapo hapo ili tuendelee kukusanya fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la Benki ya Kilimo, Benki ya Kilimo hapa tumeshashauri mara nyini sana. Benki ya Kilimo ina *stimulate* sana uchumi wa nchi hii, kwa sababu ndio Benki ambayo inamjali mkulima kuliko benki yoyote ile huo ndio ukweli. Tumesema mara kadhaa hapa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tunaomba sana benki hii fanya *consideration* ya kuiongezea mtaji ili iweze kufikia Watanzania wengi Zaidi. Wananchi wengi huko hawapati mikopo ya Benki ya Kilimo kwa sababu mtaji ina maana ni mdogo. Kwa hiyo, tunaomba sana jitahidi sana uipe kipaumbele benki hii ya Tanzania ili iweze kuwafikia Watanzania ambao ni wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilitaka kuzungumzia kuhusu maduka, utaratibu wa maduka ya kubadilisha fedha. Nadhani lazima tuangalie sheria ikoje inayo *govern* suala hili, kwa sababu utaratibu ni mgumu kiasi kwamba unalazimisha watu kufanya biashara hii katika namna ambayo sio halali. Yako maeneo hasa ya mpakani, maeneo ya mpakani hasa kama kule kwetu Kigoma na maeneo mengine, suala la kubadilisha dola ni suala la kila siku, watu wanatoka Congo, wanatoka Burundi, wanatoka Rwanda…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vuma kengele ya pili.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja.

**NAIBU SPIKA:** Muda wako mwingi umetumia kwenye stempu.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kw Amuda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Sekunde tano.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nishauri Serikali iweke utaratibu mzuri kwa kuruhusu biashara hii ifanyike vizuri waweze kupata kodi kupitia maduka ya kubadilishia fedha, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Komanya, jiandae Dkt. Kimei Charles

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kutoa maoni yangu kwa hoja iliyopo mbele yetu. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha lakini pamoja na maoni ya Kamati ya Bajeti ambayo ni mmoja wa Wajumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazofanya ikiwepo kurejesha nyongeza ya mshahara wa watumishi *annual increment* hii ni faraja kubwa kwa watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake na wataalam wote waliopo chini ya Wizara ya Fedha, kwa kweli kazi nzuri wanafanya katika kutekeleza majukumu yao lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kulipa madai ya watumishi na watumishi wanafurahi. Nimewauliza wakasema hawana changamoto zilizopo ni ndogo ndogo lakini kubwa kurudisha *on call allowance*, kwa sabbau tunatambua kwamba watumishi wetu ni wachache. Mtumishi mmoja wa afya anafanya kazi ya watumishi ambayo ingefanywa na watumishi watatu, hivyo kurudisha *on call allowance* ni faraja sana kwa watumishi wetu. Lakini nikupongeze kwa namna mnavyolipa madai ya wakandarasi, madai ya watumishi, kwa hiyo, hata uchumi wa Nchi unaendelea kuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru kwa Mheshimiwa Waziri katika majukumu ya Wizara ya fedha niongelee jukumu moja ambalo amelifanya vizuri na sisi wote tunaona kuhusu kuratibu upatikanaji wa fedha kutoka taasisi za fedha za kikanda na za kimataifa kwa ajili ya kutekeleza bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika katika miaka ya nyuma upelekaji wa fedha hususan fedha za maendeleo katika halmashauri za Serikali za mitaa ulikuwa chini kabisa. Hadi kumaliza mwaka ni asilimia 30 au 20 ya miradi ya maendeleo ndio iliyokuwa imepelekwa lakini sasa tumeona wote ni mashahidi na zaidi ya asilimia 90 na wengine kuvuka malengo na wengine kuletewa fedha ambazo hazikuwa kwenye mfumo wa bajeti ya halmashauri za wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru wengi tunaona wananchi wanaona miradi inatekelezwa katika halmashauri zetu kila kata ukienda, kila kata watumishi wako bize kutekeleza miradi ya maendeleo. Huu ni ushahidi tosha kabisa katika Wizara ya

Fedha kwa awamu hii upelekaji wa fedha katika ngazi za chini unaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mapato mengi yanatumika pia yanatumika pia mapato ya ndani. Nishukuru tunatumia fedha zetu wenyewe kupeleka kutokana na tozo mbalimbali lakini niipongeza *TRA* kwa mwezi Desemba ilivunja rekodi ya makusanyo ambayo ilikusanya trilioni 2.7 ambayo haijawahi kutokea. Niombe tuendelee kuwatia moyo watumishi wa *TRA* pamoja na Kamishna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee na niipongeze Serikali kwa kutumia mifumo yetu wenyewe iliyotengenezwa na wataalamu wetu. Kiupekee nimpongeze Mkurugenzi wa Mifumo wa TAMISEMI, nimpongeze Mkurugenzi wa Mifumo wa Hazina lakini niombe sasa, niishauri Serikali tuendelee kuwajengea uwezo, tuendelee kuwapa motisha ili waweze kufanya kazi vizuri, kwa sabbau wameokoa fedha nyingi za kigeni ambazo tulikua tunatumia kulipa mifumo iliyotengenezwa nje lakini mifumo hiyo inatengenezwa na wataalamu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sikuchangia TAMISEMI, naomba niongelee maboresho katika ukusanyaji wa mapato ya halmashauri kwa kuboresha Mfumo wa *LGRCIS* na kuupa jina la Tausi. Ni ukweli usiopingika katika mfumo uliokuwepo wa *POS* mapato ghafi mengi yalikuwa yanapotea kabla ya kufikishwa benki. Fedha nyingi zilikua zinakusanywa na kutumia kabla ya kufika benki na hivyo kupunguza mapato ya halmashauri husika. Lakini sasa kwa kutumia Mfumo wa Tausi niipongeze TAMISEMI kutakuwa na udhibiti wa mapato ghafi kwa kutumia matumizi ya zuio la kiwango katika ukusanyaji ambayo ni *float management*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ushauri wangu kwa kutumia mfumo huu wa *float management*, nina uhakika sasa ule wasiwasi uliokuwepo wa halmashauri kumpa wakala chanzo kwa kuhofu kwamba atakusanya mapato mengi yasifike halmashauri na yeye akanufaika. Sasa tatizo hili linaenda kutatuliwa na *float management* kwa kuwa wakala yule atatoa kwanza fedha

ambazo alitakiwa kulipa aikusanye, ikiisha anapewa nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika niiombe Serikali, niwaombe watumishi wetu waongeze umakini katika kutumia mfumo huu kwa sababu kwa kutumia *float management* sasa halmashauri inaweza ikafanya tathmini ya chanzo kimoja baada ya kingine. Niwaombe wakala anapofikia kile kiwango ambacho alitakiwa kulipa mwisho wa mwaka, basi tusifanye udanganyifu wa kukusanya mapato nje ya mfumo, tumuache akusanye mpaka mwisho wa mwaka na itatupa dira ya kiwango kwa kila chanzo kinachotakiwa kukusanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii itasaidia sasa kuondokana na tatizo lile la *underestimate* na niombe sasa niombe Serikali kwa kutumia mfumo huu basi ipo haja sasa baadaye watumishi wetu wajitoe katika kukusanya mapato ya halmashauri, tuwaachie mawakala kama mfumo huu utatumika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, jiande Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii ya mimi nihutubie pia Taifa kidogo. Kusema kweli wanahitaji pongezi nyingi uongozi wa Wizara lakini zaidi Mheshimiwa Rais ambaye amewezesha fedha kupatikana na Wizara zote zikapata fedha kwa uwiano uliokuwepo mzuri zaidi ya kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Komanya zaidi ya asilimia 80 Wizara zimepata mpata mpaka hadi Aprili ambaye ni ndugu yangu mzuri na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Nampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa kuweza kupangua wakurugenzi wa halmashauri zetu hiyo ni njia moja ya kupunguza maficho ya ufisadi. Kwa hiyo, nashukuru kwamba amefanya hilo naamini litasaidia na naamini kwamba Wizara nyingine hasa ile Wizara ya Ardhi itaanza na yenyewe

kutafuta namna ya kupangua maafisa ardhi kwenye mikoa na kwenye wilaya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme kidogo kwamba nashangaa Mheshimiwa Kishimba anapata wapi hizo hoja zake anaziibua kutoka wapi lakini nimefurahi hoja zake zimenifurahisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa vile Wizara imeweza kulipa madeni vizuri sana, karibu madeni yote yamelipwa kwa wakati ningeomba niseme kwamba kuna suala la madeni ya fidia, madeni ya fidia hayaonekani kwenye vitabu ni *contingency liabilities* lakini yapo hayo madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madeni kwa mfano kule kwangu Vunjo wakazi wa Eneo la Chekereni, Njia Panda ambako wanajenga kituo cha *one stop center ya customs* pamoja na kule Uchira toka mwaka 2013 wanadai zaidi ya bilioni 10 na hawajalipwa. kwa hiyo, naona niwa-*dominate* Waziri alichukue na hilo najua kwamba siku ya karibuni walifanya tathmini upya na naamini zile dhamana zilizokuwa zimepatikana miaka ile wataongezewa fidia yao inavyostahili kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, langu la pili linahusu vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Fedha na vingine vipo chini ya Wizara ya Biashara, vyuo ambavyo viliundwa kwa mantiki ya kutengeneza au kutoa *skills* kwa waliomaliza shule ili waweze kuingia kwenye kazi moja kwa moja. Kwa mfano *IFM* tulijua kwamba ilikuwa *diploma, advanced diploma* na *post graduate diploma* na zingine zilikuwa hivyo hata Mzumbe lakini baadaye hata *CBE* nayo ilianza sasa kuwa kama *university* lakini mantiki yake ilikuwa ni vyuo vya kati ambavyo vitataengeneza watu wenye *study* kwenye fani husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wamebadilisha kabisa hiyo dira iliyokuwepo toka mwanzo na wameingia sasa kuwa ni vyuo vikuu na kwa bahati mbaya na kwa sababu hiyo utaona kwamba pia hivi vyuo havi-*publish* nyaraka ambazo za kitafiti ambazo zinaongeza nanii duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nafikiri hivi vyuo haviko mahali pake. Kwa sababu sasa tumeshabadilisha ile dira tunafikiri vyuo hivi virudi kwenye Wizara ya Elimu ivisimamie kama inavyosimamia vyuo vile vingine vyote, lakini kukaa kwenye Wizara hizi havipati usimamizi unaostahili na ninaamini ndiyo sababu tunaona hata kwenye vyuo elimu inaporomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nizungumze suala la Kitengo cha Mkaguzi Mkuu lakini naona limeshazungumziwa vya kutosha. Lakini kuna hoja pia zingine nitazungumza; hoja ya kwamba tutenge fungu la *contingency* la dharura kwenye bajeti (Mfuko wa Dharura kwenye Bajeti). Ni jambo ambalo liko kwenye *constitution* kwenye katiba na pia ni hitaji la Sheria ya Bajeti. Hatujaweza kufanya vile na mimi nasema kwamba silaumu na mimi nina hoja yangu binafsi, nasema ukianza kutenga fedha kwenye Mfuko wa Dharura unaweka akiba kwa tatizo litakalokuja na unaweza kufanya vile kama una bajeti ambayo haina nakisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti zote tangu tupate uhuru zimekuwa ni bajeti ambazo zina nakisi kubwa ndiyo sababu tunakwenda kukopa na kuomba wahisani na kadhalika. Endapo tutasema tunatengeneza mfuko wa dharura ukienda kwa mhisani atakwambia kwamba kula kwanza uliyoweka akiba ndipo nikupe mimi; kwa hiyo hatakupa na misaada itapungua na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naamini hapo tutakapofikia uwezo wa kuwa na bajeti ambayo ni *surplus budget* basi tunaweza kuzungumzia suala zima la kuweza kuweka fedha kwenye mfuko wa dharura ambao unahitajika bahati nzuri sasa hivi tunajua kwamba unatenga shilingi bilioni 100 ambazo zinaweza zikatumika wakati wowote, lakini sheria inataka mfuko kamili ambao utakuwa unakuzwa na wenyewe uwe na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza sana kwamba tumeanza kutengeneza dira ya 2050. Ninaamini ni jambo jema lakini mimi nilikuwa nafikiri huwezi kutengeneza dira kabla hujafanya tathmini ya ulikotoka, ulipo ndipo uweze kusema ninaenda wapi. Naona kwamba hatujaweza kufanya hiyo

tathmini. Tunaambiwa tathmini imeanza kufanyiwa kazi lakini nilishangaa kwamba tumeweza kufungua. *Of course,* tulizindua mchakato huu wa kutengeneza hii dira lakini bahati mbaya naona kama itakuwa siyo vizuri kama hatujapata tathmini nzuri au hata wale waliopewa kuifanya hiyo kazi watafutiwe kwa upesi sana tathmini hiyo ikamilike ili waweze kutumia na kuelewa ni wapi tumetoka na tumejifunza nini kutokana na utekelezaji wa dira ya 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka pia niseme kwamba mimi naunga hoja mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza na mimi niungane na wengine kukupongeza Mheshimiwa Waziri na msaidizi wako kwa hotuba nzuri lakini kipekee kama Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo nisimame hapa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tukio kubwa na la kihistoria linaloendelea Mkoa wa Njombe. Kwa ulipwaji wa fidia uliozinduliwa leo kwenye miradi ya Liganga na Mchuchuma, kama kamati tunafarijika na hasa mimi ambaye nimekuwa kinara wa jambo hili ninapoona hatua hii kubwa ya ku-*inject* shilingi bilioni 15 kwa ajili ya wananchi maana yake tunaona mradi mkubwa wa kimkakati wa kulinyanyua Taifa hili wa uchimbaji wa chuma Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma sasa unaenda kufanya kazi. Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia upande wangu mimi wa kuchangia, kama nilivyosema mimi ni Mjumbe wa Kamati na kwenye kamati yetu tangu tumefika kumekuwa na habari ya zile risiti za *electronic* au ambazo zimekuwa zinafanywa na Kampuni ya *SICPA*. Sasa nilikuwa naomba nijielekeze hapa kwenye habari ya risiti za *ETS* ili walau na mimi niweze kupata nafasi ya kuchangia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wametufuata sana kwenye Kamati nadhani tangu miaka hii miwili yote iliyopita

na hata juzi walikuwa hapa wanaendelea na jambo hili. Hili Bunge ni la wananchi, wafanyabiashara kila wanapohisi kwamba wanahitaji msaada wamekuwa wanakimbilia katika Bunge. Sasa mimi kama mjumbe tumekaa miaka yote hii lakini bado hatujapata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikawa nimekuja leo, naomba nitoe ushauri tu kwa Waziri wa Fedha, nadhani anakumbuka vikao tulishafanya mpaka Kamati ya Uongozi wa Bunge na wewe mwenyewe ukiwemo, maofisa wa *TRA;* wafanyabiashara wanayo hoja na hoja ambayo lazima isikilizwe. Hii ni kwa sababu hawa ndiyo wanaolipa kodi, ni wazalishaji wakubwa wameajiri Watanzania. Kwa hiyo hatuwezi kuendelea kufanya nao bisahara huku wakiwa wana sononeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, *point* yao kubwa ni kwamba gharama ziko juu sana ukilinganisha na nchi nyingine; na wao wanasema mwanzo walivyoanza zilikuwa kampuni karibu tisa na huyu muwekezaji akasema amewekeza mtaji. Kwa hiyo angetakiwa ku-*recuperate* ile *capital* yake ambayo ameweka na akawa anawachaji juu akitegemea kwamba baada ya muda ingeshuka. Sasa kutoka kampuni tisa zilizoanza sasa tuna kampuni zaidi ya 200 sasa. Kwa hiyo wafanyabiashara wanahisi zile gharama inabidi zishuke ili na wao waweze kuji-*tune* na wafanye biashara katika unafuu zaidi waweze kuajiri Watanzania wengi na kupanua wigo wa biashara zao; nadhani ameongelea Mheshimiwa Vuma hapo

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu jambo moja Mheshimiwa Waziri. Tumeliongea sana kwenye kamati hili lione. Ongea na mwekezaji huyo aliyepo ambaye anafanya kazi hii ili ashushe gharama hizi ili kwa pamoja wafanyabiashara pia waweze kuridhika. Na kwa sababu wao wamekuwa wanakuja kwenye Kamati na wewe hujawahi kukaa nao, sasa, andaa kikao awepo mzabuni, wawepo wafanyabiashara na wewe mwenyewe ikiwezekana na Kamati tukae hili jambo tujadili kwa pamoja. Kwa sababu haiwezekani tukawa tunafanya biashara na watu ambao wana lalamika. Mwwekezaji kawekeza mtaji wake na hivyo ni lazima tujue amewekeza fedha lakini aone pia jinsi ya kupunguza ili iwe *justifiable* kwa sababu hiki kitu watu wanaona.

Dunia ni kijiji, wewe mwenyewe katika bajeti hii ulituhubiria kwamba tutaenda kufanya biashara yaani tutaendesha Serikali kidijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo leo kila kitu kiko wazi. Kila kinachofanyika sehemu yoyote kiko wazi watu wanaona. Kwa hiyo tuombe hili ulichukue wafanyabiashara wakapatiwe unafuu ili waweze kufaidika na kile kidogo wanachokizalisha na Watanzania waweze kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikitoka kwenye habari ya *SICPA* au kwenye stempu hizi za *ETS,* mimi ni mjumbe kama nilivyosema, kilimo kiko kwetu. Mheshimiwa Waziri mme-*inject* fedha nyingi sana kwenye Mradi wa *BBT,* nyote ni mashahidi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa *project* hiyo ambayo inaenda kuinua vijana na wakina mama; lakini iko habari ya Benki yetu ya Kilimo *(Tanzania Agricultural Development Bank)*. Hii benki kwenye Azimio la Bunge la mwaka jana mwezi Novemba kwenye Ripoti ya *PAC* walisema kabisa kwamba benki ilipewa mtaji wa bilioni 208 na kukawa na ahadi ya Serikali kuiongezea mtaji mpaka ifike shilingi bilioni 760 lakini hatujapata ripoti kujua kazi hii ilifanywa vipi na *so far* mmeongeza nini na mwaka wa fedha unaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunachoomba ahadi ilikuwa kufikisha mtaji wa benki hii iwe shilingi bilioni 760. Mheshimiwa Waziri hatuwezi…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa.

## TAARIFA

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji Serikali ingeipa Benki ya *TADB* bilioni 100 ingelikuwa na mtaji wa zaidi ya shilingi bilioni 760, ingewakopesha wakulima wengi, ingekopesha vyama vya

ushirika vingi na ingeleta mapinduzi makubwa kwenye hii sekta ya kilimo nchini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ezra taarifa?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa naipokea na ndipo hapo nilikuwa naendelea; kwamba maelekezo au Azimio la Bunge tuwe tunatoa shilingi bilioni 100 kila mwaka. Kwahiyo tunachoomba azimio lile ambalo Bunge lako lilipitisha mwaka jana Novemba hebu liweze kufanyiwa kazi. Kwa sababu kwa sisi tunaotoka vijijini siyo kila mtu yuko kwenye *BBT,* wala siyo kila mtu anaweza kukopesheka benki, wengine hawana dhamana kwenye benki za biashara. Benki yetu hii riba ni ndogo, asilimia tisa hadi asilimia kumi na mbili, si kila benki inaweza kutoa hivyo. Kwa hiyo tunachoomba mtaji uongezwe ili wakulima wetu huko vijijini waweze kupata nafasi ya kuweza kushiriki uchumi na hasa fedha hizi ambazo Mama Samia anazitoa sehemu nyingi na anavyozidi kuifungua nchi kiuchumi hata sisi huko vijijini waweze kushiriki kufanya uchumi wa nchi hii hatimaye waweze kupata maendeleo; niliombe hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha najua mikopo ile ya asilimia 10 imesitishwa. Niombe kwenye hili, kipindi mnajaribu kuangalia kanuni na ukopeshaji mpya, kundi la vijana ni kundi linalokua. Unapoweka kijana wa miaka 35, *these guys are still teenagers.* Walio wengi hawajajua hata thamani ya ile fedha, mnawapa hii fedha baadaye wanaanza kusumbuana na halmashauri. Ongezeni umri *at least* miaka 45 na wenyewe bado ni vijana. Waende huko wapewe watu ambao kidogo wako *matured* hizi fedha watazipata watafanyia biashara, watawaajiri wale vijana wenye miaka 18, 20 waweze kufanya nao kazi huku fedha iki-*rotate* na kurudi; kuliko leo ambavyo unampa fedha mtu kijana wa miaka 18 au 25 haendi, hajui aitumiaje. Lakini kwa sababu ameambiwa fedha ipo anachukua na hatimaye anashindwa kuirejesha na thamani ya ile fedha inashindwa kuonekana…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIK:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha ubunifu wa ukusanyaji mapato na usimamizi mzuri wa matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa miradi ya kimkakati na pia utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miezi kumi, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imesimamia kwa ufanisi ukusanyaji mapato na utekelezaji wa miradi mingi ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na kaadhalika. Napongeza Serikali kwa mwendelezo mzuri wa utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa umeme Mto Rufiji, Mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uboreshaji wa bandari utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. Umeme, reli na bandari ni nguzo imara ya kiushindani katika uchumi wa

Tanzania na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki wakati dunia inapambana na athari za vita vya Urusi na Ukraine na pia janga la *corona virus (covid-19),* tumejifunza umuhimu wa kuwepo kwa mikakati mbadala kutokana na nchi nyingi tunazoshirikiana kibiashara na kiuchumi kukumbwa na mtikisiko wa kiuchumi. Biashara zilizoathirika kwa kiasi kikubwa ni za usafirishaji hasa wa anga uliathirika sana na napongeza mkakati wa shirika la ndege kwa utendaji wenye tija na hata kununua ndege mpya ya mizigo na kujipanga kuanza kutumia ndege zake kusafirisha mizigo. Mkakati huu ambao umetumiwa na hata mashirika makubwa ya ndege duniani, utawezesha usafirishaji wa mazao yetu ya kilimo kufikia masoko kirahisi na hapo hapo uhakika wa mapato kwa shirika la ndege hasa kipindi hiki kukiwa na uhutaji mkubwa wa usafirishaji mizigo kwa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Msajili wa Hazina anapaswa kuendelea kuimarisha mitaji kwa mashirika ambayo yatachochea ukuaji wa uchumi ikiwemo Benki za *TADB, TCB, TIB* na *ATCL* ili iweze kusimama kibiashara ikiwa ni nguzo muhimu hata kwa sekta zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa kurudisha Tume ya Mipango na hata maboresho ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Tume ya Mipango ni nguzo muhimu katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu hasa katika kipindi hiki tunapotekeleza miradi mingi ya kimkakati. Upangaji na utekelezaji wa miradi unahitaji kuwa na chombo madhubuti kinachoweza simamia miradi kitaifa badala ya kusimamiwa kisekta. Msajili wa Hazina anapaswa kupewa nguvu zaidi ili asimamie mashirika ya umma ili yaendeshwe kibiashara na kwa tija ya kiushindani kwa hapa nchini na hata nje ya nchi. Kuongezeka kwa tija kwenye mashirika ya kibiashara itapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa mapato ya kikodi na hata mikopo kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea hata kwa kutafuta vyanzo mbadala vya fedha kugharamia ujenzi huo, kwa vile kutakuwa na fursa kubwa

za usafirishaji. Pamoja na ujenzi wa *SGR,* napendekeza kuendelea na kuboresha reli ya *TAZARA* na uboreshaji wa bandari zetu ikiwemo ujenzi wa bandari kavu ikiwemo ya Inyala, Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki ili kupunguza gharama za kusafirisha pembejeo na mazao. Serikali ichukue hatua za haraka kuinusuru reli ya *TAZARA* hata ikibidi kurekebisha mikataba ya umiliki na uongozi ili mradi iendeshwe kwa tija. Kuna umuhimu mkubwa kuchukua hatua za makusudi kwa kutumia zaidi *TAZARA* kusafirisha mizigo ambayo imeelemea hata uwezo wa barabara zetu. Usafirishaji wa mizigo kwa kutumia *TAZARA* ilenge kupunguza gharama za usafirishaji mizigo kwa wateja wa bandari kutoka Zambia, DRC, Malawi na hata kwa kupunguza gharama za usafirishaji wa pembejeo kwa wakulima na wakati huo kupunguza gharama za kusafirisha mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iwekeze angalau shilingi bilioni 200 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya kuboresha mindombinu ya reli na karakana. Uwekezaji huu utawezesha *TAZARA* kujiendesha kwa faida na hata kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipa zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa mwaka ikiwa ni mishahara ya wafanyakazi wa *TAZARA*. Uwekezaji huu unahitajika haraka wakati Serikali za Tanzania na Zambia zinaendelea na jitihada za kurekebisha mikataba ikiwemo wa uendeshaji wa *TAZARA*. Pamoja na kuboresha *TAZARA*, napendekeza kukamilisha taratibu za ujenzi wa Bandari Kavu ya Inyala, Mbeya ambapo Mamlaka ya Bandari kwa kipindi kirefu wamewahakishia wananchi kulipa fidia ya eneo lao wanalolichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fursa nyingi za muda mfupi za kuongeza mapato kupitia hatua za kiutawala ikiwemo ya kuondokana na matumizi na malipo ambayo hayana tija kwa Serikali na hata walipakodi. Kutokana na mahitaji makubwa ya uwekezaji kwenye miradi ya kimkakati, uchumi wetu utaendelea kuwa na mahitaji makubwa ya mikopo ya pesa za kigeni na wakati huo huo kulipa mikopo iliyoiva. Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha mapato ya fedha za kigeni yanaongezeka kupitia mazao ya kilimo, madini na utalii. Kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yatasaidia kuimarisha uhimilivu wa deni la Taifa na

pia kuendeleza utulivu wa shilingi yetu dhidi ya sarafu kuu za kigeni na hata kuhakikisha utulivu wa mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe kipaumbele cha kuwekeza kwenye kilimo ikiwemo pembejeo na umwagiliaji kwa lengo la kuongeza tija na pia kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kulinda mfumuko wa bei. Serikali inashauriwa kuchukua hatua zaidi za kuimarisha sekta za kilimo, utalii, na madini ili kukabiliana na athari za kiuchumi wa kidunia. Kutokana na athari za kiuchumi uliokumba dunia nzima ikiwemo changamoto za upatikanaji wa fedha za kigeni, hatua za kuimarisha sekta hizo hapo juu, inaweza kuwa fursa kwa Serikali kuvutia uwekezaji zaidi kwenye madini hasa dhahabu, viwanda vya mbolea kutokana uwepo wa malighafi za madini ya *calcium carbonate, lime* na *phosphate*. Dhahabu ina historia ya bei kutoyumba kwenye soko la dunia kwa vile mabenki yanatumia dhahabu kwenye kuwekeza na kutokana pia na kuyumba kwa thamani ya shillingi na hata dola ya Marekani, Serikali inaweza kutumia dhahabu kama mbadala wa kuwekeza amana zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi kidunia, Benki Kuu nyingi duniani zimeanza kuwekeza zaidi kwenye dhahabu na hii ni ishara nzuri kwa bei ya dhahabu kuendelea kuimarika kwenye soko la dunia ambapo kwa mwezi Aprili, 2023 bei zaidi ya asilimia 11 ukilinganisha na bei za Desemba, 2022. Serikali ijielekeze kununua dhahabu kwa shilingi toka kwa wachimbaji wadogo na kisha kuzitafutia soko la kigeni la moja kwa moja na hatua hii itapunguza na kuzuia uvujaji wa mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya Niobium ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha Ferroniobium (FeNb) ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani

hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya Niobium ambayo inapatikana Milima ya Pandahill Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya Ferroniobium (FeNb *end product)* yanaendelea kuwa makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahitaji kujiwekekea mikakati ya haraka *(quick wins)* ili kuhakikisha inaimarisha uchumi ikiwemo kuboresha urari wa biashara kukabiliana na athari za *Covid-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa Niobium na Kiwanda cha Ferroniobium, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo na ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka ni shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(modern manufacturing plant and smelter)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itakuwa itachangia huduma za kijamii *(Corporate Social Investment in Community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upotevu mkubwa wa fedha za Serikali ikiwemo miradi ya Serikali Kuu na Halmashauri, napendekeza Serikali kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kuongeza ufanisi na uhuru wa Wakaguzi wa Ndani. Serikali ihakikishe Mkaguzi wa Ndani wakati wote anakuwa huru kutoka kwa Afisa Masuuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri wasimamiwe na Mkaguzi Mkuu wa Mkoa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Serikali iimarishe uhuru wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani *(Internal Auditor General)* na napongeza Serikali

kupandisha hadhi ya Ofisi kuwa na Fungu la Bajeti linalojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb) na Naibu wake Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Katibu Mkuu Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Naibu Makatibu Wakuu Lawrence Mafuru, Jenifa Omolo na Amina Shaaban na wataalamu wa Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na wadau wa maendeleo wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya katika sekta ya fedha na uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni ulizuka mzozo kati ya wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo na Serikali ambapo wafanyabiashara walifunga biashara zao kwa takribani siku mbili. Mambo makubwa waliyolalamikia wafanyabiashara wa soko hili ni usajili wa *store* zao za mizigo wasioutaka, tuhuma za rushwa kwa watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* wasio waaminifu, kamatakamata na kunyanyaswa na kikosi kazi *(Task Force)* cha *TRA*, viwango vikubwa vya makadirio ya kodi na utitiri wa kodi. Mpaka wafanyabiashara walipogoma, walijihisi kuwa Serikali iliwakamua sana na walikuwa na hofu ya kumaliza mitaji yao na biashara zao kufilisika kwani wakusanya kodi na ushuru walikuwa wanachukua zaidi ya kile walichokuwa wanazalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa busara zake na kuutatua huu mgogoro kisiasa. Soko la Kariakoo linahudumia wafanyabiashara kutoka mikoa yote Tanzania na nchi za nje kama Demokrasia ya Watu wa Congo (DRC), Burundi, Malawi, Zambia, Rwanda na Uganda likiwa linaendeshwa na wafanyabiashara wakubwa, wadogo na wachuuzi. Wote hawa huliingizia Taifa letu kipato cha kutosha. Inakadiriwa kwamba soko la Kariakoo linaweza kuiingizia Serikali mpaka zaidi ya shilingi bilioni 10 kwa mwezi kama malipo ya kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la Kariakoo likitetereka, matokeo yake ni mabaya kwani kwani litaathiri biashara nchi nzima na nchi za jirani ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato hapa nchini. Kutokana na umuhimu wa soko hili kwa uchumi wa Taifa letu, ni vyema Serikali ikajipanga na kukwepesha mgogoro wa aina yoyote ule na hiki chanzo kikubwa cha mapato. Tujikumbushe kwamba ni mara ya kwanza toka tupate uhuru kuona tukio baya la mgomo katika soko letu la Kariakoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu mkubwa wa kuipa moyo na kuisaidia hii sekta binafsi ili waendeshe shughuli zao wakiwa na utulivu. Wakikatishwa tamaa na kuziacha biashara zao, madhara yake yatakuwa makubwa kwa Taifa letu. Kutokana na fundisho tulilolipata huko Kariakoo, naishauri Serikali ipeleke Bungeni sheria zinazolalamikiwa na wafanyabiashara na kuzifanyia marekebisho ili ukusanyaji ufanyike kwa kutumia sheria na kanuni rafiki za kikodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, ni vyema kupitia upya na kuangalia baadhi ya vipengele vya Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Tozo za Huduma ya Bandari, Sheria ya Magari (kodi katika usajili na kuhamisha umiliki), Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sheria ya Forodha (Usimamizi na Ushuru) Sheria ya Rufaa ya Mapato ya Kodi, Sheria ya Serikali za Mitaa (Ukadiriaji) na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Waziri akaja na mapendekezo yake katika kipindi hiki cha bajeti ili kuhakikisha Serikali inazikabili changamoto za kibiashara kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, napendekeza utafiti unaofanywa na Wizara uwe endelevu na ulenge kuibua fursa mpya za mapato ya kodi na yasiyo ya kikodi ili kuongeza wigo wa walipakodi na kuondokana na kuwategemea walipakodi wachache kuiendesha nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa 1.3.1. Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2022, Uchumi wa Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji chanya wa uchumi ulichangiwa na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Ukraine na Urusi; ruzuku kwenye mafuta shilingi milioni 100 kila mwezi, uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati (trilioni 6.55 limefika 86.89%), maji (trilioni 1), afya (trilioni 1), elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe na kuongezeka kwa mikopo katika sekta binafsi ambayo imechochea shughuli za kiuchumi.

Aidha, ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa shughuli za utalii kutokana na kampeni ya *Royal Tour*. Ukuaji huu wa uchumi unaashiria kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika sekta mbalimbali pamoja na kuongezeka kwa ajira na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo matatu ambayo yatasababisha Watanzania kuhamisha uwanja wa vita; kwanza *Bureau De Change - BoT*/masharti ya kuanzisha *Bureau De Change* yawe rahisi ili kurahisisha upatikanaji wa dola nchini na kukuza utalii; pili, madeni ya kodi za muda mrefu - *TRA* lifanyiwe kazi; tatu, gawio kwa Watanzania kwenye makampuni ya hisa-kama Vodacom wafuatiliwe ili wawe wanatoa gawio.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraka ya Kamishna ni makubwa mno kiasi cha kukiuka haki za binadamu na baadhi ya sheria hasa Kamishna akiwa *negative thinker*.

Mheshimiwa Naibu Spika, machinga wa Iringa waliahidiwa na Rais fedha zao shilingi milioni 700; tunaomba Wizara ya Fedha itoe.

Kuhusu utoaji maamuzi chanya kwa viongozi wa juu wa taasisi unazoziongoza uko chini sana, wawe wanatoa maamuzi

mapema na kwa wakati ili kuepusha migogoro kama migomo na kufifisha uzalishaji kwa wananchi; kupuuza maagizo ya viongozi ikiwemo Mheshimiwa Rais, mfano kutotoza kodi za miaka ya nyuma na ya muda mrefu, kutorudisha fedha za *Bureau De Change* na kusingizia Bunge na vyombo vingine vya sheria waache. Wawajibike! Nia ovu isiwepo kama ku-*seize* fedha za *Community Banks* kama *Mucoba bank* milioni 600, ni kutowatendea haki wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika mjadala huu. Awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi ambaye ametuwezesha kubakia hapa leo na kujadili bajeti ya Mapato ya Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuwepo katika Wizara hii ya Fedha na Mipango. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana wote sisi hapa ni mashahidi. Uwezo wake mkubwa sana wa kutafsiri sera kutoka kwenye makaratasi na kuja kwenye vitendo. Wote ni mashahidi na mwenye macho haambiwi tazama. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na tuna muomba Mheshimiwa Rais aendelee kuchapa kazi. Haya maneno ambayo baadhi labda yanaweza kutokea tokea na watu kukosoa kosoa basi ndiyo ada ya binadamu kuzungumza, ndiyo ada ya binadamu kuzungumza… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimwa Wabunge, naongeza nusu saa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo ada ya binadamu kusema. Hata wahenga husema, "*Mwenda hidimani ndiye mkosa.*" Unapokuwa unafanya kazi vizuri basi lazima kutatokea maelekezo kwa nia safi tu na kukosoa kosoa. Na mfano wa hili pengine labda inawezekana wengine nimewaacha kwamba mwenda hidimani ndiye mkosa ni pale kwa mfano upande wa michezo anaweza kusema hapa

Mheshimiwa Waziri kwamba pale Mayele bora angepiga shuti badala ya kutoa pasi, lakini kwa kuwa amefanya kazi nzuri ndiyo amepata kukosoa lile. Lakini mwingine anaweza kusema Chama alikuwa asitoe pasi badala yake apige. Kwa hiyo ndiyo mwenda hidimani ndiye mkosa. Tuendelee kufanya kazi na ninaamini kabisa mafanikio ya kazi hii itapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwapongeze sana na kuwashukuru sana Kamati ya Bajeti, kuanzia Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, ninawapongeza sana na ninawashukuru sana. Kamati ya Bajeti wanafanya kazi nzuri na kubwa sana ya kiuzalendo. Na kwa ushahidi wa hilo Kamati ya Bajeti inakosa hata muda wa kailula, muda wote wao wapo kazini ni kwa sababu ya uzalendo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa namna wanavyotupa ushirikiano mkubwa sana. Lakini si kwa umuhimu, naomba nimpongeze sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, kwa kiasi kikubwa anatupa maelekezo na kunishauri vizuri. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye hoja kwa maslahi ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hoja ya Mheshimiwa Kilumbe. Mheshimiwa Kilumbe amezungumzia kwamba asilimia 70 ya fedha zilizopo Tanzania ziko mikononi kwa watu na haziko katika mifumo rasmi ya kifedha zikiwemo benki na ametoa pendekezo kabisa kwamba kwa kuwa suala hili lipo basi Wizara ya Fedha ichukue majukumu au jukumu lake la kutoa elimu. Ninacho mhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Fedha inatoa elimu siku hadi siku kupitia vyombo vya habari vyote nchini lakini hata kwa mtu mmoja mmoja. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kuchukua fursa hii ya kutoa taaluma kwa wananchi wetu kuwahimiza na kuwashajiisha waweke fedha zao katika mikono salama ambazo ni benki zetu na mifumo rasmi ya kifedha au ya sekta ya fedha ambazo zipo. Huko kwenye benki zetu kuweka fedha ni salama zaidi kuliko kuziweka kwenye nyumba zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nijielekeze kwenye hoja ya ndugu yangu kaka yangu Mheshimiwa Hassan King. Hoja ya kwanza mahususi amesema kwamba watumishi wazee wetu ambao wamestaafu kwa bahati mbaya sana wanachelewa kupewa fedha yao ambayo ni haki yao ya msingi. Mimi nimhakikishie Mheshimiwa kwamba suala hili tumelichukua na tunaenda kulifanyia kazi. Lakini nimuombe tu ile hoja mahususi ya watu mahususi ambao amewataja pale naomba tukimaliza tu hii bajeti basi tuonane anikabidhi yale majina. Nimhakikishie kabisa, mimi niko na Mheshimiwa Waziri, tutayafanyia kazi haraka iwezekanavyo. Kwa sababu amenitisha kidogo ametumia msamiati mkubwa sana kwamba wazee hawa wanadhulumiwa. Na jambo ambalo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linamkosesha raha na kumnyima usingizi ni suala la…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Mtoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili kuweza kuhitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa hoja ambazo wamezitoa na nianzie ufafanuzi wangu kwenye eneo hilo la jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili na Watanzania wajue, leo hii tunayoijadili ni Wizara ya Fedha, Bajeti ya Serikali itakuja wiki ijayo. Kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge tumepokea hoja zote, na waridhie zile zinazoangukia kwenye hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali, kwa sababu matayarisho yake bado yanakamilika kamilika zikiwepo zile za hatua za kikodi, waridhie kwamba tumezipokea na tutakuwa na mjadala mpana tutakapokuwa tumewasilisha yale ambayo tumeyaweka maoni yao na yale ambayo watatamani tuyabadilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo yale masuala yote ambayo yamejitokeza yanayohusisha masuala ya kikodi niwaombe waridhie kwamba tutayajadili kwa upana baada ya kuwa tumeshawasilisha kile ambacho tumekiandaa katika kauli ya Serikali, ambayo tutaiotoa tarehe 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, pia kwa manufaa ya ufafanuzi ili na wananchi waelewe; bajeti ya maendeleo ambayo tunaiongelea kwenye muktadha huu hapa ni bajeti ya maendeleo kwa Wizara ya Fedha na taasisi zake. Huwa inatokea tukisema bajeti ya kawaida ni mathalan hapa shilingi trilioni 15, wanatokea wengine wanasema bajeti ya maendeleo ni kidogo, kama hivi iko shilingi bilioni karibu 500, inazidiwa na bajeti ya matumizi ya kawaida. Kwa leo hii hapa tunapoongea bajeti ya matumizi ya kawaida ndani yake ina takribani shilingi trilioni 10 ambazo zinaangukuia kwenye Deni la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa kama tulivyotoa kwenye ufafanuzi wa majukumu ya Wizara linasimamiwa na Wizara ya Fedha. Kwa hiyo tuna trilioni 10 ambazo zenyewe ni Deni la Taifa kwa mwaka, na bilioni 500 wanayoiona hiyo ni bajeti ya maendeleo kwa Wizara ya Fedha na taasisi zake. Bajeti ya Maendeleo ya Nchi nzima tutaitaja tutakapotoa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Deni la Taifa wanaloliona, hizo shilingi trilioni ni Deni la Taifa kuanzia awamu ya kwanza. Awamu ya kwanza, awamu ya pili, awamu ya tatu, awamu ya nne, awamu ya tano na kwa awamu ya sita kwa mikopo hii ya *roll over* pamoja na ya ndani kwa sababu za mikopo ya nje bado hazijaiva ndiyo inayoleta jumla ya deni la hilo la shilingi trilioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha pia ndani yake pia kuna Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambapo na yenyewe fungu lake tunaliomba pamoja na mafungu haya mengine, na tuna ofisi zingine kama tulivyoziorodhesha wakati wa kuwasilisha taarifa hii rasmi ya leo. Kwa hiyo uwiano ule wa fedha za matumizi ya Kawaida kuwa kubwa na uwiano wa matumizi ya maendeleo kuwa ndogo ni kwa sababu matumizi ya kawaida yanahusisha Deni la Taifa ambalo ni la awamu zote. Na matumizi ya maendeleo namba yake ni ndogo kwa sababu tu inahusisha

matumizi ya Wizara ya Fedha na taasisi zake na matumizi ya maendeleo ya jumla yatakuja kwenye Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri wa kamati, na maeneo yale kama nilivyosema mengine yamejikita kwenye sera za masuala ya kikodi kwa hiyo tutatoa tamko tutakapokuja wakati wa tamko la Bajeti ya Serikali. Tumepokea hoja kubwa ambayo imejadiliwa kwa mapana na Wabunge wengi kuhusu ukaguzi wa ndani. Wabunge watakumbuka mwaka jana walitupitishia mabadiliko ya kimuundo ya Ofisi ya Ukaguzi wa Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichokuwa kinatokea kabla ya huo muundo wa mwaka jana ambao tulipitishiwa mapendekezo na Bunge, Wakaguzi wengi wa Ndani walikuwa ni sehemu ya *management*. Kwa sababu Fungu lao, *vote* yao ilikuwa inaangukia kwa wale wanaowasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia mwaka jana tulibadilishiwa muundo, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani ilipewa *vote* yake na mtiririko wake. Sasa baada ya Bunge kupitisha, ilienda kwenye hatua za kutengeneza muundo wake ambao wanaweza wakaona labda haijaweza kuwa na kiwango kikubwa. Kwa sababu ndiyo kwanza mwaka huu ambao tumeumaliza ndiyo tumepata ridhaa ya Bunge baada ya kupitishiwa mapendekezo na tukaenda kwenye kutengeneza muundo na muundo ambao umefanyiwa kazi ni kwamba taarifa zote zile sasa hazitakuwa zinapelekwa kwa yule anayekaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilivyokuwa mwanzo ilikuwa ukimkagua yule unayemkagua ndiyo unampatia ile taarifa ya ukaguzi, lakini kwa sasa watatoa ushauri kwa wale wanaofanya nao kazi. Kama ni halmashauri watatoa ushauri kwa Mkurugenzi, kama ni ofisi yeyote ile watoa ushauri kwa mkurugenzi. Lakini taarifa itaenda kwenye ofisi ya juu ya yule aliyekaguliwa, za halmashauri zinaenda mkoani na siyo kwa Mkaguzi Mkuu wa upande wa mkoa lakini ni kwa mkoani kwa maana kama Mbunge alivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa zile ambazo zinakwenda juu kwa maana ya ngazi ya Taifa, tulizipeleka ziende kwa Mkaguzi

Mkuu wa Taifa ili baadaye yeye ndiye anayehusika kwenda kuwasilisha kwa Kamati ya Baraza la Mawaziri la kazi, ambalo linaongozwa na Waziri Mkuu ambaye ndiyo *coordinator* wa Shughuli za Serikali. Hapo ndipo ambapo tuliona yule Mkaguzi Mkuu wa Ndani anatakiwa aende kuziwasilisha. Hii tumeiweka pale kwa sababu tuna taarifa za halmashauri, tuna taarifa za *local government,* tuna taarifa za Serikali Kuu na tuna taarifa za Mashirika ya Umma, kama ambavyo zinaweza kuwasilishwa kwa upande wa *CAG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeongelea upande wa nyongeza ya fedha kwa upande wa *CAG*. Tukishamaliza bajeti hii tutakuwa na mashauriano ya Serikali na Kamati, kwa hiyo yale yote yanayohusisha nyongeza tumeyapokea na tutaenda kuyaandalia majibu kupitia mashauriano ambayo yatafanyika kati ya Kamati na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri kuhusu masuala ya fedha haramu, tumepokea ushauri kuhusu kufanya marejeo masuala ya pensheni, yote yale tumeyapokea na Naibu Waziri amejibu. Tumepokea maoni ya Mheshimiwa King yanayohusisha masuala ya mgao pamoja na mahusiano. Yote hayo yanafanyiwa kazi na yako hatua nzuri yatakapokuwa yamekamilika tutatoa kauli na yataenda moja kwa moja kwenye utekelezaji ambao utakuwa umeshafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya kimfumo, kazi kubwa inaendelea kwa upande wa mifumo ya *TRA* na kwa upande huu ambao Waheshimiwa Wabunge wameongea *ETS* na yenyewe yanafanyiwa kazi. Tunajua mifumo na yenyewe hawafanywi mara moja, kujenga mfumo si jambo la mara moja. Unatakiwa kutathimini aina ya mifumo, kusimika mifumo, kuweka mifumo iweze kusomana na hilo ndiyo jambo kubwa ambalo linafanyika hata lile alilosema Mheshimiwa Kishimba la dola tutalitolea kauli tunaposoma Hotuba kubwa, kwa sababu kazi yake kubwa imeendelea kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, alilolisema Mheshimiwa Katimba la suala la manunuzi, Sheria ya Manunuzi tunaileta upya, imeshasomwa kwa mara ya kwanza. Itakuja hapa na itajadiliwa

kwa mapana yake na tunaamini kwamba itakuwa na ushauri wote ule ambao Mheshimiwa Mbunge amesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameongelea Mheshimiwa Nusrat, masuala ya kodi na yenyewe nimeishasema tutayaongelea kwa mapana tutakapoleta kodi na lile alilosema kuhusu kutoa elimu. Tunatarajia tufanye semina kwanza kwa Waheshimiwa Wabunge, tuwaelezee haya masuala ya kodi na jinsi ambavyo yanawiana na maendeleo yetu na jinsi ambavyo inawiana, kwamba watu wengi sana wakilipa kodi itatuwezesha kupunguza ukubwa wa kodi. Kwa kadri wanavyolipa kodi watu wachache ndivyo tunavyofanya mzigo ule uwe mkubwa zaidi, kwa sababu unabebwa na wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa tumeshafanya semina Waheshimiwa Wabunge wakaelewa, tutaomba ninyi wenyewe ndiyo mkawe mabalozi kila mtu kwenye Jimbo lake kama tulivyofanya kwenye Sensa na tukaona mafanikio makubwa, yakajitokeza katika Sensa ile tuliyoifanya mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea yale ya Mheshimiwa Hasunga. Tumepokea yale ya *real time* ya Mheshimiwa Songe, Mbunge makini, tumepokea yale ya Mheshimiwa Swai, ya Mheshimiwa Kwagilwa nimeshajibu, ya Mheshimiwa Sillo Mwenyekiti wangu kabambe kabisa nimeshajibu, ya Mheshimiwa Hassan king nimeshajibu. Tumepokea yale ya *Hotel Levy* Mheshimiwa Kilumbe na tulikuwa kwenye zana na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Kwa sababu tutakuwa na mashauriano na tutaangalia upya haya masuala ya kikodi, niombe Wabunge waridhie kwamba yote hayo tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea hoja za Wabunge wote waliochangia kwa kuongea na wale waliochangia kwa maandishi na yote yale tutayafanyia kazi, kwa sababu bado tutakuwa na muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tujielekeze katika kitabu cha Pili - Matumizi ya Kawaida, Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango, ukurasa wa 453 na katika kishkwambi ni ukurasa wa 516.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………...........................Sh.13,497,566,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, kama nilivyosema Bunge Dini yake ni *time* na nilisema naongeza nusu saa na sasa ni muda wa *guillotine*. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………...........................Sh.13,497,566,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..............Sh.2,128,387,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*.............................Sh. 63,110,563,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*............................Sh. 2,142,412,000

Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*..Sh. 1,566,964,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*...............................Sh.1,411,252,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*.....Sh. 2,591,113,000
Kifungu 1010 – *Information and Communication Technology Unit*……........................……………....Sh. 0
Kifungu 3001 – *Internal Auditor General*.....................................Sh. 0
Kifungu 5001 – *Government Asset Management Division*…..........................................….Sh. 9,859,240,000
Kifungu 6001 – *Financial Management Information Systems Division*…...........................……Sh.10,516,478,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 01 – Deni la Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration*..........................Sh. 10,480,130,968,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 06 – Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani Wa Serikali**

Kifungu 2001 – *Quality Assurance*…………………....Sh. 5,892,574,000
Kifungu 2002 – *Technical Audit*……………….............................Sh.751,620,000
Kifungu 2003 – *Local Government Authorities Audit*………...…………..….Sh.1,028,780,000
Kifungu 2004 – *Ministries, Independent Departments and Audit*…........................................…Sh.1,160,470,000
Kifungu 2005 – *Risk Management Systems and Controls*…..........................................………Sh. 733,560,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……….......................Sh. 5,674,593,640
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*................Sh. 963,320,500

Kifungu 1003 – *Planning Unit*......................................Sh.1,294,858,400
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit* ..............................Sh. 933,804,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit* ........Sh.360,044,800
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Unit*…….........................Sh.1,265,780,000
Kifungu 1007 – *Information, Education and Communication Unit*......................................................Sh. 467,496,920
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit* ...............................Sh. 694,587,420
Kifungu 2001 – *Public Investment Management Division*…………..…….Sh.26,404,247,736
Kifungu 3001 – *Privatization and Monitoring*.............Sh.2,821,071,584
Kifungu 4001 – *Management Service Division*..........Sh.1,940,511,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Business Support Division*....................Sh.2,184,630,000
Kifungu 1002 – *Internal Audit Unit* .................................Sh.176,860,000
Kifungu 1003 – *Finance and Account Unit*...................Sh.306,500,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit* .................................Sh.37,140,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit* ..........Sh.72,260,000
Kifungu 2001 – *Technical Department*..........................Sh.395,800,000
Kifungu 2002 – *Zanzibar Office*........................................Sh.90,659,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Unit*…........................Sh.1,957,069,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..................Sh. 82,040,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*....................................Sh.14,450,000
Kifungu 1004 – *Monitoring and Analysis Unit*............... Sh.324,180,000
Kifungu 1005 – *Inspection Unit*......................................Sh.268,520,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit* ..........Sh.41,870,000
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*................................Sh.874,666,000

Kifungu 1008 – *Management Information Systems Unit*...........................................Sh.169,760,000
Kifungu 1009 – *Planning Unit*……………..……………..Sh.128,810,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 21 – Hazina**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*...............Sh.1,927,290,000
Kifungu 1009 – *Public Procurement Policy Unit (PPU)*…......................................…Sh.2,184,150,000
Kifungu 2001 – *Government Budget Division*.....Sh.1,791,659,551,550
Kifungu 2002 – *Policy Analysis Division*....................Sh.465,680,212,850
Kifungu 4001 – *External Finance Division*.................Sh. 68,403,602,500
Kifungu 4002 – *Public Private Partnership Unit* ..........Sh.2,131,919,000
Kifungu 5001 – *Financial Sector Development Division*................................................Sh. 6,543,220,500
Kifungu 6001 – *Debt Management Division*.............Sh.6,870,240,000
Kifungu 7001 – *Poverty Eradication Department*..........................Sh.0
Kifungu 8001 – *National Planning Division*...............Sh.10,967,032,600

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 22 – Huduma za Mfuko Mkuu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.............................Sh. 2,314,839,338,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3001 – *Consolidated Fund Services* ............Sh.1,015,002,874
Kifungu 3002 – *Expenditure Management*................Sh.4,844,490,000
Kifungu 3003 – *Financial Management*...................Sh.35,380,938,156
Kifungu 3004 – *Financial Operations and Standards*...................................Sh.9,287,342,970

Kifungu 3005 – *Sub Treasury Arusha*..............................Sh. 363,920,000
Kifungu 3006 – *Sub Treasury Coast*................................Sh.185,350,000
Kifungu 3008 – *Sub Treasury Iringa*.................................Sh.193,445,000
Kifungu 3009 – *Sub Treasury Kagera* .............................Sh.211,365,000
Kifungu 3010 – *Sub Treasury Kigoma* ............................Sh.234,180,000
Kifungu 3011 – *Sub Treasury Kilimanjaro*........................Sh.194,020,000
Kifungu 3012 – *Sub Treasury Lindi*..................................Sh. 224,690,000
Kifungu 3013 – *Sub Treasury Mara*.................................Sh.194,530,000
Kifungu 3014 – *Sub Treasury Mbeya* .............................Sh.184,940,000
Kifungu 3015 – *Sub Treasury Morogoro*........................Sh. 246,880,000
Kifungu 3016– *Sub Treasury Mtwara* .............................Sh.185,412,500
Kifungu 3017 – *Sub Treasury Mwanza* ..........................Sh.184,770,000
Kifungu 3018 – *Sub Treasury Rukwa*...............................Sh.184,880,000
Kifungu 3019 – *Sub Treasury Ruvuma*...........................Sh. 263,000,000
Kifungu 3020– *Sub Treasury Shinyanga*.........................Sh.184,070,000
Kifungu 3021 – *Sub Treasury Singida* ............................Sh.185,210,000
Kifungu 3022 – *Sub Treasury Tabora*.............................Sh.180,570,000
Kifungu 3023 – *Sub Treasury Tanga*..............................Sh. 207,415,000
Kifungu 3024 – *Sub Treasury Manyara*..........................Sh. 234,560,000
Kifungu 3025 – *Sub Treasury Njombe*...........................Sh. 238,230,000
Kifungu 3026 – *Sub Treasury Geita*.................................Sh.184,910,000
Kifungu 3027– *Sub Treasury Katavi*.................................Sh.185,050,000
Kifungu 3028 – *Sub Treasury Simiyu*...............................Sh. 212,510,000
Kifungu 3029 – *Sub Treasury Songwe*……………………Sh.182,520,000
Kifungu 3030 – *Sub Treasury Dar es Salaam*……….….Sh.349,120,000
Kifungu 4001 – *Local Government Finances* ………......Sh.986,830,000
Kifungu 7001 – *Pension and Gratuity*..........................Sh.1,276,933,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.......................Sh.17,207,356,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..............Sh.1,416,857,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*…...............................Sh. 455,377,450
Kifungu 1004 – *Ministerial Audit Division*...................Sh.10,241,768,000
Kifungu 1005 – *Local Government Authorities Division*..............................................Sh.18,421,138,000

Kifungu 1006 – *Performance Audits Division*.............Sh. 5,537,836,000
Kifungu 1007 – *National Account Division*................Sh. 5,862,018,000
Kifungu 1008 – *Technical Support Service Unit*.........Sh.8,135,646,000
Kifungu 1009 – *Public Authorities Audit Division*.......Sh. 6,045,393,000
Kifungu 1010 – *Planning, Monitoring & Evaluation Division*..............................Sh.1,894,829,000
Kifungu 1011 – *Procurement Management Unit*........Sh. 681,776,000
Kifungu 1012 – *Information and Communication Technology Unit*..................................Sh.3,767,545,000
Kifungu 1013 – *Forensic Audit Unit*............................Sh. 4,590,244,550
Kifungu 1014 – *Quality Assurance Unit*.......................Sh.1,166,421,000
Kifungu 1015 – *Government Communication Unit*......Sh.556,898,000
Kifungu 1016 – *Risk Management and Compliance Unit*…….......................…..…Sh.187,532,000
Kifungu 1017– *Legal Services Unit* .................................Sh.575,021,000
Kifungu 1018 – *Parliamentary Coordination Unit*.........Sh.978,740,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajielekeza katika Kitabu cha Nne – Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 06 – Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali

Kifungu 2001 – *Quality Assurance*..................................Sh.156,800,000
Kifungu 2002 – *Technical Audit*......................................Sh.34,150,000
Kifungu 2003 – *Local Government Authorities Audit*.....Sh.23,400,000
Kifungu 2004 – *Ministries, Independent Departments and Audit*…..............................................Sh.32,600,000
Kifungu 2005 – *Risk Management Systems and Control*..…....................................…Sh.113,050,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..................................Sh. 0
Kifungu 1003 – *Planning Unit*.........................................Sh.278,000,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit* ................................................Sh. 0
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit* .................................................Sh. 0
Kifungu 2001 – *Public Investment Management Division*....................................................Sh.286,470,000
Kifungu 3001 – *Privatization and Monitoring*................Sh.192,790,000
Kifungu 4001 – *Management Service Division*............Sh.182,740,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Unit*…...........................…Sh. 455,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 21 – Hazina**

Kifungu 1009 – *Public Procurement Policy Unit (PPU)*................................................Sh. 235,375,000
Kifungu 2001 – *Government Budget Division*.......Sh. 424,893,182,000
Kifungu 2002 – *Policy Analysis Division*.....................Sh.68,661,733,000
Kifungu 4001 – *External Finance Division*........................Sh.40,000,000
Kifungu 4002 – *Public Private Partnership Unit* .........Sh.2,820,000,000
Kifungu 5001 – *Financial Sector Development Division*….......................Sh.606,950,000
Kifungu 6001 – *Debt Management Division*.................Sh.300,000,000
Kifungu 8001 – *National Planning Division*...................Sh.199,335,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3003 – *Financial Management*.....................Sh.1,423,360,000
Kifungu 3004 – *Financial Operations and Standards*...................Sh. 0
Kifungu 4001 – *Local Government Finances* ...............Sh.274,320,000
Kifungu 7001 – *Pension and Gratuity*.............................Sh.182,320,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*…………..Sh. 7,328,000,000
Kifungu 1010 – *Planning, Monitoring and Evaluation Division*............................Sh.2,083,878,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…...............................….Sh.2,958,347,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*..............................Sh.52,875,572,000
Kifungu 1010 – *Information and Comm. Technology Unit*............Sh.0
Kifungu 3001 – *Internal Auditor General*........................................Sh.0
Kifungu 5001 – *Government Asset Management Division*.........................Sh.3,500,000,000
Kifungu 6001 – *Financial Management Information Systems Division*................................Sh. 3,500,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Hivyo naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2023/2024. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipnago kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Serikali kwa ujumla, lakini kwa leo lazima niwashukuru Wabunge, michango yenu imeonyesha ukomavu wenu, *very professional contributions* ambazo leo Wabunge mmetoa hapa. Sikusikia mtu anaulizia barabara wala *REA* kwenye Wizara, mara nyingi zamani watu wanakosea wanaleta mambo ya *REA*, barabara, visima, sijui majasho, majosho, sijui manini? *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tofauti leo wote waliyochangia wamezungumza hoja za msingi za majukumu ya hii Wizara, inaonyesha namna mnavyokomaa, inaonyesha namna sasa

mnaelewa kazi za Serikali na namna gani Serikali yetu inachapa kazi, hongereni sana. *(Makofi)*

Bajeti hii imepita rasmi, sasa Mheshimiwa Waziri kazi kwako, bado una bajeti ile kubwa ambayo Wabunge wanaingoja kwa hamu na baadhi ya michango ambayo leo iligusiwa ya Mifumo na Sera za Kodi uje utolee majibu kama mchango wa Mheshimiwa Nusrat, ni vitu muhimu sana hivi na wala havina gharama. Nashangaa sana, unasikia mtu anakuja mfumo sijui wa kodi dola milioni 200, hakuna kitu kama hicho *unless* na mimi nasikia vibaya. *(Makofi)*

Sasa, hili suala la *ETS* tulilizungumza sana toka awamu ile ya nyuma na kuachia *foreign entity* kuendeleza kufanya shughuli hii ni ku-*surrender tax regime* kwa *foreign entity* ambayo ni makosa. Hii kazi kwenye mkataba wa mwanzo ilikuwa lazima watoe *training* na baada ya muda fulani wana–*transfer* ili teknolojia kwa *local content*. Tukasema apewe *TCRA* au apewe *TTCL,* lakini tunaweza tukaja zaidi *TRA* Kidata unaweza ukafanya hiyo kitu, awe na kitengo chake, sababu miundombinu ya mfumo huu wanafanya wenye makampuni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, badala ya kugombana na watu wa vitenge, pesa zimo humu. Hebu Mheshimiwa Waziri mbadilike sasa. Hii kitu ifanywe na *TRA* wenyewe sababu kuna mambo mengi ya ujanja ujanja kuna stempu mbovu Serikali inajua? Serikali inapewa akaunti, lakini ndani ya akaunti mnahakikisha kweli ndiyo akaunti yenyewe? Nani anakwenda ku–*audit* hizo akaunti? Je, mimi kama ndiyo nina biashara yangu ya yakufanyiwa huo mfumo, halafu na-*conspire* sisemi kama nini kinafanyika, napewa akaunti ndogo Serikali mnajuaje? *(Makofi)*

Kwa hiyo, *TRA* sasa *it's high time* nyinyi wenyewe mwendeshe hii kitu, mapato yabaki kwenu na haya yaende kujenga nchi. Sasa hivi mnaona hii barabara kwa wale Waheshimiwa Wabunge, mkiingia mjini mshaona zile barabara zinavyochafuka sasa hivi kwa ma udongo na malami na sementi? Barabara hii ya Nyerere *road,* barabara mpya inavyojengwa, hii barabara inataka pesa na hizi pesa ndiyo hizi. Kwa hiyo tunampongeza Mama Samia kwa namna anavyoboresha

miundombinu, lakini tumsaidie Wabunge kwa kuweka maelekezo kwa Serikali, mapato yabaki hapa hapa ndani ya nchi. *(Makofi)*

Kuna tangazo la Katibu, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwa mujibu wa Kanuni ya 124 ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Februari, 2023 kuanzia kesho tarehe 8 Juni, 2023, Serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti watakuwa na Vikao vya Majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zenye maslahi kwa Taifa zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Makadirio ya Bajeti za Wizara.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 124(3) Wajumbe Kamati ya Uongozi kwa nafasi zao watakuwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti na hivyo watatakiwa kuhudhuria vikao hivyo. Katika kipindi hicho cha majumuisho Kanuni ya 124(2) inaelekeza kwamba Bunge litaendelea na shughuli zake nyingine kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya mkutano wa 11 wa Bunge ambao ipo kwenye vishikwambi vyenu.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.17 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 8 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*